CHEMBA YA TAIFA YA BIASHARA - TNCC

# HALI YA BIASHARA NA UWEKEZAJI TANZANIA

## Mtazamo wa Sekta Binafsi

NELSON URIO, KELVIN OGODO & MATINA NKURLU

© 2026

**NELSON URIO, KELVIN OGODO & MATINA NKURLU**

Nelson Urio: +255 688 482 721 | nelson.urio@tncc.or.tz

Kelvin Ogodo: +255 758 654 545 | kelvin.ogodo@tncc.or.tz

Matina Nkurlu: +255 754 710 099 | matina.nkurlu@tncc.or.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Huruhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa, kutafsiri au kutoa sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa njia yeyote bila idhini ya mwandishi.

Book Typesetting: Lamax Designs | +255 764 793 105

# YALIYOMO

**1. ORODHA YA VIFUPISHO** ---------- **v**

**DIBAJI** ---------- **vii**

**SHUKRANI** ---------- **ix**

**MUHTASARI** ---------- **xi**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ---------- **1**

1.1. Usuli ---------- 1

1.2. Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC) ---------- 2

1.3. Malengo ya Tathmini ---------- 3

**SURA YA PILI: HALI YA BIASHARA NA UWEKEZAJI KIMKOA** ---------- **4**

2.1. Mkoa wa Dar es Salaam ---------- 5

2.2. Mkoa wa Pwani ---------- 6

2.3. Mkoa wa Lindi ---------- 9

2.4. Mkoa wa Mtwara ---------- 11

2.5. Mkoa wa Morogoro ---------- 13

2.6. Mkoa wa Dodoma ---------- 14

2.7. Mkoa wa Singida ---------- 16

2.8. Mkoa wa Tabora ---------- 18

2.9. Mkoa wa Shinyanga ---------- 20

2.10. Mkoa wa Kagera ---------- 22

2.11. Mkoa wa Geita ---------- 24

2.12. Mkoa wa Mwanza ---------- 26

2.13. Mkoa wa Simiyu ---------- 29

2.14. Mkoa wa Mara ---------- 31

2.15. Mkoa wa Kigoma ---------- 33

2.16. Mkoa wa Katavi ---------- 35

2.17. Mkoa wa Rukwa ---------- 38

2.1. Mkoa wa Songwe ---------- 39

2.19. Mkoa wa Ruvuma ---------- 42

2.20. Mkoa wa Arusha ---------- 44
2.21. Mkoa wa Iringa ---------- 46
2.22. Mkoa wa Kilimanjaro ---------- 48
2.23. Mkoa wa Manyara ---------- 50
2.24. Mkoa wa Mbeya ---------- 53
2.25. Mkoa wa Njombe ---------- 55
2.26. Mkoa wa Tanga ---------- 58
**SURA YA TATU: UCHAMBUZI WA TATHMINI ---------- 61**
3.1. Juhudi za Serikali katika Kuboresha Mazingira ya Biashara ---------- 61
3.2. Changamoto zinazokabili Biashara na Uwekezaji ---------- 63
3.3. Fursa za Biashara na Uwekezaji ---------- 65
**SURA YA NNE: MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ---------- 68**
4.1. Mapendekezo ya Kiutendaji au Kiutawala ---------- 68
4.2. Mapendekezo kwa serikali za mitaa ---------- 81
4.3. Mapendekezo ya sera ---------- 85
4.4. Hitimisho ---------- 90

# 1. ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AfCFTA | Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika |
| BOT | Benki Kuu ya Tanzania |
| BRELA | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni |
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| DSE | Soko la Hisa la Dar es Salaam |
| EABC | Baraza la Biashara la Afrika Mashariki |
| EACCIA | Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Afrika Mashariki |
| EAC | Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| EFD | Mashine ya Kielektroniki ya Kutolea Risiti |
| EPZ | Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Ajili ya Mauzo ya Nje |
| FDI | Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje |
| FYDP | Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
| GCLA | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali |
| GDP | Pato la Taifa |
| HS Code | Namba ya Mfumo wa Kimataifa wa Uainishaji wa Bidhaa |
| ICC | Chemba ya Biashara ya Kimataifa |
| ICT / TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| ILO | Shirika la Kazi Duniani |
| IMF | Shirika la Fedha la Kimataifa |
| ISO | Shirika la Kimataifa la Viwango |
| LGA | Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| MIT | Wizara ya Viwanda na Biashara |
| MSME | Biashara Ndogo, Ndogo za Kati na za Kati |
| NBS | Ofisi ya Taifa ya Takwimu |
| NEMC | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
| NGO | Shirika Lisilo la Kiserikali |
| NTBs | Vikwazo Visivyo vya Kodi |
| OSHA | Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi |
| PACCI | Chemba ya Biashara na Viwanda ya Afrika |
| PPP | Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi |
| PSI | Ukaguzi wa Mizigo Kabla ya Kusafirishwa |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika |
| SIDA | Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden |
| SME | Biashara Ndogo na za Kati |
| TADB | Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania |

| | |
|---|---|
| TAEC | Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TANROADS | Wakala wa Barabara Tanzania |
| TASAC | Wakala wa Usafiri wa Meli Tanzania |
| TBS | Shirika la Viwango Tanzania |
| TCCIA (zamani) | Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (Jina la zamani la TNCC) |
| TNCC | Chemba ya Taifa ya Biashara |
| TFS | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania |
| TIC | Kituo cha Uwekezaji Tanzania |
| TIN | Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi |
| TIRDO | Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania |
| TISEZA | Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi na Uwekezaji Tanzania |
| TPA | Mamlaka ya Bandari Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TPSF | Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania |
| UN | Umoja wa Mataifa |
| UNIDO | Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa |
| USAID | Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani |
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| WCF | Shirikisho la Kimataifa la Mabaraza ya Biashara |
| WMA | Wakala wa Vipimo |
| WTO | Shirika la Biashara Duniani |

# DIBAJI



Kitabu cha Hali ya Biashara na Uwekezaji Nchini Tanzania: Mtazamo wa Sekta Binafsi kinatoa tathmini ya malengo na matokeo ya ziara za viongozi wa TNCC katika mikoa ya Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na maendeleo ya sekta binafsi. Kitabu hiki kimegawanywa katika Sura Nne ambapo kila moja ina mtazamo wa kipekee. Sura ya kwanza inaelezea historia, madhumuni, na malengo ya ziara. Sura ya pili inafafanua hali ya biashara katika mikoa tofauti, ikieleza kwa undani fursa na changamoto za sekta ya biashara na viwanda. Pia, Sura ya tatu inatoa tathmini ya jitihada za serikali katika kuweka mazingira bora, fursa na changamoto za biashara. Mwisho, Sura ya nne inatoa mapendekezo ya kiutendaji, kiutawala, na kisera ambayo yanaweza kusaidia kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Kwa hiyo, kitabu kimejikita katika kuangazia changamoto na fursa zinazokabili sekta za biashara na uwekezaji, pamoja na kutoa mapendekezo ya mikakati ya kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa. Kupitia ziara hizo, TNCC ilikusudia kubaini changamoto zinazokabili wafanyabiashara na wawekezaji. Changamoto hizo ni pamoja na kodi na tozo kubwa, urasimu katika kupata huduma, ukosefu wa miundombinu bora, na ukosefu wa mikopo yenye masharti nafuu. Aidha, tathmini hii imeelezea umuhimu wa kuimarisha mfumo wa elimu kwa wadau wa sekta binafsi kuhusu sera na taratibu za serikali ili kuwarahisishia kufanya biashara kwa ufanisi na kuepuka migongano na mamlaka za serikali.

Kitabu kinatilia mkazo pia fursa mbalimbali zinazopatikana katika sekta za kilimo, ufugaji, viwanda, na biashara katika mikoa ya mipakani. Fursa hizo zinajumuisha uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji, usindikaji wa mazao ya kilimo, ufugaji wa samaki, na biashara ya mipakani. TNCC imetoa mapendekezo mahsusi ya kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa nia ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara na kukuza uchumi.

Kwa kuzingatia maoni ya wadau wa sekta binafsi waliotembelewa, kitabu hiki kinalenga kuwasilisha na kutoa mwanga mpya kuhusu njia bora za kuchochea maendeleo ya sekta binafsi na kuchangia kwa ufanisi zaidi katika kukuza uchumi wa taifa. Aidha, kitabu kinaonesha namna ambavyo

serikali imejidhatiti kupitia sera na mipango mbalimbali ya maendeleo, hatua zinazolenga kutoa vivutio kwa wawekezaji, kuboresha miundombinu, na kuweka mazingira rafiki ya biashara.

Kwa kutambua mchango wa serikali na wadau wengine, kitabu hiki kinatoa mwito wa ushirikiano zaidi ili kuhakikisha changamoto zinazokabili sekta za uchumi zinashughulikiwa kwa ufanisi. Kwa ujumla, kitabu hiki ni mwongozo muhimu kwa wadau wote wa sekta ya biashara. Ni matumaini ya TNCC kwamba kitabu hiki kitachangia kuboresha mazingira ya biashara na kuwezesha Tanzania kufikia maendeleo endelevu ya kiuchumi kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Vicent Bruno Minja.
Rais - Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC)

# SHUKRANI



Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC) ina miaka 37 ya uendeshaji wa shughuli za kuishauri serikali ya Tanzania ili kuboresha na kuimarisha mazingira ya sekta binafsi. Hivyo basi, TNCC inatekeleza majukumu mbalimbali, ikiwemo kutoa huduma za taarifa kwa wafanyabiashara na wawekezaji wanaotafuta taarifa sahihi na za kuaminika.

Chemba inachangia kuimarisha mazingira bora ya biashara kwa kushiriki katika utetezi wa sekta binafsi nchini. Chemba hushawishi ngazi mbalimbali za serikali ili kukuza na kulinda maslahi ya biashara na uwekezaji. Pia, inarahisisha biashara kwa kutoa vyeti vya uasili wa bidhaa. Jukumu jingine la Chemba ni kuratibu mikutano ya mitandao kwa kutoa jukwaa la kushirikiana kati ya biashara kwa biashara na vitengo vya serikali. Aidha, Chemba pia inarahisisha safari za kibiashara na maonesho kwa kuandaa misafara ya kibiashara kwenda nchi za kigeni kwa madhumuni ya kuunganisha au kuwezesha upatikanaji wa masoko na mahusiano ya biashara kwa jamii ya wafanyabiashara wa Tanzania.

Mbali na kuendelea kwetu kusaidia sekta binafsi, Chemba pia imejipanga katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22–2025/26. Sekta binafsi ina matumaini makubwa kwa bajeti ya mwaka 2024/2025 kwani inaakisi mambo muhimu katika harakati zake za maendeleo tunapoelekea ukingoni mwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) (2021/2022–2025/2026). Sekta binafsi ni mdau wa kitaifa ambaye anaendelea kuimarika kila wakati na anapaswa kuendelea kuchukua jukumu kubwa katika maendeleo ya nchi. Katika maendeleo ya kiuchumi, baadhi ya dhana zitaathiri hali ya kiuchumi, na baadhi ya dhana hizo zinaweza kujumuishwa katika uundaji na utekelezaji wa bajeti za kitaifa. Hata hivyo, baadhi ya mambo yanayohitajika ili kuchochea sekta binafsi kutoa matokeo muhimu yanategemea mazingira mazuri yanayolenga kuboresha sekta binafsi. Zaidi ya hayo, sekta binafsi inahitaji vichocheo vinavyoiwezesha kufanya kazi kwa ufanisi na kutumia motisha ambazo zitakuza biashara na uwekezaji wa siku zijazo.

Ili kufikia lengo hili, timu ya viongozi na wataalamu wa Chemba, ikiongozwa na rais wake, iliazimia kutembelea mikoa 26 ya Tanzania Bara ikiwa na malengo yafuatayo:

(i) Kufanya tathmini ya ufanisi na uendeshaji wa shughuli mbalimbali za TNCC katika ngazi za mikoa na wilaya husika;

(ii) Kukuza uhusiano wa karibu na serikali kuu kupitia ofisi za wakuu wa mikoa, ili kushirikiana katika kukuza sekta ya biashara na uwekezaji;

(iii) Kufanya tathmini ya hali ya wanachama wa TNCC katika ngazi za mikoa na wilaya; (iv) Kutazama fursa zilizopo mikoani na kuwasiliana moja kwa moja kuhusu fursa hizo, ili wawekezaji wazawa wazitumie kwa ufanisi na kikamilifu; na

(v) Kutazama changamoto za kibiashara zilizopo mikoani na kuweza kutoa mapendekezo ili kuweka mazingira bora kwa wafanyabiashara.

Matokeo ya ziara hizo yatachangia katika mchakato wa kufikia mpango wa serikali endapo mambo yaliyoibuliwa yatashughulikiwa ipasavyo. Daima tunapaswa kuweka akilini kuwa mazingira ya biashara hubadilika mara kwa mara, hivyo ni muhimu sana kwa Chemba kufanya tathmini mara kwa mara ili kubaini fursa zinazoibuka na kuondoa changamoto ili kukuza sekta binafsi.

Ninapenda kutoa shukrani zangu kwa wadau wote, wakiwemo wakuu wa mikoa, viongozi wote wa serikali, na wafanyabiashara kwa maoni yao muhimu na muda wao ambao umeisaidia Chemba kuja na kitabu hiki. Shukrani pia ziende kwa wataalamu wetu kwa mchango wao katika uandishi wa kitabu hiki. Mwisho, na siyo kwa umuhimu, ninawashukuru sana Bodi ya TNCC na timu ya uandishi wa kitabu kwa juhudi zao zisizo na mwisho katika kuandika na kukamilisha kitabu hiki. Kwa kushirikiana kwa karibu na serikali na wadau wengine, tunaweza kufikia maendeleo endelevu ya sekta binafsi na kuboresha kiwango cha maisha cha Watanzania.

Ninaamini kwa dhati kuwa tunaweza kufanya zaidi, kufanya vizuri zaidi, na kufika mbali zaidi kwa kutumia rasilimali chache na fursa tulizonazo hapa Tanzania.



Oscar Kissanga
Afisa Mtendaji Mkuu
Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC)

# MUHTASARI

Kitabu hiki, Hali ya Biashara na Uwekezaji Nchini Tanzania: Mtazamo wa Sekta Binafsi, ni matokeo ya tathmini ya kitaifa iliyofanywa na Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC) kupitia ziara za viongozi na wataalamu wake katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Lengo kuu la tathmini hii lilikuwa kupata picha halisi, ya kina, na yenye ushahidi wa moja kwa moja kuhusu mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, kwa kuzingatia uzoefu wa wafanyabiashara, wawekezaji, na wadau wa sekta binafsi katika ngazi za mikoa na wilaya.

Tathmini hii imefanyika katika kipindi ambacho Tanzania inaendelea kutekeleza sera na mipango ya mageuzi ya kiuchumi yenye lengo la kujenga uchumi wa kati unaotegemea viwanda, biashara shindani, na ushiriki mpana wa sekta binafsi. Katika muktadha huu, sekta binafsi ina nafasi muhimu kama injini ya ukuaji wa uchumi, chanzo cha ajira, mapato ya serikali, na kichocheo cha ubunifu na uongezaji thamani wa rasilimali za taifa. Hata hivyo, uwezo wa sekta binafsi kuchangia kikamilifu hutegemea ubora wa mazingira ya biashara na uwekezaji yanayojumuisha sera, sheria, mifumo ya udhibiti, kodi na tozo, pamoja na upatikanaji wa miundombinu na huduma za umma.

Kupitia ziara hizo, TNCC ilifanya mazungumzo na wakuu wa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, taasisi za umma, wanachama wa Chemba, wafanyabiashara, wakulima, wachimbaji, wavuvi, wenye viwanda, na wawekezaji wa sekta mbalimbali. Aidha, timu ilitembelea viwanda, miradi ya uwekezaji, masoko, na maeneo ya uzalishaji ili kushuhudia kwa vitendo hali halisi ya uendeshaji wa biashara, gharama za uzalishaji, upatikanaji wa huduma za umma, na changamoto za miundombinu. Mbinu hii ilihakikisha kuwa mapendekezo yaliyotolewa yanatokana na ushahidi wa moja kwa moja na uzoefu halisi wa wadau wa sekta binafsi.

Kwa ujumla, tathmini imebaini kuwa Tanzania ina fursa nyingi za kiuchumi katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, biashara ya mipakani, uchumi wa buluu, na huduma. Mikoa mingi ina rasilimali za asili, nguvu kazi, na nafasi ya kijiografia inayoweza kuchochea uwekezaji na uzalishaji wa bidhaa zenye ushindani katika masoko ya ndani, kikanda, na kimataifa. Fursa hizi zinajumuisha kilimo cha umwagiliaji, usindikaji wa mazao, ufugaji wa samaki, uchimbaji na uongezaji thamani wa madini, pamoja na ukuzaji wa viwanda vidogo na vya kati vinavyounganishwa na minyororo ya thamani ya kikanda.

Pamoja na fursa hizo, kitabu kimeainisha changamoto kadhaa zinazokwamisha ukuaji wa biashara na uwekezaji. Changamoto kuu zilizojitokeza mara kwa mara katika mikoa mingi ni pamoja na wingi na uzito wa kodi na tozo mbalimbali, tafsiri na utekelezaji usio sawia wa sheria na kanuni, urasimu na ucheleweshaji wa utoaji wa huduma, gharama kubwa za uzalishaji, pamoja na upungufu wa miundombinu bora ya barabara, nishati, masoko, na maghala. Wadau pia walieleza changamoto za upatikanaji wa mitaji nafuu, elimu ndogo kuhusu sera na taratibu za kibiashara, pamoja na ukosefu wa uratibu thabiti kati ya taasisi za udhibiti.

Maeneo maalum ya kisekta yalibainisha changamoto za kipekee. Katika kilimo, masuala ya mfumo wa stakabadhi ghalani, bei zisizoeleweka mapema kwa wakulima, na upungufu wa miundombinu ya umwagiliaji yalitajwa kama vikwazo vya kuongeza tija na mapato ya wakulima. Katika biashara na masoko, wafanyabiashara walilalamikia ushuru wa huduma katika halmashauri mbalimbali, utofauti wa viwango vya tozo kati ya maeneo, pamoja na urasimu katika forodha na usimamizi wa mizigo. Sekta ya uvuvi ilikabiliwa na changamoto za miundombinu ya mialo, leseni na tozo, wakati sekta ya viwanda ilieleza gharama kubwa za uzalishaji, ukosefu wa vifungashio vya ndani, na ucheleweshaji wa malipo kwa wazabuni wa ndani.

Kwa upande wa taasisi, tathmini pia ilichunguza uwezo wa kimuundo na kiutendaji wa TNCC katika ngazi za mikoa na wilaya. Imebainika kuwa Chemba ina mtandao mpana unaoiwezesha kufikia wadau wengi wa sekta binafsi, lakini kuna haja ya kuimarisha zaidi ofisi za mikoa na wilaya ili ziwe na uwezo mkubwa wa kutoa huduma kwa wanachama, kukusanya na kuwasilisha hoja za wafanyabiashara, na kushiriki kikamilifu katika majukwaa ya maendeleo ya kiuchumi ya maeneo husika. Hii itaongeza ufanisi wa Chemba kama sauti ya sekta binafsi katika mijadala ya sera na maboresho ya mazingira ya biashara.

Kutokana na uchambuzi wa changamoto na fursa hizo, kitabu kinatoa mapendekezo ya kina katika ngazi tatu kuu: kiutendaji/kiutawala, serikali za mitaa, na kisera. Mapendekezo haya yanahusu kurahisisha taratibu za utoaji huduma, kupunguza urasimu na mwingiliano wa taasisi, kuboresha miundombinu ya uzalishaji na masoko, kuimarisha elimu ya walipa kodi na wafanyabiashara kuhusu sheria na taratibu, pamoja na kufanya maboresho ya sera na sheria ili kuleta uwiano na utabirikaji katika mazingira ya biashara. Mapendekezo pia yanasisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kupanga na kutekeleza mikakati ya maendeleo ya kiuchumi.

Kwa hitimisho, kitabu hiki ni nyenzo muhimu ya ushahidi inayowasilisha sauti na uzoefu wa sekta binafsi kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania. Kinatoa msingi wa mazungumzo ya kisera kati ya serikali na sekta binafsi kwa lengo la kujenga mazingira rafiki zaidi ya biashara na uwekezaji yatakayochochea ukuaji jumuishi wa uchumi, ajira, mapato ya serikali, na ustawi wa wananchi. Kupitia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa, Tanzania ina nafasi kubwa ya kuimarisha ushindani wake wa kikanda na kimataifa na kuhakikisha sekta binafsi inakuwa mhimili mkuu wa maendeleo endelevu ya taifa.

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.1. Usuli

Biashara na uwekezaji ni injini kuu za ukuaji wa uchumi wa Tanzania na msingi wa mageuzi kuelekea uchumi wa kati wenye ushindani wa kikanda na kimataifa. Kupitia biashara na uwekezaji, rasilimali za taifa hubadilishwa kuwa bidhaa na huduma zenye thamani ya kiuchumi, hivyo kuongeza uzalishaji wa taifa, mapato ya serikali, na uwezo wa nchi kushiriki kikamilifu katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa. Kadiri biashara na uwekezaji vinavyokua, ndivyo uwezo wa uchumi wa Tanzania wa kuzalisha ajira, kuongeza mapato ya wananchi, na kupanua wigo wa shughuli za uzalishaji unavyoongezeka. Uwekezaji wa ndani na wa nje huongeza uwezo wa nchi kuzalisha kwa kiwango kikubwa zaidi na kwa tija zaidi, huku biashara ikihakikisha kuwa bidhaa na huduma zinazozalishwa zinafika katika masoko ya ndani, kikanda, na ya kimataifa. Mzunguko huu wa uwekezaji na biashara huongeza mapato ya kigeni, hupunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje, na huimarisha uthabiti wa mizania ya malipo ya taifa.

Kwa mtazamo wa kijamii, biashara na uwekezaji ni chanzo kikuu cha ajira na kipato kwa mamilioni ya Watanzania. Miradi ya uwekezaji katika uzalishaji, usindikaji, huduma, na miundombinu huunda nafasi za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, huku ukuaji wa biashara ndogo, za kati, na kubwa ukiimarisha mnyororo mzima wa ugavi unaojumuisha wazalishaji, wasambazaji, wauzaji, na watoa huduma. Kupitia mnyororo huu, biashara na uwekezaji huongeza ushiriki wa wananchi katika uchumi rasmi, huongeza mapato ya kaya, na hivyo kuchangia kupunguza umaskini na kukuza ustawi wa jamii. Wawekezaji huleta mitaji, maarifa ya usimamizi, viwango vya kimataifa, na teknolojia ambazo huongeza tija na ushindani wa uchumi wa ndani. Kadri mazingira ya biashara yanavyoboreshwa, ndivyo Tanzania inavyovutia zaidi uwekezaji wa kimkakati unaolenga kuongeza thamani ya uzalishaji, kukuza mauzo ya nje, na kuunganisha uchumi wa taifa katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa.

Hata hivyo, uwezo huu mkubwa wa biashara na uwekezaji kuchochea maendeleo ya taifa hutegemea sana ubora wa mazingira ya biashara na uwekezaji. Sera, sheria, mifumo ya taasisi, taratibu za udhibiti, kiwango cha kodi na tozo, pamoja na ubora wa huduma na miundombinu vinaathiri moja kwa moja maamuzi ya wawekezaji na ufanisi wa wafanyabiashara.

Mazingira yasiyotabirika, gharama kubwa za uendeshaji, urasimu, na ukosefu wa uwiano wa kitaasisi vinaweza kudhoofisha uwekezaji na kupunguza kasi ya ukuaji wa biashara, hata pale fursa za kiuchumi zinapokuwepo.

Ni katika muktadha huu ndipo Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC), kwa kutambua nafasi yake kama sauti ya sekta binafsi, iliona umuhimu wa kufanya tathmini ya kitaifa ya hali ya biashara na uwekezaji nchini. Tathmini hii ililenga kupata picha halisi ya mazingira ya biashara kutoka kwa wafanyabiashara na wawekezaji katika mikoa yote ya Tanzania Bara, kwa kuangalia kwa kina uzoefu wao kuhusu sera, kanuni, tozo, huduma za umma, miundombinu, na mifumo ya utekelezaji. Matokeo ya tathmini hii ndiyo msingi wa toleo la kwanza la kitabu cha "Hali ya Biashara na Uwekezaji Nchini Tanzania: Mtazamo wa Sekta Binafsi", ambacho kinakusudia kutoa ushahidi wa kitaalamu na wa vitendo utakaosaidia maboresho ya sera na utekelezaji kwa ajili ya kukuza biashara na uwekezaji endelevu nchini.

## 1.2. Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC)

Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC), iliyokuwa ikijulikana kama Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), ni taasisi ya sekta binafsi iliyoanzishwa mwaka 1988 kwa msaada wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuimarisha, kuwakilisha, na kukuza maendeleo ya sekta binafsi nchini. Chemba hii ilianzishwa katika kipindi muhimu cha mageuzi ya kiuchumi ambapo Tanzania ilikuwa inatoka kwenye mfumo wa uchumi unaotawaliwa na umiliki na uendeshaji wa serikali, kuelekea kwenye uchumi wa soko huria na wa mchanganyiko unaotoa nafasi kubwa kwa biashara na uwekezaji wa sekta binafsi.

TNCC ilianzishwa kama jukwaa rasmi la sauti ya wafanyabiashara, wawekezaji, na wajasiriamali wa Kitanzania ili kuwezesha ushiriki wao katika mijadala ya sera, kuboresha mazingira ya biashara, na kuimarisha ushindani wa uchumi wa taifa. Tangu kuanzishwa kwake, Chemba imeendelea kufanya kazi kwa karibu na serikali katika ngazi zote pamoja na wadau wa maendeleo, ikilenga kujenga mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji yanayochochea ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu.

Kwa kipindi kirefu, TNCC imekuwa mshirika muhimu wa mashirika ya maendeleo ya kimataifa katika kutekeleza miradi ya kuimarisha sekta binafsi. Miongoni mwa wadau wakuu waliounga mkono juhudi hizi ni Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Kiswidi (SIDA), ambalo lilitoa mchango mkubwa

katika uanzishaji na uimarishaji wa Chemba za mikoa na wilaya kupitia mafunzo ya uongozi na uendeshaji, utoaji wa vifaa vya ofisi, pamoja na uhamasishaji na elimu kwa jamii ya wafanyabiashara. Msaada huu uliwezesha TNCC kujenga mtandao wa kitaifa unaofikia mikoa yote ya Tanzania Bara, hivyo kuifanya Chemba kuwa taasisi inayowakilisha kwa upana maslahi ya sekta binafsi nchini.

Kimataifa na kikanda, TNCC ina nafasi ya kipekee katika uwakilishi wa Tanzania katika jumuiya za biashara. Ni mwanachama pekee wa Baraza la Biashara la Kimataifa (International Chamber of Commerce – ICC) nchini Tanzania, hali inayoiwezesha kuwakilisha maslahi ya wafanyabiashara wa Tanzania katika majukwaa ya kimataifa ya biashara, uwekezaji, na sera za uchumi. Aidha, TNCC ni mwanachama hai wa taasisi muhimu za kikanda na bara la Afrika, ikiwemo East African Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (EACCIA), Pan African Chamber of Commerce and Industry (PACCI), pamoja na East African Business Council (EABC). Ushiriki huu unaipa TNCC uwezo wa kuunganisha sekta binafsi ya Tanzania na fursa za biashara, masoko, na mijadala ya sera katika ukanda wa Afrika Mashariki na bara la Afrika kwa ujumla.

Kupitia mtandao wake wa kitaifa na ushiriki wake wa kikanda na kimataifa, TNCC inafanya kazi kama kiunganishi muhimu kati ya wafanyabiashara, wawekezaji, serikali, na jumuiya ya kimataifa kwa lengo la kukuza biashara, kuvutia uwekezaji, na kuboresha ushindani wa uchumi wa Tanzania.

## 1.3. Malengo ya Tathmini

Tathmini ya Kitaifa ya Hali ya Biashara na Uwekezaji iliyoendeshwa na Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC) kupitia ziara zake katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ilikuwa na lengo kuu la kupata picha halisi na ya kina ya mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, kwa mtazamo wa moja kwa moja wa sekta binafsi. Tathmini hii ililenga si tu kukusanya taarifa za jumla, bali pia kuelewa kwa undani changamoto, fursa, na uwezo wa taasisi na mifumo inayosimamia biashara na uwekezaji katika ngazi za kitaifa, mikoa, na wilaya.

Kwanza, tathmini hii ililenga kufanya tathmini ya kina ya hali ya biashara na uwekezaji katika mikoa na wilaya, kwa kuangalia kiwango cha ushiriki wao, changamoto wanazokabiliana nazo katika uendeshaji wa biashara na uwekezaji, upatikanaji wa huduma za serikali, masuala ya kodi na tozo, pamoja na upatikanaji wa masoko, mitaji, na miundombinu. Hii ilisaidia

kupata ushahidi wa moja kwa moja wa uzoefu halisi wa sekta binafsi katika mazingira ya biashara ya Tanzania.

Pili, kupitia ziara za kutembelea viwanda, biashara, na miradi ya uwekezaji katika maeneo husika, TNCC ililenga kupata ushahidi wa vitendo kuhusu hali halisi ya uzalishaji, uendeshaji wa biashara, upatikanaji wa huduma za umma, changamoto za miundombinu, gharama za uzalishaji, pamoja na fursa zilizopo kwa ajili ya kuongeza thamani na ushindani wa bidhaa za Tanzania.

Tatu, tathmini ililenga kuchunguza na kuthibitisha uhai wa kimuundo na kitaasisi wa TNCC katika ngazi za mikoa na wilaya, kwa kuangalia uwezo wa ofisi za Chemba katika kutoa huduma kwa wanachama, kuwakilisha maslahi ya sekta binafsi, na kushiriki kikamilifu katika majukwaa ya maendeleo ya kiuchumi ya kanda. Kupitia tathmini hii, TNCC ilikusudia kubaini nguvu, udhaifu, na mapungufu katika uendeshaji wa mtandao wake wa kitaifa ili kuboresha utendaji wake na kuimarisha nafasi yake kama sauti ya sekta binafsi.

Nne, tathmini ilikusudia kuimarisha na kupanua mahusiano ya kikazi kati ya TNCC na serikali kuu pamoja na mamlaka za mikoa na wilaya, kwa lengo la kuweka msingi thabiti wa ushirikiano katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Kupitia mikutano na wakuu wa mikoa na viongozi wa serikali za mitaa, TNCC ililenga kujenga maelewano ya pamoja kuhusu changamoto zinazokumba wafanyabiashara, utekelezaji wa sera na kanuni, pamoja na fursa za ushirikiano katika kuhamasisha uwekezaji na uzalishaji.

Kwa ujumla, malengo ya tathmini hii yalikuwa kuweka msingi wa kitaalamu na wa ushahidi wa vitendo kwa ajili ya kuandaa mapendekezo ya sera, maboresho ya kisheria na kiutendaji, pamoja na mikakati ya kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa manufaa ya sekta binafsi na uchumi wa taifa kwa ujumla.

## 2.1. Mkoa wa Dar es Salaam

Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo kitovu kikuu cha biashara, uwekezaji, na huduma za kifedha nchini Tanzania. Licha ya kuchukua chini ya asilimia moja ya eneo la ardhi ya Tanzania Bara, mkoa huu unachangia zaidi ya asilimia 16 ya Pato la Taifa (GDP) na zaidi ya asilimia 40 ya mapato yote ya kodi ya ndani, jambo linaloonesha uzito wake wa kipekee katika uchumi wa taifa. Zaidi ya asilimia 60 ya viwanda vikubwa na vya kati nchini vinapatikana Dar es Salaam, na mkoa huu ndio lango kuu la biashara ya kimataifa kupitia Bandari ya Dar es Salaam, inayohudumia takribani asilimia 90 ya biashara ya nje ya Tanzania pamoja na nchi zaidi ya nane zisizo na bandari katika ukanda wa Afrika ya Kati na Kusini.

Kwa mujibu wa Blueprint Impact Assessment Report (2024), Dar es Salaam ndiyo mkoa wenye mkusanyiko mkubwa zaidi wa mitaji ya sekta binafsi, shughuli za kifedha, usafirishaji, na biashara za huduma. Mkoa huu unachangia zaidi ya asilimia 70 ya mikopo yote ya kibiashara inayotolewa na benki nchini, hali inayoonesha nafasi yake kama injini ya uwekezaji na mtaji wa biashara. Aidha, zaidi ya nusu ya kampuni zote zilizosajiliwa BRELA zina makao yao makuu Dar es Salaam, ikionyesha kuwa sera, kanuni, na mazingira ya biashara katika mkoa huu yanaathiri moja kwa moja mwenendo wa uchumi wa taifa zima.

Dar es Salaam pia ni kitovu cha mifumo ya kidijitali ya biashara, ikijumuisha Benki Kuu ya Tanzania, Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Mamlaka za Mapato (TRA), BRELA, na taasisi nyingi za kifedha na bima. Blueprint Impact Assessment Report (2024) inaonesha kuwa zaidi ya asilimia 80 ya miamala ya biashara ya kielektroniki ya kitaifa hupitia taasisi na mifumo iliyoko Dar es Salaam, jambo linaloufanya mkoa huu kuwa uti wa mgongo wa mageuzi ya kidijitali ya biashara nchini.

Hata hivyo, ripoti ya Blueprint pia inaonesha kuwa gharama za kufanya biashara Dar es Salaam ni miongoni mwa gharama kubwa zaidi nchini, hasa kutokana na msongamano wa bandari, ucheleweshaji wa forodha, urasimu wa leseni, kodi za awali, na gharama za ardhi na miundombinu. Takwimu za tathmini zinaonesha kuwa ucheleweshaji wa mizigo bandarini na katika mifumo ya forodha unaweza kuongeza gharama za biashara kwa kati ya asilimia 15 hadi 25 ya thamani ya mzigo, hali inayopunguza ushindani wa wafanyabiashara wa Tanzania katika soko la kikanda na kimataifa.

Aidha, Dar es Salaam ni mkoa unaovutia zaidi ya asilimia 35 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje (FDI) unaoingia Tanzania, hasa katika

sekta za bandari, viwanda, huduma za kifedha, mali isiyohamishika, TEHAMA, na biashara ya jumla. Blueprint Impact Assessment Report (2024) inabainisha kuwa karibu miradi yote mikubwa ya kimkakati ya sekta binafsi nchini huanza au kusimamiwa kutoka Dar es Salaam, hata pale uzalishaji unapotokea mikoani.

Kwa mtazamo wa mazingira ya sera na kanuni, Dar es Salaam ndiyo mkoa unaohisi kwa haraka zaidi athari za mabadiliko ya kodi, ada, leseni, na taratibu za udhibiti. Blueprint Impact Assessment inaonesha kuwa zaidi ya asilimia 65 ya malalamiko ya sekta binafsi kuhusu urasimu, kodi, tozo, na vibali huanzia au hujikita Dar es Salaam, si kwa sababu mkoa huu una matatizo pekee, bali kwa sababu ndiko kuna mkusanyiko mkubwa zaidi wa shughuli rasmi za biashara nchini.

Kwa msingi huo, tathmini ya TNCC katika Mkoa wa Dar es Salaam ina uzito wa kitaifa, kwani changamoto na mafanikio yanayoonekana hapa huathiri moja kwa moja ushindani wa Tanzania katika biashara ya kikanda na kimataifa. Dar es Salaam si tu mkoa wa biashara, bali ni kituo cha neva cha uchumi wa Tanzania, ambapo sera, mifumo ya udhibiti, miundombinu, na huduma za kifedha hukutana na kuamua mwelekeo wa ukuaji wa sekta binafsi ya taifa zima.

## 2.2. Mkoa wa Pwani

Mkoa wa Pwani ni miongoni mwa mikoa yenye nafasi ya kimkakati katika uchumi wa taifa kutokana na jiografia yake, rasilimali zake za asili, na ukaribu wake wa karibu na Mkoa wa Dar es Salaam, kitovu kikuu cha biashara, fedha, na usafirishaji nchini. Makao makuu ya mkoa yapo Kibaha, na mkoa unapakana na Tanga upande wa kaskazini, Morogoro upande wa magharibi, Lindi upande wa kusini, huku ukiuzunguka Mkoa wa Dar es Salaam upande wa mashariki. Mkoa huu pia unapakana na Bahari ya Hindi upande wa kaskazini mashariki na kusini mashariki, jambo linaloupa fursa muhimu za biashara ya baharini, usafirishaji wa kimataifa, uvuvi wa kibiashara, na utalii wa fukwe.

Kijiografia na kimazingira, Mkoa wa Pwani una baadhi ya maeneo muhimu zaidi ya kimkakati, ikiwemo Kisiwa cha Mafia ambacho ni kivutio kikubwa cha utalii wa baharini na ikolojia, Delta ya Rufiji ambayo ni kitovu muhimu cha kilimo, maji, na bioanuai, Hifadhi ya Taifa ya Saadani ambayo ni hifadhi ya kipekee inayounganisha rasilimali za nchi kavu na bahari, pamoja na Mji wa

Bagamoyo wenye umuhimu mkubwa wa kihistoria, kibiashara, na kitamaduni kama mji wa kwanza wa kikoloni wa Afrika Mashariki ya Kijerumani. Maeneo haya yanaipa Pwani nafasi ya kipekee katika kuunganisha uchumi wa uzalishaji, utalii, uhifadhi wa mazingira, na biashara.

Kiuchumi, Mkoa wa Pwani unategemea kwa kiasi kikubwa kilimo, ambacho ndicho chanzo kikuu cha ajira na kipato kwa wakazi wengi wa mkoa. Kilimo kinajumuisha mashamba ya kibiashara na kilimo cha wakulima wadogo, huku mazao muhimu yakijumuisha nazi, korosho, mihogo, na mpunga. Uzalishaji wa nazi na bidhaa zake, hususan mafuta, karanga, na bidhaa za nyuzinyuzi, una mchango mkubwa katika mapato ya kaya na biashara za ndani. Aidha, shughuli za mifugo na uvuvi zinaendelea kuchangia katika uchumi wa mkoa, hasa katika maeneo ya pwani na visiwa, ambapo uvuvi wa bahari, ufugaji wa samaki, na biashara ya mazao ya baharini vina nafasi kubwa ya ukuaji.

Kwa upande wa uwekezaji na viwanda, Mkoa wa Pwani unaendelea kujitokeza kama eneo muhimu la kupokea viwanda vinavyohama au kupanuka kutoka Dar es Salaam kutokana na gharama kubwa za ardhi, msongamano, na vikwazo vya miundombinu katika jiji. Maeneo kama Kibaha, Zegereni, Mkuranga, na Bagamoyo yanazidi kuvutia uwekezaji katika viwanda vya ujenzi, usindikaji wa mazao, maghala, vifaa vya ujenzi, na huduma za usafirishaji. Hali hii inaufanya Mkoa wa Pwani kuwa daraja muhimu kati ya uzalishaji wa ndani, soko la Dar es Salaam, na masoko ya nje kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Ziara ya TNCC katika Mkoa wa Pwani ilionesha kiwango kikubwa cha utayari wa serikali ya mkoa kushirikiana na sekta binafsi katika kukuza uwekezaji na biashara. Mazungumzo kati ya Rais wa TNCC, Ndugu Vicent Bruno Minja, Katibu Tawala wa Mkoa, Bw. Rashid Mchatta, na Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Abubakari Mussa Kunenge yalibainisha dhamira ya pamoja ya kuimarisha Mabaraza ya Biashara ya Mkoa na Wilaya (RBC na DBC), kukuza ubia wa sekta ya umma na binafsi (PPP), pamoja na kuifanya Pwani kuwa miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa kuvutia uwekezaji wa viwanda, utalii, na biashara jumuishi, ikiwemo biashara za wanawake na vijana.

Ziara katika Kiwanda cha Japha Investment and Supply kilichopo Zegereni ilitoa mfano halisi wa mwelekeo wa viwanda unaoendelea kukua mkoani Pwani. Kiwanda hiki, kinachozalisha mabomba ya chuma, mabati, na misumari, kimefaidika na ongezeko la shughuli za ujenzi nchini, lakini pia kilibainisha changamoto muhimu za kimfumo, ikiwemo kukatika kwa umeme bila ratiba maalumu na ucheleweshaji wa malighafi bandarini, hali

inayoongeza gharama za uzalishaji na kupunguza ushindani wa viwanda vya ndani.



Shughuli za Uzalishaji zikiendelea katika kiwanda cha Japha Investment and Supply kilichopo Zegereni mkoani Pwani.

Mkoa wa Pwani una fursa kubwa za kiuchumi kutokana na ukaribu wake na Dar es Salaam na Bandari ya Dar es Salaam, upatikanaji wa ardhi kwa gharama nafuu ikilinganishwa na jiji, uwepo wa rasilimali za bahari, ardhi yenye rutuba, na vivutio vikubwa vya utalii wa asili na urithi. Fursa hizi zinaifanya Pwani kuwa eneo bora kwa uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na uvuvi, vifaa vya ujenzi, utalii wa fukwe, maghala, na huduma za usafirishaji na ugavi. Aidha, uwepo wa maeneo makubwa yasiyotumika kikamilifu unatoa nafasi ya kuanzishwa kwa kanda za viwanda na biashara zinazohudumia soko la ndani na la nje.

Hata hivyo, Mkoa wa Pwani unakabiliwa na changamoto kadhaa zinazoweza kupunguza kasi ya uwekezaji na biashara. Changamoto hizo ni pamoja na miundombinu ya umeme isiyo imara, hususan katika maeneo ya viwanda vinavyoibukia, upatikanaji mdogo wa maji ya viwandani, ucheleweshaji wa mizigo na malighafi bandarini, pamoja na changamoto za upangaji wa matumizi ya ardhi na umilikishaji wa viwanja kwa wawekezaji. Aidha, baadhi ya wafanyabiashara wanakabiliwa na urasimu katika vibali, leseni, na tozo mbalimbali, hali inayoongeza gharama za kufanya biashara.

Kwa ujumla, Mkoa wa Pwani una uwezo mkubwa wa kuwa kitovu muhimu cha pili cha uzalishaji na uwekezaji nchini baada ya Dar es Salaam. Endapo changamoto za miundombinu, uratibu wa taasisi, na mazingira ya biashara zitashughulikiwa ipasavyo, mkoa huu unaweza kuchukua nafasi ya kimkakati katika kuharakisha viwanda, kukuza biashara, na kuongeza mchango wa sekta binafsi katika uchumi wa taifa.

## 2.3. Mkoa wa Lindi

Mkoa wa Lindi upo kusini mwa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye umuhimu wa kimkakati katika uchumi wa taifa kutokana na nafasi yake ya kijiografia, rasilimali asilia, na ukaribu wake na Bahari ya Hindi. Mkoa unapakana na Morogoro (kaskazini), Ruvuma (magharibi), Mtwara (kusini), na Bahari ya Hindi (mashariki). Mpangilio huu unaifanya Lindi kuwa lango muhimu la biashara ya kikanda na kimataifa, hususan kupitia usafiri wa bahari.

Lindi ina pwani ndefu, mabonde yenye rutuba, misitu, na nyanda za kati zinazofaa kwa kilimo, ufugaji, misitu, na shughuli za kiuchumi zinazohusiana na maliasili. Hali hii inaipa mkoa uwezo mkubwa wa uzalishaji wa chakula, mazao ya biashara, na rasilimali ghafi za viwanda. Uchumi wa Mkoa wa Lindi unatokana zaidi na sekta za msingi—kilimo, uvuvi, misitu, na uchimbaji mdogo wa rasilimali asilia. Sekta hizi zinaajiri asilimia kubwa ya wakazi wa mkoa, lakini mchango wake katika pato la taifa bado ni mdogo kutokana na utegemezi wa mauzo ya malighafi ghafi bila kuongeza thamani.

Kilimo ndicho chanzo kikuu cha ajira na kipato katika Mkoa wa Lindi. Mkoa ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa korosho nchini Tanzania, na zao hili ndilo uti wa mgongo wa uchumi wa kaya nyingi. Mbali na korosho, mkoa huzalisha kwa wingi karanga, ufuta, alizeti, mahindi, mpunga, na muhogo.

Kwa mtazamo wa sekta binafsi, Lindi ina faida za msingi za ushindani (comparative advantages) katika kilimo: ardhi yenye rutuba na maeneo makubwa yanayoweza kuendelezwa, hali ya hewa inayofaa kwa mazao ya mafuta na biashara, na nguvu kazi ya kutosha vijijini.

Hata hivyo, kilimo kinaendeshwa zaidi kwa njia za jadi, zenye tija ndogo, na bila miundombinu ya kutosha ya umwagiliaji, maghala, masoko, na usindikaji. Hii husababisha upotevu wa thamani na utegemezi wa masoko ya ghafi.

Kwa msingi huo, Lindi ina fursa kubwa ya uwekezaji katika usindikaji wa korosho, alizeti, ufuta, na karanga, maghala ya kisasa na masoko ya mazao, kilimo cha mkataba na biashara ya pembejeo, na huduma za kifedha za kilimo-biashara.





Ziara bandari Lindi

Ukaribu wa Lindi na Bahari ya Hindi unaipa mkoa fursa ya kipekee katika uchumi wa buluu (blue economy). Uvuvi wa baharini na wa pwani ni chanzo muhimu cha ajira, chakula, na mapato ya ndani. Hata hivyo, tathmini ya TNCC inaonesha kuwa sekta ya uvuvi bado inakabiliwa na utegemezi wa zana za jadi, ukosefu wa miundombinu ya baridi na usindikaji, na upotevu mkubwa wa mazao ya baharini baada ya kuvuliwa. Hali hii inaashiria uwepo wa fursa kubwa za uwekezaji katika bandari ndogo za uvuvi, viwanda vya kuchakata samaki, mifumo ya baridi, na biashara ya mauzo ya nje ya bidhaa za baharini.

Lindi ina bandari ndogo ya bahari ambayo ina uwezo wa kuunganisha biashara kati ya kusini mwa Tanzania na nchi za ukanda wa Bahari ya Hindi, hususan Visiwa vya Comoro na Msumbiji. Bandari hii inaweza kuwa kichocheo kikubwa cha biashara ya mazao ya kilimo, bidhaa za baharini, na malighafi za viwanda. Hata hivyo, miundombinu ya bandari, vifaa, na huduma za kibiashara bado haijafikia kiwango cha kuhimili biashara ya kisasa ya kimataifa.





Ziara ofisi ya mkuu wa mkoa Lindi

Tathmini ya TNCC katika Mkoa wa Lindi imebaini changamoto za msingi zifuatazo kama vile: uwekezaji mdogo katika viwanda na usindikaji, upatikanaji mdogo wa mitaji na huduma za kifedha, ujuzi mdogo wa biashara na ujasiriamali, miundombinu hafifu ya uhifadhi, barabara, na nishati, na ushirikiano mdogo kati ya sekta binafsi na taasisi za umma. Kwa mtazamo wa TNCC, Mkoa wa Lindi una rasilimali, jiografia, na uzalishaji wa kutosha kuugeuza kuwa kitovu muhimu cha kilimo-biashara, uchumi wa bahari, na viwanda vya malighafi katika ukanda wa kusini wa Tanzania. Changamoto iliyopo si ukosefu wa fursa, bali ni upungufu wa miundombinu, uwekezaji wa thamani, na uratibu wa taasisi za maendeleo ya sekta binafsi. Ikiwa rasilimali za kilimo, uvuvi, na madini zitaunganishwa na viwanda, masoko, na mitaji, Lindi inaweza kuwa mojawapo ya nguzo mpya za uchumi wa viwanda na biashara ya nje ya Tanzania.

## 2.4. Mkoa wa Mtwara

Mkoa wa Mtwara upo kusini-mashariki mwa Tanzania na una nafasi ya kimkakati katika uchumi wa taifa kutokana na ukaribu wake na Bahari ya Hindi, mpaka wa kimataifa na Msumbiji, pamoja na uwepo wa miundombinu ya usafiri na nishati. Mkoa unapakana na Lindi (kaskazini), Ruvuma (magharibi), na Msumbiji (kusini), hali inayouwezesha kuwa kitovu muhimu cha biashara ya kikanda na mipakani. Mtwara una mandhari ya pwani, ardhi yenye rutuba, na hali ya hewa ya kitropiki inayofaa kwa uzalishaji wa mazao ya biashara, chakula, na malighafi za viwandani. Makabila kama Wamakonde, Wazaramo, na Wamatumbi yamejenga urithi wa kijamii na kitamaduni unaochangia katika shughuli za uzalishaji na biashara.

Uchumi wa Mkoa wa Mtwara unaongozwa na kilimo, nishati, viwanda, biashara ya mipakani, na huduma za bandari. Mkoa una sifa za uchumi unaochanganya sekta za msingi (kilimo na uvuvi) na sekta za kimkakati (nishati, viwanda, na usafirishaji wa kimataifa). Kutokana na uwepo wa gesi asilia, bandari ya kina kirefu, na viwanda vikubwa kama vile Dangote Cement, Mtwara ina nafasi ya kipekee katika mpito wa Tanzania kuelekea uchumi wa viwanda unaotegemea malighafi za ndani.

Kilimo ni mhimili muhimu wa uchumi wa Mkoa wa Mtwara. Mkoa ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa korosho nchini, zao ambalo ni la kimkakati kwa mapato ya wakulima na mapato ya nje ya nchi. Mbali na korosho, mkoa huzalisha ufuta, alizeti, mahindi, mpunga, na mihogo kwa wingi.




Kushoto; Bandari ndogo ya Mtwara, lango kuu la biashara na uchumi mkoa wa mtwara. Kulia; Kiwanda cha Saruji cha Dangote mkoani Mtwara.

Mtwara ni kitovu kikuu cha gesi asilia nchini Tanzania. Uwepo wa miundombinu ya kuchakata na kusafirisha gesi unaifanya mkoa kuwa mhimili muhimu wa sera ya taifa ya nishati na viwanda. Gesi asilia inatumika kama chanzo cha umeme, nishati ya viwanda, na malighafi kwa uzalishaji wa mbolea, saruji, na kemikali. Hii inaweka msingi mkubwa wa uwekezaji katika viwanda vinavyotumia gesi kama nishati, sekta ya petro-kemia na mbolea, na uzalishaji wa umeme na viwanda vya kati.

Bandari ya Mtwara ni mojawapo ya miundombinu muhimu zaidi ya biashara kusini mwa Tanzania. Inahudumia biashara ya Tanzania na Msumbiji pamoja na nchi za kusini mwa Afrika. Bandari hii ni lango la kusafirisha saruji, korosho, gesi, na bidhaa nyingine za viwandani. Uwepo wa bandari, barabara za kisasa, na uwanja wa ndege unaifanya Mtwara kuwa kitovu cha lojistiki na biashara ya mipakani.

Tathmini ya TNCC imebaini kuwa, pamoja na fursa kubwa zilizopo, mazingira ya biashara katika Mkoa wa Mtwara yanakabiliwa na changamoto kadhaa, zikiwemo: changamoto za kiusalama mpakani na Msumbiji zinazoathiri biashara ya mipakani, upungufu wa rasilimali watu wenye ujuzi wa viwanda na nishati, na miundombinu ya barabara na usafirishaji wa bidhaa za viwandani.

Kwa mtazamo wa TNCC, Mkoa wa Mtwara ni nguzo ya kimkakati ya uchumi wa viwanda, nishati, na biashara ya kimataifa katika ukanda wa kusini wa Tanzania. Mchanganyiko wa gesi asilia, bandari, kilimo cha biashara, na viwanda unaipa Mtwara uwezo wa kuwa kitovu kikuu cha uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa za Tanzania kwenda masoko ya kikanda na kimataifa. Uboreshaji wa mazingira ya biashara, miundombinu, na usalama wa mipaka utaamua kwa kiwango kikubwa kasi ambayo Mtwara itageuka kutoka mkoa

wa rasilimali kwenda kuwa kitovu cha uchumi wa kisasa unaoongozwa na sekta binafsi.

## 2.5. Mkoa wa Morogoro

Mkoa wa Morogoro unapakana na mikoa ya Tanga, Pwani, Lindi, Ruvuma, Iringa, Dodoma, na Manyara, na uko katikati ya mikoa ya pwani ya Bahari ya Hindi na Nyanda za Juu za kusini mwa Tanzania. Jiografia hii inaipa Morogoro nafasi ya kipekee ya kuwa kitovu cha uzalishaji, usafirishaji, na usambazaji wa bidhaa za kilimo na viwanda kwenda masoko ya ndani na ya nje. Mkoa una tambarare pana zenye rutuba kama Bonde la Kilombero (Ifakara) pamoja na maeneo ya milima kama Milima ya Uluguru, ambako Mlima Kimhandu una urefu wa mita 2,646 kutoka usawa wa bahari. Mito mikubwa ya Wami na Ruvu hutiririka kutoka katika milima hii, ambapo Mto Ruvu ni chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam. Mchanganyiko huu wa mabonde, milima, na vyanzo vya maji unaifanya Morogoro kuwa miongoni mwa mikoa yenye uwezo mkubwa wa uzalishaji wa kilimo nchini.

Uchumi wa Mkoa wa Morogoro unaongozwa na kilimo, usindikaji wa mazao, viwanda vidogo na vya kati, pamoja na huduma za biashara na usafirishaji. Mkoa una sifa ya kuwa "ghala la chakula" kutokana na uzalishaji mkubwa wa mahindi, mpunga, mihogo, matunda, mbogamboga, na mazao ya viungo. Hii inafanya Morogoro kuwa mkoa wa mpito kati ya uchumi wa kilimo cha msingi na uchumi wa viwanda vya kuongeza thamani. Uwepo wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, taasisi za utafiti wa kilimo, pamoja na miundombinu ya barabara unaifanya Morogoro kuwa kitovu muhimu cha kilimo-biashara (agribusiness hub).







Ziara Wilmer Rice/Intermech

Mkoa pia una mkakati wa kubadilisha muundo wa uzalishaji wake kutoka kilimo cha jadi kwenda kilimo cha kimkakati cha viungo. Lengo la kimkakati ni kuufanya Morogoro kuwa "Spices Hub" ya Tanzania. Katika mwelekeo huu, mkoa una mpango wa kuzalisha takribani tani 2,000 za karafuu kwa mwaka katika kipindi kifupi kijacho, hatua ambayo itaubadilisha Morogoro kutoka eneo la mazao ya kawaida kwenda kitovu cha mazao ya thamani ya juu kwa masoko ya ndani na ya kimataifa.

Morogoro ina idadi inayoongezeka ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, hali inayoifanya kuwa miongoni mwa mikoa muhimu katika mnyororo wa thamani wa kilimo nchini. Sekta ya uchakataji wa mazao ya kilimo imeajiri idadi kubwa ya wanawake na vijana, na kuchangia katika upatikanaji wa ajira, mapato ya kaya, na kodi kwa serikali. Hata hivyo, tathmini ya TNCC inaonesha kuwa uwezo wa uzalishaji bado unakabiliwa na upungufu wa mitambo ya kisasa, changamoto za upatikanaji wa malighafi bora, na miundombinu ya uhifadhi na barabara katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji.

## 2.6. Mkoa wa Dodoma

Mkoa wa Dodoma ni kitovu cha kiutawala cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndiyo makao makuu ya serikali, bunge, na taasisi kuu za taifa. Kijiografia, Mkoa wa Dodoma unapakana na mikoa ya Manyara, Morogoro, Iringa, na Singida. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Dodoma una wakazi zaidi ya milioni 3, hivyo kuufanya kuwa miongoni mwa mikoa yenye soko kubwa la ndani na nguvu kazi muhimu kwa shughuli za uzalishaji na biashara.

Dodoma ina nafasi ya kipekee katika maendeleo ya sekta binafsi kutokana na uwepo wa serikali kuu, taasisi za fedha, mashirika ya umma, na miundombinu mikubwa ya kitaifa. Ushirikiano kati ya serikali ya Mkoa wa Dodoma na TNCC umejikita katika kuimarisha uwezeshaji wa sekta binafsi kama injini ya maendeleo ya mkoa. Msingi wa ushirikiano huo ni kuhakikisha kuwa sera, mipango ya maendeleo, na miradi ya kimkakati ya mkoa inatekelezwa kwa kuzingatia mahitaji ya wawekezaji, wajasiriamali, na viwanda. Kwa muktadha huo, Mkoa wa Dodoma unatambuliwa kama eneo la kimkakati kwa uwekezaji wa viwanda, huduma za kifedha, usafirishaji, ujenzi, kilimo cha kibiashara, na biashara za kimataifa kutokana na kuwa kituo cha maamuzi ya kisera na matumizi ya serikali.

Katika sekta ya viwanda vya kilimo, Dodoma imejipambanua kama kitovu cha uzalishaji wa mazao ya kimkakati, hususan zabibu, alizeti, mtama, mahindi, na dengu. Mkoa wa Dodoma huzalisha zaidi ya asilimia 60 ya zabibu zote za Tanzania, jambo linaloufanya kuwa msingi wa sekta ya mvinyo na bidhaa zitokanazo na zabibu nchini. Uwepo wa viwanda kama Alko Vintages Ltd, ambacho kina zaidi ya miaka 20 ya uzalishaji wa mvinyo na vinywaji vya zabibu, unaonesha uwezo wa mkoa katika kuunganisha kilimo na viwanda, ajira, mapato ya kodi, na biashara ya kimataifa. Tathmini ya TNCC imebaini kuwa sekta hii ina uwezo mkubwa wa kuongeza mauzo ya nje (exports) iwapo itaungwa mkono kwa sera rafiki, ruzuku za ushindani wa kimataifa, na miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa.



Ziara ofisi ya mkuu wa mkoa wa Dodoma

Katika mijadala ya TNCC na wadau wa viwanda vya Dodoma, changamoto za kimuundo katika mazingira ya biashara zimejitokeza kwa uwazi. Hizi ni pamoja na uelewa mdogo wa masuala ya biashara na kodi kwa baadhi ya watendaji wa mamlaka za mapato, jambo linaloathiri utabiri wa gharama za uwekezaji; ushindani mdogo wa bidhaa za Tanzania katika masoko ya kimataifa kutokana na gharama za uzalishaji na usafirishaji; sera na programu za kilimo ambazo mara nyingi hujikita kwenye mazao machache badala ya kuendeleza mnyororo mzima wa thamani; pamoja na tofauti za kimuundo katika tozo na kodi kati ya wawekezaji wazawa na wageni, hali inayoweza

kudhoofisha ukuaji wa wawekezaji wa ndani. Kwa mtazamo wa TNCC, changamoto hizi zinahitaji maboresho ya sera, uratibu wa taasisi za serikali, na mifumo rafiki ya biashara.

Sekta ya mafuta ya kula ni eneo jingine muhimu katika uchumi wa Mkoa wa Dodoma. Mkoa ni mzalishaji mkubwa wa alizeti, na uwepo wa viwanda kama Three Sisters Oil Mill unaonesha uwezo wa kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao hili kuanzia kwa mkulima hadi kwa mlaji wa mwisho. Kiwanda hiki kimefanikiwa kuhudumia soko la Dodoma na mikoa jirani kwa kusambaza mafuta ya alizeti, hivyo kuchangia usalama wa chakula, ajira, na mapato ya ndani. Hata hivyo, tathmini ya TNCC inaonesha kuwa viwanda vya aina hii vinakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa umeme wa uhakika pamoja na wigo mpana wa tozo na vibali kutoka mamlaka mbalimbali, hali inayoongeza gharama za uzalishaji na kupunguza ushindani wa bidhaa.

Kwa ujumla, Mkoa wa Dodoma unaendelea kujijenga kama kitovu cha utawala, biashara, kilimo cha kibiashara, na viwanda. Kwa mtazamo wa TNCC, fursa za Dodoma zipo katika kuunganisha nguvu ya serikali kuu, soko kubwa la wakazi zaidi ya milioni tatu, uzalishaji wa mazao ya kimkakati kama zabibu na alizeti, pamoja na ukuaji wa mahitaji ya bidhaa na huduma kutokana na ongezeko la watumishi wa umma, taasisi, na balozi. Mkakati wa TNCC ni kuhakikisha kuwa ukuaji huu wa kijiografia na kiutawala unatafsiriwa kuwa ukuaji halisi wa sekta binafsi, viwanda vya ndani, ajira, na mapato ya taifa, hivyo kuifanya Dodoma kuwa mfano wa mji mkuu unaochochea uchumi wa soko huria unaoongozwa na sekta binafsi.

## 2.7. Mkoa wa Singida

Mkoa wa Singida upo katika ukanda wa kati wa Tanzania na una nafasi ya kimkakati katika muunganiko wa biashara kati ya kaskazini, magharibi, na Nyanda za Juu za kusini. Mkoa unapakana na mikoa ya Manyara upande wa kaskazini, Dodoma mashariki, Iringa na Mbeya kusini, Tabora magharibi, na Shinyanga. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Singida una wakazi zaidi ya milioni 2.0, ambao ni rasilimali muhimu ya nguvu kazi kwa sekta ya kilimo, ufugaji, usindikaji wa mazao, na biashara.

Uchumi wa Mkoa wa Singida unategemea kwa kiasi kikubwa ufugaji wa mifugo, ambao ni uti wa mgongo wa kipato kwa kaya nyingi. Mkoa unakadiriwa kuwa na takribani ng’ombe milioni 1.4, sambamba na idadi

kubwa ya mbuzi, kondoo, punda, na kuku, hali inayoifanya Singida kuwa miongoni mwa mikoa muhimu katika uzalishaji wa nyama, maziwa, na bidhaa zitokanazo na mifugo. Hata hivyo, fursa za sekta ya mifugo bado hazijatumika kikamilifu kutokana na changamoto za malisho, huduma za mifugo, upatikanaji wa masoko ya uhakika, na miundombinu ya minyororo ya thamani.

Sekta ya kilimo nayo ni nguzo muhimu ya uchumi wa Mkoa wa Singida, japokuwa inakabiliwa na changamoto ya upungufu na kutotabirika kwa mvua. Mazao makuu yanayolimwa ni pamoja na mtama, alizeti, vitunguu, viazi, mahindi, karanga, na maharage. Mkoa wa Singida ni moja ya wazalishaji wakubwa wa vitunguu nchini Tanzania, huku Wilaya za Ikungi, Iramba, na Mkalama zikitambulika kama maeneo makuu ya uzalishaji wa zao hilo. Zao la alizeti nalo ni muhimu kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya kula, na linatoa fursa kubwa kwa viwanda vya kusindika mazao.





Ziara Singida Fresh Oil/Soko la Vitunguu

Uwepo wa viwanda vya kusindika alizeti kama Singida Fresh Oil Mill unaonesha uwezo wa Mkoa wa Singida kuunganisha kilimo na viwanda (agro-processing). Kiwanda hiki huzalisha mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za alizeti na mazao mengine ya mafuta, na bidhaa zake husambazwa ndani ya Tanzania na pia kuuzwa katika masoko ya kikanda na kimataifa. Sekta hii ina mchango mkubwa katika ajira, mapato ya kodi, na kuongeza thamani ya mazao ya wakulima wa ndani.

Hata hivyo, tathmini ya TNCC imebaini changamoto kubwa zinazolikabili eneo hili, ikiwemo uhaba wa malighafi ya alizeti nchini, hali ambayo imesababisha karibu asilimia 99 ya viwanda vya mafuta mkoani Singida kusitisha uzalishaji kwa takribani miezi sita, pamoja na upungufu wa mbegu bora, ushindani wa mafuta ya kula yanayoagizwa kutoka nje, na kushuka kwa nguvu ya fedha ya Tanzania katika masoko ya kimataifa.

Changamoto za uzalishaji pia zinahusiana kwa karibu na uwezo mdogo wa wakulima kutumia teknolojia na mbinu za kilimo chenye tija, pamoja na uhaba wa tathmini za kitaalamu za ardhi na rutuba yake. Kwa mtazamo wa TNCC, uboreshaji wa mifumo ya ugani, upatikanaji wa pembejeo bora, na uwekezaji katika utafiti wa mbegu za alizeti na mazao mengine ya kimkakati ni nyenzo muhimu za kuongeza uzalishaji na kuhakikisha uendelevu wa viwanda vya kusindika mazao mkoani Singida.

Mkoa wa Singida pia una nafasi muhimu katika biashara ya vitunguu katika soko la kikanda na kimataifa kupitia Soko la Kimataifa la MISUNA. Soko hili ni lango kuu la wakulima wa vitunguu kuingia katika masoko ya Afrika Mashariki, hususan Kenya, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na nchi za Afrika ya Kati. Hata hivyo, tathmini ya TNCC imeonesha kuwa uwezo wa MISUNA bado haujatumiwa kikamilifu kutokana na changamoto za miundombinu, ikiwemo ukosefu wa paa la kisasa, huduma duni za maji, vyoo, chakula, na mazingira yasiyokidhi hadhi ya soko la kimataifa, pamoja na changamoto za kisheria, tozo, na mifumo ya ushuru isiyoendana na uhalisia wa wakulima.

## 2.8. Mkoa wa Tabora

Mkoa wa Tabora upo katika ukanda wa magharibi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa mikubwa kwa ukubwa wa eneo na mchango wake katika uzalishaji wa mazao ya kilimo. Mkoa unapakana na mikoa ya Shinyanga na Simiyu upande wa kaskazini, Singida mashariki, Katavi kusini, na Kigoma magharibi. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Tabora una wakazi zaidi ya milioni 3.3, idadi inayotoa soko kubwa la ndani pamoja na nguvu kazi kwa sekta za uzalishaji.

Mkoa wa Tabora una mchanganyiko wa milima ya chini, mabonde, misitu, na mabwawa, hali inayoupa uwezo mkubwa wa shughuli za kilimo na ufugaji. Mkoa hupata mvua za wastani hadi nyingi wakati wa msimu wa mvua, hali inayouwezesha kulima mazao mbalimbali ya chakula na biashara. Ardhi ya Tabora kwa ujumla inafaa kwa kilimo cha mazao ya msimu na ya kudumu, japokuwa changamoto za miundombinu ya umwagiliaji na teknolojia ya kisasa bado zinazuia matumizi kamili ya rasilimali ardhi.

Sekta ya kilimo ndiyo mhimili mkuu wa uchumi wa Mkoa wa Tabora. Mkoa unajulikana kitaifa kama mmoja wa wazalishaji wakubwa wa pamba, ambayo ni zao la kimkakati na chanzo kikuu cha kipato kwa wakulima wengi wa vijijini. Mbali na pamba, Tabora huzalisha kwa wingi mahindi, mpunga, maharage, karanga, na mboga mboga, mazao yanayohudumia soko la ndani na la nje ya mkoa. Uwepo wa wigo mpana wa mazao unatoa fursa kubwa ya kuanzisha na kupanua viwanda vya kusindika mazao (agro-processing) ili kuongeza thamani, kupunguza upotevu wa mazao, na kuongeza mapato ya wakulima.

Mbali na kilimo, Mkoa wa Tabora una rasilimali za madini, zikiwemo dhahabu na shaba, ambazo zina mchango unaokua katika uchumi wa mkoa. Shughuli za uchimbaji wa madini, hususan kwa wachimbaji wadogo na wa kati, zimeongeza ajira na mzunguko wa fedha katika baadhi ya maeneo ya mkoa. Hata hivyo, tathmini ya TNCC inaonesha kuwa sekta ya madini bado inahitaji uwekezaji zaidi katika teknolojia, usalama wa migodi, uongezaji thamani wa madini, na urasimishaji wa shughuli za wachimbaji wadogo ili kuongeza mchango wake katika mapato ya mkoa na taifa. Mkoa huu pia una rasilimali za kihistoria na vivutio vya utalii wa kiutamaduni, hususan maeneo yanayohusishwa na historia ya biashara ya kale na harakati za ukombozi. Ingawa vivutio hivi bado havijatumika kikamilifu kibiashara, vina fursa kubwa ya kuendelezwa kupitia uwekezaji katika miundombinu ya utalii, huduma za malazi, na masoko ya utalii wa ndani na wa kimataifa.

Katika jitihada za TNCC kutathmini mazingira ya biashara na uwekezaji mkoani Tabora, ziara ilifanyika kuanzia katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, na baadaye kutembelea maeneo mbalimbali ya uzalishaji na biashara. Miongoni mwa maeneo yaliyotembelewa ni Kiwanda cha Kuchakata Asali cha TWC – Tabora, ambacho kinaendeshwa kwa ushirikiano wa vikundi vya wanawake na kujikita katika mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki, ukusanyaji wa asali, na usindikaji wa mazao yatokanayo na asali. Kiwanda hiki ni mfano wa biashara jumuishi (inclusive business) inayochangia ajira, kipato cha kaya, na uwezeshaji wa wanawake katika sekta ya uzalishaji.

Tathmini ya TNCC katika kiwanda cha TWC – Tabora imebaini changamoto kadhaa zinazokwamisha ukuaji wa biashara ndogo na za kati (MSMEs), ikiwemo ugumu wa kupata leseni na alama ya ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), uhaba wa mitaji ya kuendesha na kupanua biashara, pamoja na changamoto za upatikanaji wa malighafi bora, hususan karanga na mazao mengine yanayotumika katika usindikaji. Aidha,

changamoto za uhaba wa wanachama katika vikundi vya uzalishaji na malimbikizo ya kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zimebainishwa kama vikwazo vinavyopunguza uendelevu wa biashara na uwezo wa wafanyabiashara kukua.

## 2.9. Mkoa wa Shinyanga

Mkoa wa Shinyanga upo katika ukanda wa ziwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na una nafasi ya kimkakati katika mtiririko wa biashara na uzalishaji kati ya kanda ya ziwa, ukanda wa magharibi, na kanda ya kati. Mkoa unapakana na mikoa ya Mwanza, Geita, na Kagera upande wa kaskazini, Tabora upande wa kusini, Kigoma upande wa magharibi, na Simiyu upande wa mashariki. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Shinyanga una idadi ya watu inayokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 2.2, hali inayoupa mkoa huu nguvu kazi kubwa na soko la ndani kwa bidhaa na huduma mbalimbali.

Mkoa huu una ardhi tambarare inayofaa kwa shughuli za kilimo, ufugaji, na uchimbaji wa madini. Hali ya hewa ni ya ukame wa wastani hadi nusu-ukame, jambo linaloathiri uzalishaji wa kilimo cha kutegemea mvua, lakini pia kutoa fursa ya kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji na teknolojia za kisasa za kilimo. Ardhi ya mkoa inafaa kwa uzalishaji wa mazao kama pamba, mpunga, mahindi, alizeti, na mazao ya mifugo, sambamba na shughuli za ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, na kondoo ambazo ni sehemu ya maisha ya kiuchumi ya wakazi wengi wa mkoa.

Uchumi wa Mkoa wa Shinyanga unajikita kwa kiasi kikubwa katika sekta ya madini, hususan uchimbaji mdogo na wa kati wa dhahabu na almasi. Wilaya za Kahama, Msalala, na Ushetu ni miongoni mwa maeneo yenye shughuli nyingi za uchimbaji wa dhahabu, zikiwemo shughuli za wachimbaji wadogo (ASM – Artisanal and Small-scale Mining). Sekta hii imekuwa chanzo muhimu cha ajira, kipato cha kaya, na mzunguko wa fedha katika miji na vijiji vinavyozunguka maeneo ya migodi. Kwa mtazamo wa TNCC, sekta ya madini mkoani Shinyanga ina fursa kubwa ya kuimarishwa zaidi kupitia urasimishaji wa wachimbaji wadogo, uwekezaji katika teknolojia salama za uchimbaji, uongezaji thamani wa madini, na uimarishaji wa minyororo ya biashara inayohusisha wasambazaji wa pembejeo, huduma za kifedha, na masoko.





Kikao na wadau Shinyanga

Katika jitihada za TNCC kutathmini mazingira ya biashara na uwekezaji mkoani Shinyanga, ziara ya kitaasisi ilifanyika kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi. Ziara hiyo ilihusisha mazungumzo na uongozi wa mkoa, Ofisi za TNCC – Shinyanga, pamoja na mikutano na wakulima, wafanyabiashara, wachimbaji wa madini, na wawakilishi wa taasisi za umma. Aidha, mdahalo wa wadau wa sekta binafsi na sekta ya umma ulifanyika, ukiwakutanisha wafanyabiashara, wenye viwanda, wakulima, na watendaji wa serikali kwa lengo la kubaini changamoto, fursa, na mapendekezo ya kuboresha mazingira ya biashara mkoani humo. Mdahalo huo uliibua masuala muhimu yanayohusu kodi, leseni, upatikanaji wa mitaji, miundombinu, na uratibu wa taasisi za udhibiti katika kusaidia ukuaji wa sekta binafsi.

Miongoni mwa vielelezo muhimu vya maendeleo ya viwanda mkoani Shinyanga ni Kiwanda cha Jambo, ambacho ni moja ya viwanda vinavyojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa za chakula na vinywaji. Kiwanda hiki huzalisha bidhaa mbalimbali ikiwemo juisi, maji ya kunywa, biskuti, pipi, na bidhaa za vifungashio, ambazo husambazwa katika masoko ya ndani na, kwa kiwango fulani, masoko ya nje ya nchi. Uwepo wa kiwanda hiki una mchango mkubwa katika ajira kwa wakazi wa Shinyanga, kuongeza mapato ya serikali kupitia kodi na tozo, na kuimarisha mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa chakula na vinywaji katika ukanda wa ziwa.

Kwa ujumla, Mkoa wa Shinyanga una nafasi muhimu katika uchumi wa Tanzania kutokana na utajiri wake wa rasilimali za madini, nguvu kazi kubwa, uwepo wa viwanda vya uzalishaji, na nafasi yake ya kijiografia katika ukanda wa ziwa. Tathmini ya TNCC inaonesha kuwa kwa kuimarisha uratibu kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, kuboresha miundombinu, kuwezesha wachimbaji wadogo na MSMEs, pamoja na kuwekeza katika viwanda vya

kuongeza thamani, Mkoa wa Shinyanga unaweza kuwa kitovu muhimu cha uzalishaji, biashara, na ajira endelevu nchini Tanzania.

## 2.10. Mkoa wa Kagera

Mkoa wa Kagera upo kaskazini-magharibi mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye umuhimu mkubwa wa kimkakati katika uchumi wa taifa kutokana na rasilimali zake za asili, nafasi yake ya kijiografia, na mchango wake katika biashara ya mipakani. Mkoa unapakana na nchi tatu za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambazo ni Uganda upande wa kaskazini, Rwanda upande wa magharibi, na Burundi upande wa kusini, huku upande wa mashariki ukipakana na Mkoa wa Geita. Mpaka huu wa kimataifa unaifanya Kagera kuwa lango muhimu la biashara, usafirishaji, na mahusiano ya kiuchumi kati ya Tanzania na nchi jirani.

Mkoa wa Kagera una sifa ya uwepo wa Ziwa Viktoria upande wa kaskazini, ambalo ni ziwa kubwa zaidi barani Afrika, pamoja na maeneo ya milima, mabonde, na ardhi yenye rutuba kubwa kwa kilimo. Mazingira haya yanawezesha uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara kwa kiwango kikubwa. Zaidi ya asilimia 70 ya wakazi wa Kagera hutegemea kilimo kama shughuli kuu ya kiuchumi, jambo linaloufanya mkoa kuwa mhimili muhimu wa usalama wa chakula na malighafi za viwanda. Mazao ya chakula yanayolimwa kwa wingi ni pamoja na mahindi, mpunga, muhogo, maharage, na viazi vitamu, huku mazao ya biashara yakijumuisha kahawa, chai, na kwa kiwango kidogo korosho. Kahawa ya Kagera, hususan aina ya Robusta, ni miongoni mwa mazao ya kimkakati yanayochangia mapato ya wakulima na fedha za kigeni kupitia mauzo ya nje. Mkoa pia una mashamba makubwa ya chai, yakiwemo yale yanayoendeshwa na Kagera Tea Company Limited, ambayo hutoa ajira kwa wakazi wa eneo hilo na kuchangia maendeleo ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo.



Ziara ofisi ya mkuu wa mkoa Kagera

Ziwa Viktoria linatoa fursa kubwa katika sekta ya uvuvi na biashara ya mazao ya samaki. Dagaa na sangara ni miongoni mwa bidhaa kuu zinazovuliwa na kusindika kwa matumizi ya ndani na masoko ya nje. Viwanda vya kuchakata mazao ya samaki, kama vile Supreme Perch, vina mchango mkubwa katika kuongeza thamani ya mazao, kukuza mauzo ya nje, na kuongeza ajira kwa wananchi. Sekta hii ina nafasi kubwa zaidi ya kukua endapo uwekezaji utaelekezwa katika teknolojia za kisasa za uchakataji, uhifadhi, na usafirishaji wa mazao ya uvuvi.

Miundombinu ya usafiri na biashara katika Mkoa wa Kagera inaendelea kuboreshwa ili kuendana na mahitaji ya uchumi wa kikanda. Mkoa una mtandao wa barabara unaounganisha wilaya zake na mikoa jirani, pamoja na bandari za Ziwa Viktoria kama Bandari ya Kemondo na Bandari ya Bukoba, ambazo ni muhimu kwa usafirishaji wa bidhaa na abiria. Aidha, uboreshaji wa uwanja wa ndege wa Bukoba unaimarisha zaidi usafiri wa anga na kurahisisha shughuli za kibiashara, uwekezaji, na utalii.



Kikao na kamati tendaji Kagera

Katika muktadha wa maendeleo ya biashara na uwekezaji, Mkoa wa Kagera umeendelea kuchukua hatua za kimkakati kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi. Hatua hizi ni pamoja na utengenezaji na utekelezaji wa Ramani ya Uwekezaji ya Mkoa (Investment Map) kwa kushirikiana na UNDP, kuimarisha mabaraza ya biashara katika ngazi za wilaya na mkoa, pamoja na kufufua na kuimarisha vikundi vya kiuchumi (clusters) katika sekta za biashara, kilimo, uvuvi, na mifugo. Mipango mingine ya kimkakati ni pamoja na maandalizi ya Investment Forum, kuanzisha masoko makubwa ya mazao ya uvuvi hususan dagaa wakavu, na kuendeleza kampeni ya "Ijuka Omuka" inayolenga kuwahamasisha wana Kagera kurejea nyumbani kuwekeza.

## 2.11. Mkoa wa Geita

Mkoa wa Geita upo kaskazini-magharibi mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye umuhimu mkubwa wa kimkakati katika maendeleo ya uchumi wa taifa. Mkoa huu una rasilimali nyingi za kiuchumi, historia tajiri, na fursa pana za uwekezaji katika sekta za madini, kilimo, biashara, huduma, na utalii. Geita ni mkoa muhimu katika kukuza biashara endelevu, kuimarisha uwekezaji wa ndani na nje, pamoja na kuunganisha sekta binafsi na sekta ya umma kwa maendeleo ya pamoja. Mkoa una mandhari ya milima, mabonde, na maeneo ya maji, ukiwemo ukanda wa Ziwa Viktoria; mandhari haya yanaupa Mkoa wa Geita fursa kubwa katika sekta ya uvuvi, usafiri wa majini, na biashara ya kikanda.





Ziara GGM

Sekta ya madini ndiyo mhimili mkuu wa uchumi wa Mkoa wa Geita na miongoni mwa sekta zinazoongoza kwa mchango mkubwa katika pato la

taifa. Mkoa unajivunia uwepo wa Mgodi wa Dhahabu wa Geita (Geita Gold Mine – GGM), ambao ni mmoja wa migodi mikubwa na wazalishaji wakuu wa dhahabu nchini Tanzania. Sekta hii hutoa ajira kwa maelfu ya wananchi moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja, na pia huchochea ukuaji wa biashara za huduma, usafirishaji, ugavi wa vifaa, na chakula. Kwa mujibu wa takwimu za sekta ya madini, Mkoa wa Geita unachangia sehemu kubwa ya uzalishaji wa dhahabu nchini, jambo linaloufanya kuwa kivutio kikubwa cha uwekezaji katika uchimbaji wa madini.

Kilimo ni sekta ya pili kwa umuhimu katika uchumi wa Mkoa wa Geita, ambapo zaidi ya asilimia 60 ya wakazi wa mkoa hutegemea kilimo kama chanzo kikuu cha kipato. Mazao ya chakula yanayolimwa kwa wingi ni pamoja na mahindi, mpunga, muhogo, na viazi vitamu, wakati mazao ya biashara yanajumuisha alizeti, pamba, na kwa baadhi ya maeneo korosho. Mazao haya yanatoa fursa kubwa za uwekezaji katika kilimo cha kibiashara, viwanda vya kuchakata mazao (agro-processing), pamoja na biashara ya ndani na ya nje. Sekta ya kilimo pia ina mchango mkubwa katika upatikanaji wa malighafi kwa viwanda na kuimarisha usalama wa chakula.




Ziara ofisi ya mkuu wa mkoa Geita/Blue coast

Sekta ya mifugo na bidhaa za nyama inaendelea kukua katika Mkoa wa Geita, ikichochewa na uwepo wa machinjio ya kisasa kama Machinjio ya Kisasa ya Mpomvu. Machinjio haya yanatumia teknolojia za kisasa katika kuchinja ng'ombe, kondoo, na mbuzi, na yana mchango mkubwa katika kuongeza thamani ya mazao ya mifugo, kuboresha ubora wa nyama, na kufungua masoko ya ndani na ya nje. Uwekezaji katika minyororo ya thamani ya mifugo na nyama ni fursa muhimu ya kukuza viwanda, ajira, na mapato ya wakulima na wafugaji.

Sekta ya huduma na usafirishaji pia ina nafasi muhimu katika uchumi wa Mkoa wa Geita. Kampuni kama Blue Coast Logistics and Transport, ambayo

inamilikiwa na wazawa kwa asilimia 100, ni mfano wa mchango wa sekta binafsi katika kutoa huduma za usafirishaji wa watu na bidhaa ndani na nje ya nchi. Ushiriki wa kampuni kama hizi katika mnyororo wa thamani wa sekta ya madini, ikiwemo usafirishaji wa malighafi kwa migodi mikubwa kama GGM, unaonesha fursa kubwa ya kuimarisha ushiriki wa wazawa katika uchumi wa mkoa na taifa.

## 2.12. Mkoa wa Mwanza

Mkoa wa Mwanza upo kaskazini-magharibi mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye umuhimu mkubwa wa kimkakati katika maendeleo ya uchumi wa taifa. Mwanza ni kitovu muhimu cha biashara, usafirishaji, na huduma katika ukanda wa Ziwa Viktoria. Mkoa una rasilimali nyingi za asili, nafasi ya kipekee ya kijiografia, na miundombinu inayoendelea kukua, hali inayoupa uwezo mkubwa wa kuchochea biashara ya ndani, kikanda, na kimataifa. Mkoa huu unapakana na Mkoa wa Kagera upande wa magharibi, Mkoa wa Shinyanga upande wa kusini, Mkoa wa Geita upande wa mashariki, na Jamhuri ya Uganda upande wa kaskazini. Ziwa Viktoria, ambalo ni ziwa kubwa zaidi barani Afrika na la pili kwa ukubwa duniani, linapita katika eneo kubwa la mkoa huu. Uwepo wa ziwa hili unaipa Mwanza nafasi ya kipekee katika biashara ya majini, usafirishaji wa bidhaa, uvuvi, utalii, na uhusiano wa kiuchumi na nchi jirani zinazozunguka ziwa.



Ziara ofisi za TNCC Mwanza

Sekta ya kilimo ni mhimili muhimu wa uchumi wa Mkoa wa Mwanza, ambapo sehemu kubwa ya wakazi wanategemea kilimo kama chanzo kikuu cha kipato. Mazao ya chakula yanayozalishwa kwa wingi ni pamoja na mahindi, mpunga, muhogo, na viazi vitamu, wakati mazao ya biashara yanajumuisha

pamba, alizeti, na kwa baadhi ya maeneo kahawa. Mkoa wa Mwanza ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa pamba nchini, zao ambalo ni malighafi muhimu kwa viwanda vya nguo na mafuta ya pamba. Kilimo cha kibiashara na uongezaji thamani wa mazao (agro-processing) vina nafasi kubwa ya kuongeza ajira, mapato, na ushindani wa biashara.

Sekta ya uvuvi ni mojawapo ya sekta kuu za uchumi wa Mkoa wa Mwanza kutokana na rasilimali za Ziwa Viktoria. Samaki aina ya dagaa, sato (tilapia), na sangara ni bidhaa muhimu katika biashara ya ndani na nje ya nchi. Maelfu ya wananchi wanapata ajira katika shughuli za uvuvi, usindikaji, usafirishaji, na biashara ya samaki. Uwepo wa viwanda vya kusindika samaki na bidhaa za uvuvi katika Mwanza unaifanya mkoa kuwa kitovu cha biashara ya mazao ya uvuvi katika ukanda wa Ziwa Viktoria.

Rasilimali za madini pia zinapatikana katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mwanza, ikiwemo dhahabu, shaba, na chokaa. Madini haya yanaipa Mwanza fursa ya kuendeleza shughuli za uchimbaji mdogo na wa kati, pamoja na biashara zinazohusiana na huduma za migodi. Sekta ya madini, inapounganishwa na huduma za usafirishaji, fedha, na ugavi, inaweza kuwa kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi wa mkoa.



Ziara ofisi ya mkuu wa mkoa Mwanza

Sekta ya utalii katika Mkoa wa Mwanza inaendelea kukua, ikichochewa na mandhari ya Ziwa Viktoria, miamba ya kuvutia ya Jiji la Mwanza, na vivutio vya asili na kihistoria. Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo ni moja ya vivutio vikubwa vya utalii, ikitoa fursa za uwekezaji katika hoteli, huduma za usafiri wa majini, utalii wa mazingira, na burudani. Utalii wa mikutano, mapumziko, na luxury cruising kupitia Ziwa Viktoria ni eneo lenye fursa kubwa zaidi kwa wawekezaji.

Miundombinu ya usafiri ni nguzo muhimu ya maendeleo ya biashara katika Mkoa wa Mwanza. Mkoa una mtandao wa barabara kuu zinazouunganisha na mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kati. Aidha, Uwanja wa Ndege wa Mwanza ni miongoni mwa viwanja vya ndege vinavyohudumia idadi kubwa ya abiria na mizigo nchini, hivyo kuimarisha biashara, utalii, na huduma. Usafiri wa majini kupitia Ziwa Viktoria unaipa Mwanza nafasi ya kuwa lango la biashara kati ya Tanzania na nchi jirani.

Katika kuimarisha miundombinu ya kimkakati, miradi mikubwa inaendelea kutekelezwa. Ujenzi wa Meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tuu, unaotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), unatarajiwa kuongeza uwezo wa usafirishaji wa abiria wapatao 1,200, magari madogo 20, magari makubwa 5, na mizigo ya tani 400. Mradi huu utachochea biashara ya kikanda, kuongeza mapato ya bandari, na kukuza utalii wa kifahari (luxury cruising) katika Ziwa Viktoria. Aidha, Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) – Kituo cha Mwanza, unaogharimu takribani shilingi trilioni 2.3, unatarajiwa kuunganisha Mwanza na mtandao wa reli ya kisasa, hivyo kupunguza gharama za usafirishaji na kuongeza ushindani wa bidhaa za mkoa katika masoko ya ndani na nje.




Ziara bandari Mwanza

Maendeleo ya miundombinu ya biashara yanaonekana pia kupitia ujenzi wa Soko Jipya la Mjini Kati (Central City Market), ambalo lilianza kujengwa mwaka 2020 na kukamilika mwishoni mwa mwaka 2024. Soko hili linatarajiwa kuwa kitovu cha biashara ya rejareja na jumla, kuboresha mazingira ya biashara, na kuongeza mapato ya wafanyabiashara na Halmashauri.

Mkoa wa Mwanza una fursa nyingi za kiuchumi zinazojitokeza katika sekta mbalimbali. Fursa hizo ni pamoja na kilimo cha kibiashara na viwanda vya kuchakata mazao, uvuvi na usindikaji wa mazao ya uvuvi, utalii wa mazingira na wa majini, pamoja na biashara ya usafirishaji kupitia Ziwa Viktoria,

bandari, na reli ya kisasa. Uwekezaji katika masoko ya kisasa, maghala, viwanda vidogo na vya kati, pamoja na huduma za kifedha na kidigitali, una nafasi kubwa ya kuchochea ukuaji wa biashara. Kwa mtazamo wa TNCC, Mwanza pia ni lango muhimu la biashara ya kikanda kati ya Tanzania na nchi za Afrika Mashariki zinazozunguka Ziwa Viktoria.

Pamoja na fursa zilizopo, Mkoa wa Mwanza unakabiliwa na changamoto kadhaa za kibiashara na kiuchumi. Changamoto hizo ni pamoja na gharama za juu za uzalishaji na usafirishaji kwa baadhi ya bidhaa, changamoto za miundombinu ya masoko na maghala kwa wafanyabiashara wadogo, mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri kilimo na uvuvi, pamoja na changamoto za upatikanaji wa mitaji nafuu kwa MSMEs. Aidha, uratibu wa sera, tozo, na kanuni za biashara katika ngazi za mikoa na mamlaka mbalimbali bado unahitaji kuimarishwa ili kuondoa vikwazo visivyo vya lazima kwa wafanyabiashara.

## 2.13. Mkoa wa Simiyu

Mkoa wa Simiyu ulianzishwa rasmi mwaka 2012 baada ya kugawanywa kutoka Mkoa wa Shinyanga, na ni miongoni mwa mikoa mipya inayokua kwa kasi kiuchumi katika Kanda ya Ziwa nchini Tanzania. Simiyu ni mkoa wenye umuhimu mkubwa wa kimkakati kutokana na rasilimali zake za kilimo, mifugo, uvuvi, na nafasi yake ya kijiografia karibu na Ziwa Viktoria. Mkoa wa Simiyu unapakana na Mkoa wa Mara upande wa kaskazini, Mkoa wa Shinyanga upande wa kusini, Mkoa wa Arusha upande wa mashariki, na Ziwa Viktoria upande wa magharibi. Mandhari ya mkoa huu yanajumuisha savana pana zinazofaa kwa kilimo na ufugaji, pamoja na maeneo ya karibu na Ziwa Viktoria yanayotoa fursa za uvuvi na biashara zinazohusiana na rasilimali za maji. Wakazi wengi wa mkoa ni jamii ya Wasukuma, ambao kwa muda mrefu wamejenga uchumi wao katika kilimo, ufugaji, na biashara ndogo ndogo.

Sekta ya kilimo ni mhimili mkuu wa uchumi wa Mkoa wa Simiyu. Mazao ya chakula kama mahindi, mtama, na maharagwe huzalishwa kwa wingi kwa ajili ya matumizi ya ndani na biashara kati ya mikoa. Aidha, zao la pamba ni miongoni mwa mazao ya biashara yanayochangia kwa kiasi kikubwa pato la wakulima na mzunguko wa biashara mkoani humo. Kilimo hiki kinatoa fursa kubwa kwa uwekezaji katika viwanda vya kuchakata pamba. Uboreshaji wa kilimo cha kibiashara na kuunganisha wakulima na masoko ni eneo lenye mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Simiyu.



Ziara ofisi ya mkuu wa wilaya Bariadi

Ufugaji ni shughuli nyingine muhimu ya kiuchumi katika Mkoa wa Simiyu. Mkoa unajivunia idadi kubwa ya ng'ombe, mbuzi, na kondoo, ambao hutoa bidhaa kama nyama, maziwa, na ngozi kwa masoko ya ndani na nje ya mkoa. Sekta ya mifugo ina mchango mkubwa katika ajira na kipato cha kaya, na ina nafasi kubwa ya kuendelezwa zaidi kupitia uwekezaji katika machinjio ya kisasa, viwanda vya kusindika nyama na maziwa, pamoja na minyororo ya thamani ya ngozi na bidhaa zake.

Uwepo wa Ziwa Viktoria upande wa magharibi mwa mkoa unaipa Simiyu fursa kubwa katika sekta ya uvuvi na biashara ya mazao ya samaki. Uvuvi wa samaki na dagaa ni chanzo muhimu cha ajira na mapato kwa wakazi wa maeneo ya karibu na ziwa. Kwa mtazamo wa TNCC, fursa za uwekezaji zipo katika uboreshaji wa mbinu za uvuvi, uhifadhi, na usindikaji wa mazao ya samaki, pamoja na kuimarisha miundombinu ya masoko ya bidhaa za uvuvi.

Sekta ya viwanda katika Mkoa wa Simiyu bado iko katika hatua za ukuaji, lakini ina matarajio makubwa. Viwanda vidogo na vya kati vya kuchakata mazao ya kilimo kama pamba na alizeti vinaendelea kuibuka, vikichangia ajira na kuongeza thamani ya mazao ya wakulima. Aidha, ukaribu wa Simiyu na vivutio vikubwa vya utalii kama Hifadhi ya Taifa ya Serengeti unaipa mkoa fursa katika utalii wa kiutamaduni na mazingira, hususan katika huduma za malazi, usafiri, na bidhaa za utalii wa jamii.

Mkoa wa Simiyu una fursa nyingi za kiuchumi, hususan katika sekta za kilimo cha kibiashara (pamba, mahindi, na mazao ya chakula), ufugaji wa mifugo, uvuvi katika Ziwa Viktoria, na viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo. Fursa nyingine ni pamoja na uwekezaji katika minyororo ya thamani ya mazao, masoko ya kisasa, maghala, na huduma za kifedha kwa wakulima na wafugaji. Aidha, utalii wa kiutamaduni na wa mazingira una

nafasi ya kuchangia zaidi pato la mkoa endapo utaendelezwa kwa mipango madhubuti.

Pamoja na fursa zilizopo, Mkoa wa Simiyu unakabiliwa na changamoto kadhaa za kibiashara. Changamoto hizo ni pamoja na miundombinu ya usafiri na masoko ambayo bado inahitaji kuboreshwa, upatikanaji mdogo wa mitaji nafuu kwa wajasiriamali na MSMEs, mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri uzalishaji wa kilimo na mifugo, pamoja na changamoto za kiutendaji katika ofisi za biashara za wilaya. Aidha, uratibu wa sera, tozo, na kanuni za biashara katika ngazi za serikali za mitaa bado unahitaji kuimarishwa ili kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara.

## 2.14. Mkoa wa Mara

Mkoa wa Mara upo katika Kanda ya Ziwa kaskazini mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukiwa na umuhimu mkubwa wa kimkakati kiuchumi, kibiashara, na kijiografia. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Mara una zaidi ya watu milioni 1.7, idadi inayotoa soko kubwa la ndani pamoja na nguvu kazi muhimu kwa shughuli za uzalishaji. Mkoa wa Mara ni moja ya maeneo yenye mchanganyiko wa rasilimali za asili, urithi wa kiutamaduni, na fursa pana za uwekezaji. Mkoa wa Mara unapakana na Mkoa wa Mwanza na Simiyu upande wa kusini, Mkoa wa Arusha upande wa mashariki, Ziwa Victoria upande wa magharibi, na Jamhuri ya Kenya upande wa kaskazini. Mpangilio huu unaifanya Mara kuwa lango muhimu la biashara ya kikanda (cross-border trade), hususan katika miji ya Tarime, Sirari, na Musoma. Mandhari ya mkoa yanajumuisha savana pana za Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, maeneo ya vilima, pamoja na ukanda wa Ziwa Victoria, hali inayochochea shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi, na utalii.



Ziara ofisi ya mkuu wa mkoa Mara

Kiuchumi, kilimo ndicho mhimili mkuu wa uchumi wa Mkoa wa Mara. Mazao ya chakula kama mahindi, mihogo, mtama, na mpunga huzalishwa kwa wingi, huku mazao ya biashara kama pamba yakichangia kipato cha wakulima na mapato ya mkoa. Kwa mujibu wa takwimu za Serikali za Mitaa, zaidi ya asilimia 65 ya wakazi wa mkoa wanategemea kilimo na ufugaji kama chanzo kikuu cha maisha. Sekta ya ufugaji wa mifugo—hasa ng'ombe, mbuzi, na kondoo—ina mchango mkubwa katika uzalishaji wa nyama, maziwa, na ngozi, hali inayotoa fursa za kuanzisha na kukuza viwanda vya kuchakata bidhaa za mifugo. Kwa mfano, uwepo wa viwanda vidogo na vya kati vya ngozi na bidhaa zake, kama Credo Leather (Musoma), unaonesha uwezo mkubwa wa sekta hii endapo utawezeshwa zaidi.

Sekta ya utalii ni nguzo nyingine muhimu ya uchumi wa Mkoa wa Mara. Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, maarufu duniani kwa tukio la uhamiaji wa nyumbu (Great Wildebeest Migration), huvutia mamia ya maelfu ya watalii kila mwaka na kuchangia kwa kiasi kikubwa mapato ya taifa kupitia utalii wa picha, malazi, usafiri, na huduma nyingine. Aidha, Ziwa Victoria linatoa fursa za utalii wa maji, uvuvi wa kibiashara, na biashara zinazohusiana na usindikaji wa mazao ya samaki.



Picha: ziara kiwanda cha alizeti/kikao kamati tendaji Mara

Mkoa wa Mara pia unaonesha dalili chanya katika ukuaji wa sekta ya viwanda, hususan viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo. Uwekezaji katika viwanda vya kuchakata alizeti kwa ajili ya mafuta ya kula, kama vile Kiwanda cha Kuchakata Mafuta ya Alizeti – Nyahita, ni mfano wa namna rasilimali za ndani zinavyoweza kuongezewa thamani na kuchochea ajira, mapato ya wakulima, na ukuaji wa uchumi wa mkoa. Ukuaji wa miundombinu ya barabara, nishati ya umeme (ikiwemo miradi ya REA), pamoja na usafiri wa maji kupitia Ziwa Victoria, unaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Kwa upande wa mazingira ya biashara, Serikali ya Mkoa wa Mara imeendelea kuchukua hatua za kuboresha hali ya uwekezaji kwa kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi, kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa uwekezaji, na kuhimiza majukwaa ya majadiliano kama Mabaraza ya Biashara ya Mkoa na Wilaya. Katika muktadha huu, TNCC inaona umuhimu wa kuimarisha zaidi uratibu kati ya ofisi za Serikali na Chemba ya Biashara ili kuhakikisha kero za wafanyabiashara na wawekezaji zinashughulikiwa kwa ufanisi na kwa wakati.

Mkoa wa Mara una fursa nyingi za kimkakati kwa maendeleo ya biashara na uwekezaji. Fursa hizo ni pamoja na kilimo cha kibiashara na uwekezaji katika umwagiliaji, uzalishaji wa mbegu bora na kilimo cha mkataba; uanzishaji na upanuzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo (mahindi, pamba, alizeti) na bidhaa za mifugo (nyama, maziwa, ngozi); biashara ya mipakani na kikanda kupitia mpaka wa Tanzania na Kenya (Sirari–Isebania); utalii wa kimataifa na wa ndani kupitia Serengeti, pamoja na utalii wa ziwa na utamaduni; na uvuvi wa kibiashara na usindikaji wa mazao ya samaki kutoka Ziwa Victoria.

Pamoja na fursa zilizopo, Mkoa wa Mara unakabiliwa na changamoto kadhaa zinazohitaji juhudi za pamoja kati ya Serikali na sekta binafsi, zikiwemo upungufu wa viwanda vikubwa vya kuchakata mazao, hali inayosababisha malighafi kuuzwa ghafi bila kuongeza thamani, miundombinu ya barabara na masoko katika baadhi ya maeneo ya vijijini ambayo bado haijaimarika kikamilifu, changamoto za upatikanaji wa mitaji na huduma za kifedha kwa MSMEs, migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji, na hifadhi za wanyamapori, na uhitaji wa kuimarisha ujuzi wa biashara, teknolojia, na ubunifu kwa wajasiriamali wa ndani.

## 2.15. Mkoa wa Kigoma

Mkoa wa Kigoma upo magharibi mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye umuhimu mkubwa wa kimkakati kwa biashara na uwekezaji kutokana na jiografia yake ya kipekee na rasilimali asilia. Mkoa huu unapakana na Ziwa Tanganyika, ziwa refu zaidi duniani, ambalo ni mhimili muhimu wa uchumi wa mkoa kupitia uvuvi, usafiri wa majini, na biashara ya mipakani. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Kigoma una idadi ya watu inayokadiriwa kufikia zaidi ya milioni 2.4, hali inayoupa mkoa soko kubwa la ndani na nguvu kazi

muhimu. Kigoma ni lango la biashara ya kikanda linalounganisha Tanzania na nchi za Maziwa Makuu. Kigoma inapakana na Mkoa wa Katavi upande wa kusini, Tabora upande wa mashariki, na Kagera upande wa kaskazini-mashariki, huku ikishirikiana mipaka ya kimataifa na Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), na Zambia kupitia Ziwa Tanganyika. Mandhari ya mkoa yanajumuisha milima, mabonde, misitu ya asili, na fukwe za ziwa, hali inayoupa mkoa rasilimali nyingi kwa ajili ya kilimo, utalii, na nishati ya mazingira.

Kiuchumi, shughuli za kilimo ndizo nguzo kuu ya uchumi wa Mkoa wa Kigoma, zikiajiri zaidi ya asilimia 70 ya wakazi. Mazao ya chakula kama mahindi, mihogo, na maharage huzalishwa kwa wingi, huku mazao ya biashara kama michikichi (mawese) na kahawa yakichangia mapato ya kaya na mkoa. Kigoma ni miongoni mwa wazalishaji wakuu wa mafuta ya mawese nchini, na uwekezaji katika uchakataji wa zao hili umeanza kuonesha matokeo chanya. Mfano halisi ni Trolle Messle Tanzania Investment Limited, kiwanda cha kuchakata mafuta ya kula ya mawese, ambacho kinaongeza thamani ya malighafi za ndani, kuunda ajira, na kuchochea mnyororo wa thamani wa kilimo cha michikichi.

Ziwa Tanganyika ni rasilimali muhimu kwa uvuvi wa kibiashara, hususan wa samaki aina ya dagaa na migebuka, ambao husambazwa ndani na nje ya mkoa. Sekta hii ina mchango mkubwa katika usalama wa chakula, ajira, na mapato ya biashara, ingawa bado inahitaji uwekezaji zaidi katika teknolojia za uvuvi, uhifadhi wa samaki, na usindikaji ili kuongeza tija na thamani ya mauzo. Uvuvi na usindikaji wa mazao ya ziwa ni eneo lenye uwezo mkubwa wa kuvutia uwekezaji wa ndani na nje.

Sekta ya utalii ni eneo linalochipukia kwa kasi katika Mkoa wa Kigoma. Vivutio vikuu ni Hifadhi ya Taifa ya Gombe, maarufu kwa sokwe waliotafitiwa na Dkt. Jane Goodall, pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Mahale, inayojulikana kimataifa kwa sokwe na mandhari ya kipekee ya Ziwa Tanganyika. Utalii wa ikolojia, utalii wa utafiti, na utalii wa mazingira ya maji vina nafasi kubwa ya kuchangia mapato ya mkoa iwapo vitaunganishwa ipasavyo na huduma za sekta binafsi kama malazi, usafiri, na bidhaa za ndani.

Kwa upande wa miundombinu na biashara, Kigoma ni kitovu muhimu cha biashara ya mipakani. Bandari ya Kigoma inaunganisha Tanzania na Burundi, DRC, na Zambia kupitia usafiri wa majini, huku Reli ya Kati (Central Line) na mtandao wa barabara vikiboresha usafirishaji wa bidhaa na watu kwenda mikoa mingine. Maboresho yanayoendelea katika miundombinu ya usafiri

na nishati yanaongeza ushindani wa mkoa kama kitovu cha biashara na uwekezaji wa kikanda.

Mkoa wa Kigoma una fursa nyingi za kimkakati, zikiwemo kilimo cha kibiashara cha michikichi, kahawa, na mazao ya chakula kwa ajili ya soko la ndani na nje; uanzishaji na upanuzi wa viwanda vya kuchakata mafuta ya mawese, kahawa, na mazao ya ziwa; uvuvi wa kibiashara na usindikaji wa samaki kutoka Ziwa Tanganyika; utalii wa ikolojia, utafiti, na mazingira katika Hifadhi za Gombe na Mahale; na biashara ya mipakani na kikanda kupitia Bandari ya Kigoma na usafiri wa majini.

Pamoja na fursa zilizopo, mkoa unakabiliwa na changamoto kadhaa, zikiwemo miundombinu ya barabara na nishati katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji ambayo bado haijaimarika kikamilifu, upungufu wa mitaji na huduma za kifedha kwa MSMEs na wawekezaji wadogo, changamoto za teknolojia na uhifadhi katika sekta ya uvuvi, na gharama za usafirishaji kutokana na umbali wa mkoa kutoka masoko makuu ya kitaifa.

Mkoa wa Kigoma ni mkoa wenye umuhimu mkubwa wa kimkakati kwa uchumi wa taifa, ukiwa lango la biashara ya kikanda katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Hivyo basi, kuimarisha ushirikiano kati ya Chemba ya Biashara, Serikali za Mkoa na Wilaya, pamoja na wadau wa sekta binafsi, ni hatua muhimu katika kufungua kikamilifu fursa za kilimo, viwanda, uvuvi, utalii, na biashara ya mipakani. Hatua hizi zitachangia kukuza uchumi wa Kigoma na kuimarisha mchango wake katika maendeleo endelevu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 2.16. Mkoa wa Katavi

Mkoa wa Katavi upo Magharibi mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa mipya iliyoundwa rasmi mwaka 2012 baada ya kugawanywa kutoka Mkoa wa Rukwa. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Katavi una idadi ya watu takribani milioni 1.2, hali inayoonesha uwepo wa nguvu kazi inayokua pamoja na soko la ndani lenye fursa za biashara. Katavi ni mkoa wenye nafasi kubwa ya kimkakati kutokana na ardhi yake yenye rutuba, rasilimali asilia, na ukaribu wake na masoko ya kikanda katika Ukanda wa Maziwa Makuu.




Uongozi wa TNCC Katavi

Kijiografia, Katavi inapakana na Mkoa wa Kigoma upande wa Kaskazini, Mkoa wa Rukwa upande wa Kusini, Mkoa wa Tabora upande wa Mashariki, na Ziwa Tanganyika pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) upande wa Magharibi. Jiografia ya mkoa huu inajumuisha mabonde makubwa yenye rutuba, mito mikuu kama Mto Rukwa, na maeneo makubwa ya hifadhi za wanyamapori.

Kiuchumi, kilimo ndicho uti wa mgongo wa uchumi wa Mkoa wa Katavi, kikiajiri zaidi ya asilimia 75 ya wakazi. Mazao makuu yanayozalishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, maharage, karanga, na alizeti, yakinufaika na ardhi yenye rutuba na mvua za kutosha. Mkoa una uwezo mkubwa wa kuwa ghala la chakula katika Ukanda wa Magharibi mwa Tanzania. Ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, na kondoo nao una nafasi muhimu, ukitoa malighafi kwa viwanda vya maziwa, nyama, na ngozi, pamoja na kuchangia usalama wa chakula na mapato ya kaya.

Katavi inaanza kushuhudia ukuaji wa viwanda vinavyotegemea malighafi za ndani. Mfano ni NONDO INVESTORS LIMITED, kiwanda cha kuchakata nafaka na mafuta ya kula ya alizeti, ambacho kinaonesha fursa kubwa ya kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la alizeti mkoani humo. Vilevile, MSS Group of Companies Ltd, kiwanda cha kuchakata maziwa, ni mfano wa uwekezaji unaoongeza thamani ya mazao ya mifugo na kuimarisha soko la maziwa kwa wakulima na wafugaji wa ndani. Viwanda hivi vinaonesha kwa vitendo dhamira ya TNCC ya kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo na vya kati vinavyotumia rasilimali za ndani.

Sekta ya utalii ni eneo lenye fursa kubwa lakini bado halijatumika kikamilifu. Hifadhi ya Taifa ya Katavi, ambayo ni ya nne kwa ukubwa nchini Tanzania, ni miongoni mwa hifadhi zenye wanyamapori wengi na mandhari asilia isiyoharibiwa. Utalii wa ikolojia, utalii wa picha, na utalii wa kitalii wa hali ya

juu (exclusive tourism) vinaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa mapato ya mkoa kupitia uwekezaji katika hoteli, kambi za watalii, usafiri, na huduma saidizi.

Katavi pia ina rasilimali za madini kama dhahabu, shaba, na makaa ya mawe, ambazo bado ziko katika hatua za awali za uchimbaji. Endapo zitafanyiwa uwekezaji wa kimkakati na wa uwajibikaji, rasilimali hizi zinaweza kuchangia mapato ya mkoa, ajira, na maendeleo ya miundombinu. Aidha, ukaribu wa mkoa na Ziwa Tanganyika unaongeza fursa katika uvuvi na biashara ya mipakani, hususan na nchi jirani za DRC.

Serikali imeendelea kuboresha barabara zinazounganisha Katavi na mikoa jirani kama Tabora, Rukwa, na Kigoma. Maboresho ya miundombinu ya nishati na mipango ya kuimarisha usafiri wa majini kupitia Ziwa Tanganyika ni nyenzo muhimu katika kupunguza gharama za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa, jambo linaloendana na ajenda ya TNCC ya kuboresha mazingira ya biashara.

Mkoa wa Katavi una fursa nyingi za kimkakati, zikiwemo kilimo cha kibiashara cha mazao ya chakula na biashara, hususan alizeti, mpunga, na mahindi; uanzishaji na upanuzi wa viwanda vya kuchakata mafuta ya kula, nafaka, na maziwa; ufugaji wa kisasa na viwanda vya mazao ya mifugo (maziwa, nyama, na ngozi); utalii wa ikolojia na uwekezaji katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi; uchimbaji na usindikaji wa madini kwa kuzingatia kanuni za uwajibikaji; na uvuvi na biashara ya mipakani kupitia Ziwa Tanganyika.

Pamoja na fursa hizo, mkoa unakabiliwa na changamoto kadhaa, zikiwemo upungufu wa mbegu bora za mazao ya biashara kama alizeti, hali inayopunguza uzalishaji wa viwanda; ukatikaji wa umeme usio wa uhakika, unaoathiri uzalishaji viwandani na kuongeza gharama za uendeshaji; miundombinu ya barabara na nishati katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji bado kuwa dhaifu; sera na mifumo dhaifu ya kulinda ubora wa mazao ya mifugo, hususan maziwa kutoka kwa wafugaji; na umbali wa mkoa kutoka masoko makuu ya kitaifa, unaoongeza gharama za usafirishaji.

## 2.17. Mkoa wa Rukwa

Mkoa wa Rukwa upo Magharibi mwa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye mchango mkubwa katika uzalishaji wa chakula na rasilimali asilia. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, mkoa una wakazi takribani milioni 1.5, jambo linaloashiria uwepo wa nguvu kazi kubwa pamoja na soko la ndani linalokua. Rukwa inapakana na Mkoa wa Katavi upande wa Kaskazini, Mkoa wa Mbeya upande wa Mashariki, na Ziwa Tanganyika upande wa Magharibi, pamoja na ukaribu wa mpaka wa kimataifa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Mandhari yake yanajumuisha milima, mabonde yenye rutuba, na ukanda wa Ziwa Tanganyika, hali inayoupa mkoa huu mazingira bora kwa kilimo, ufugaji, na uvuvi. Rukwa ni mkoa wa kimkakati katika kuimarisha usalama wa chakula, biashara ya kikanda, na maendeleo ya viwanda vinavyotegemea malighafi za ndani.

Kiuchumi, kilimo ni uti wa mgongo wa Mkoa wa Rukwa, kikiajiri zaidi ya asilimia 70 ya wakazi. Mazao ya chakula kama mahindi, mpunga, muhogo, na alizeti huzalishwa kwa wingi, huku Rukwa ikitajwa mara kwa mara kuwa miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa mahindi nchini. Mazao ya biashara kama kahawa, tumbaku, na karanga pia yana mchango mkubwa katika mapato ya wakulima na biashara ya mazao ghafi. Mkoa huu una uwezo mkubwa wa kupanua uzalishaji wa kilimo cha kibiashara na kuendeleza viwanda vya kuchakata mazao hayo.

Ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, na kondoo ni shughuli nyingine muhimu kiuchumi, hasa katika wilaya za Sumbawanga na Nkasi. Sekta hii ina uwezo wa kukuza viwanda vya nyama, maziwa, na ngozi, pamoja na biashara ya mifugo katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Kwa upande mwingine wa viwanda na uongezaji thamani, uwepo wa taasisi kama Dew Drop Company and Energy Milling, inayojishughulisha na uchakataji wa maji na usambazaji wa mazao ya chakula, unaonesha mwanzo wa mwelekeo wa viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya ndani. Vilevile, masoko makubwa ya nafaka kama Soko la Wakulima la Mandela yanaonesha umuhimu wa Rukwa kama kitovu cha biashara ya nafaka, yakihusisha wafanyabiashara wa ndani na wa nchi jirani. Haya ni maeneo ambayo TNCC inaona yanaweza kuimarishwa zaidi kupitia uwekezaji katika maghala ya kisasa, usindikaji, na mifumo ya masoko.

Rukwa pia ina rasilimali za madini kama dhahabu, makaa ya mawe, na chuma, ambazo bado hazijachimbwa kikamilifu kwa kiwango cha viwanda. Uwekezaji katika sekta hii unaweza kuongeza mapato ya mkoa na ajira,

endapo utaambatana na miundombinu na sera rafiki kwa wawekezaji. Kwa upande wa uvuvi na biashara ya mipakani, ukaribu wa Rukwa na Ziwa Tanganyika unaifanya kuwa na nafasi muhimu katika uvuvi wa kibiashara na usafirishaji wa bidhaa kwenda nchi jirani kama DRC na Zambia. Bandari ndogo na usafiri wa majini vinaweza kuwa kichocheo kikubwa cha biashara ya kikanda endapo vitaimarishwa.

Sekta ya utalii pia ina nafasi ya kukua, ikihusisha ukanda wa Ziwa Tanganyika, mandhari ya asili, na ukaribu na Hifadhi ya Taifa ya Katavi. Utalii wa mazingira na utalii wa maji unaweza kuvutia uwekezaji katika hoteli, kambi za watalii, na huduma za usafiri. Aidha, miundombinu ya barabara inayounganisha Rukwa na Mbeya, Katavi, na Tabora inaendelea kuboreshwa, lakini bado kuna haja ya kuimarisha nishati ya uhakika, maghala, na miundombinu ya masoko ili kupunguza upotevu wa mazao na gharama za usafirishaji.

Rukwa ina fursa kubwa katika uzalishaji na usindikaji wa mazao ya chakula kama mahindi na mpunga, pamoja na mazao ya biashara kama kahawa na tumbaku; ufugaji wa kisasa na viwanda vya mazao ya mifugo; uwekezaji katika maghala na masoko ya nafaka kwa ajili ya biashara ya kikanda; uchimbaji na usindikaji wa madini; maendeleo ya uvuvi na usafirishaji wa majini kupitia Ziwa Tanganyika; pamoja na utalii wa mazingira na uwekezaji katika huduma za malazi na usafiri.

Pamoja na fursa hizo, mkoa unakabiliwa na changamoto za miundombinu hafifu ya barabara na nishati katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji; ukosefu wa pembejeo bora za kilimo na mbegu zenye tija; upungufu wa viwanda vikubwa vya kuchakata mazao; gharama kubwa za usafirishaji kwenda masoko makuu ya kitaifa; pamoja na mifumo isiyo imara ya masoko na uhifadhi wa mazao ambayo husababisha upotevu baada ya mavuno.

## 2.1. Mkoa wa Songwe

Mkoa wa Songwe upo Kusini-Magharibi mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa mipya nchini, ukiwa ulianzishwa rasmi mwaka 2016 baada ya kugawanywa kutoka Mkoa wa Mbeya. Songwe ni mkoa wenye nafasi ya kipekee ya kimkakati kutokana na ujumuisho wake wa rasilimali asilia, miundombinu ya biashara, na urithi wa kiutamaduni. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, idadi ya wakazi wa mkoa huu ni karibu milioni 1.2, nguvu kazi inayohitajika kwa shughuli za kilimo, biashara, na viwanda vya kibiashara. Songwe inapakana na Zambia

upande wa Magharibi, Mkoa wa Rukwa upande wa Kaskazini, Mkoa wa Mbeya upande wa Mashariki, na Ziwa Rukwa upande wa Kaskazini-Magharibi. Jiografia hii inaainishwa na mabonde yenye rutuba, milima, pamoja na fukwe za ziwa zinazoendana na hali ya hewa ya mkoa inayofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali na ufugaji wa mifugo, jambo linaloipa Songwe sifa ya mkoa wa kilimo na biashara.




Mpaka Tanzaniavs Zambia/Ofisi ya mkuu wa mkoa Songwe

Kiuchumi, sekta ya kilimo imekuwa nguzo kuu ya uchumi wa Mkoa wa Songwe. Mazao ya chakula kama mahindi, mpunga, maharage, na alizeti yanastawi vizuri kutokana na ardhi yenye rutuba na hali ya hewa ya mvua inayoweza kutabirika. Songwe pia ni miongoni mwa mikoa inayozalisha tumbaku kwa kiwango kikubwa nchini, na zao hili linatoa nafasi kubwa kwa biashara ya kimataifa na uwekezaji wa viwanda wa kuongeza thamani, kama vile viwanda vya kusindika tumbaku na usafirishaji wa bidhaa za tumbaku katika masoko ya nje.

Sekta ya mifugo pia ina mchango mzito muhimu, hasa ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, na kondoo, ambao hutoa malighafi kwa viwanda vya maziwa, ngozi, na nyama. Kuna fursa kubwa ya kuimarisha viwanda vya kuchakata maziwa na bidhaa za ngozi ili kuongeza thamani ya uzalishaji wa mifugo na kupeleka bidhaa bora sokoni ndani na nje ya nchi. Kwa upande mwingine, Songwe pia ina rasilimali za madini zinazojumuisha dhahabu, makaa ya mawe, chuma, na madini ya vito, ambazo zinatoa fursa kubwa kwa uwekezaji katika sekta ya uchimbaji na usindikaji wa madini. Hata hivyo, changamoto za ukusanyaji wa taarifa za rasilimali, udhibiti wa mazingira, na bei za pembejeo zinahitaji sera na usimamizi thabiti ili kuvutia wawekezaji kwa urahisi.

Songwe ni eneo lenye miundombinu ya kimkakati inayoboresha biashara na usafirishaji wa bidhaa, hasa kupitia barabara kuu ya kimataifa ya Tunduma–

Chingola/Ndola inayounganisha Tanzania na Zambia. Lango la mpakani la Tunduma–Nakonde ni mojawapo ya viunganisho muhimu vya biashara ya bidhaa za tani, usafirishaji wa mizigo, na uhamisho wa bidhaa za viwandani. Uwepo wa barabara hii kuu na mipango ya kuimarisha miundombinu ya nishati unaifanya Songwe kuwa lango muhimu la biashara ya transit, biashara ya kimataifa, na uwekezaji wa uzalishaji wa viwanda.




Kikao na uongozi TNCC Songwe

Sekta ya utalii pia ina nafasi kubwa ya ukuaji, ikiwemo vivutio kama Maporomoko ya Kalambo, maeneo ya kihistoria, na Ziwa Rukwa. Vivutio hivi vinaweza kuunganishwa na huduma za vituko (eco-tourism), huduma za hoteli, usafiri wa majini, na shughuli za utalii wa mazingira. Uwekezaji katika huduma za utalii zenye ubora wa kimataifa unaweza kuongeza mapato ya mkoa na kuvutia watalii wengi zaidi.

Fursa za biashara na uwekezaji mkoani Songwe ni kama vile kilimo cha kibiashara, ambapo Songwe ina ardhi yenye rutuba na hali ya hewa inayofaa kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kama tumbaku, mahindi, alizeti, na maharage. Fursa kubwa ni uwekezaji katika uzalishaji wa mbegu bora, umwagiliaji wa kisasa, na kilimo cha mkataba unaounganisha wakulima na masoko ya ndani na nje ya nchi. Ufugaji wa mifugo una nafasi ya kuimarishwa kwa kuwekeza katika viwanda vya maziwa, mipango ya ubora wa ngozi, na biashara ya bidhaa za nyama na maziwa kwa kiwango cha kimataifa. Uwepo wa Ziwa Rukwa unaifanya Songwe kuwa na fursa ya uwekezaji katika uvuvi wa kibiashara, usindikaji wa samaki, na huduma za usafiri wa majini kwa masoko ya ndani na ya nje. Vivutio kama Maporomoko ya Kalambo na fukwe za Ziwa Rukwa vinatoa nafasi ya kubuni huduma za utalii wa mazingira, hoteli, burudani, na usafiri wa watalii. Kipengele cha kimkakati cha biashara ya transit kupitia Tunduma–Nakonde kina nafasi ya kuvutia uwekezaji wa miundombinu ya kuhifadhi mizigo (logistics hubs), maghala ya kisasa, na huduma za usafirishaji wa kimataifa.

Pamoja na fursa zilizopo, Mkoa wa Songwe unakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa viwanda na uzalishaji mkubwa, hali inayoweza kupunguza tija ya uzalishaji na kuchochea matumizi ya jenereta ghali, Upungufu wa mbegu bora za mazao ya biashara, hasa tumbaku na alizeti, umeathiri uzalishaji wa viwanda vya kuchakata mazao hayo, Soko la bidhaa za kilimo linakabiliwa na changamoto za ukosefu wa maghala ya kuhifadhi na masoko ya kisasa, jambo linaloongeza upotevu wa mazao baada ya mavuno, Changamoto za gharama za ushuru, tozo, na mwendelezo wa sera kwa wafanyabiashara wa mipakani zinaweza kuathiri uhamaji wa bidhaa na uwekezaji wa biashara ya kimataifa. Sekta ya uchimbaji wa madini inahitaji udhibiti madhubuti wa mazingira na sera thabiti ili kuhakikisha uwekezaji endelevu bila kuharibu rasilimali za asili.

## 2.19. Mkoa wa Ruvuma

Mkoa wa Ruvuma upo Kusini mwa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye rasilimali nyingi za asili pamoja na historia pana ya kijamii na kiuchumi. Ulianzishwa rasmi mwaka 1974 baada ya kugawanywa kutoka Mkoa wa Mtwara. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, mkoa una wakazi takribani milioni 1.8, idadi inayotoa nguvu kazi muhimu kwa uzalishaji wa kilimo, biashara, na huduma. Ruvuma inapakana na Mkoa wa Njombe (Kaskazini), Mkoa wa Morogoro (Kaskazini-Mashariki), Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara (Mashariki), Mkoa wa Mbeya (Magharibi), na Msumbiji (Kusini). Mandhari ya mkoa yanajumuisha milima ya Matengo, mabonde yenye rutuba, na misitu mikubwa, hali inayoupa mkoa uwezo mkubwa wa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Hali ya hewa ya wastani yenye mvua za kutosha inaifanya Ruvuma kuwa moja ya maeneo muhimu kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini.

Sekta ya kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Mkoa wa Ruvuma. Mkoa ni mzalishaji mkubwa wa mahindi, mpunga, mihogo, na maharage, ambayo huchangia usalama wa chakula wa ndani na biashara ya mazao kati ya mikoa. Mazao ya biashara kama kahawa (hasa katika Wilaya za Mbinga na Nyasa), chai, korosho, na tumbaku pia yana nafasi muhimu katika mapato ya wakulima na biashara za usafirishaji wa mazao nje ya mkoa na nje ya nchi. Uwepo wa mashamba makubwa na wakulima wadogo unatoa fursa ya kuimarisha kilimo cha mnyororo wa thamani kwa kuanzisha viwanda vya kuchakata kahawa, korosho, na mazao ya nafaka.

Ruvuma pia ina rasilimali nyingi za misitu ya asili na ya kupandwa, ambazo zimechochea uwekezaji katika sekta ya mazao ya misitu. Kampuni kama Green Resources zimewahi kuwekeza katika misitu ya kupandwa na usindikaji wa mazao ya miti katika ukanda huu. Hii inaipa mkoa fursa ya kuendeleza viwanda vya mbao, samani, na karatasi, endapo uwekezaji wa teknolojia na usimamizi endelevu wa misitu utaimarishwa.

Katika sekta ya madini, Ruvuma ina rasilimali kama makaa ya mawe, chuma, na madini mengine ya viwandani, pamoja na maeneo yenye dalili za dhahabu. Aidha, mito na maporomoko ya maji yana uwezo wa kuzalisha umeme wa maji (mini-hydropower) kwa matumizi ya viwanda vidogo na jamii za vijijini. Hata hivyo, sekta hii bado inahitaji tafiti zaidi za kina na uwekezaji katika miundombinu ili kufikia uzalishaji wa kibiashara.

Kwa upande wa utalii, Ruvuma ina vivutio vya kipekee vya kihistoria na kiasili. Maporomoko ya Majimaji, yenye historia ya harakati za kupinga ukoloni (Vita vya Majimaji), pamoja na ukaribu wake na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (zamani Selous Game Reserve), vinaifanya Ruvuma kuwa na uwezo mkubwa wa kuendeleza utalii wa kihistoria na wa mazingira. Uwekezaji katika miundombinu ya hoteli, huduma za watalii, na utangazaji wa vivutio hivi unaweza kuongeza mchango wa utalii katika pato la mkoa.

Ruvuma ina fursa kubwa katika kilimo cha kibiashara kutokana na ardhi kubwa yenye rutuba na hali ya hewa inayofaa kwa mazao ya chakula na biashara. Uwekezaji katika viwanda vya kuchakata kahawa, korosho, nafaka, na maziwa unaweza kuongeza thamani ya mazao kabla ya kuuzwa nje ya mkoa. Sekta ya misitu na mazao ya miti ina nafasi ya kukuza viwanda vya mbao na bidhaa za samani. Aidha, uwekezaji katika utalii wa kihistoria na mazingira unaweza kuchochea ajira na mapato ya ndani. Biashara ya mpakani na Msumbiji pia ni eneo lenye uwezo mkubwa wa kukuza masoko ya bidhaa za kilimo na viwandani.

Pamoja na fursa zilizopo, Ruvuma inakabiliwa na changamoto kadhaa. Miundombinu ya usafiri, hasa barabara za vijijini zinazounganisha maeneo ya uzalishaji na masoko, bado inahitaji kuboreshwa. Upatikanaji wa umeme wa uhakika ni changamoto kwa viwanda vya kuchakata mazao na uwekezaji katika viwanda vikubwa. Sekta ya kilimo inakabiliwa na changamoto za bei zisizo thabiti za mazao ya biashara, upungufu wa mitaji, na teknolojia za kisasa za kilimo. Aidha, uwekezaji katika sekta ya madini na misitu unahitaji usimamizi madhubuti wa mazingira ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali.

## 2.20. Mkoa wa Arusha

Mkoa wa Arusha upo Kaskazini mwa Tanzania na ni moja ya maeneo yenye mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa kupitia utalii, biashara, kilimo cha kibiashara, na huduma za kimataifa. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, Mkoa wa Arusha una wakazi zaidi ya milioni 2.3, hali inayoupa nguvu kazi na soko la ndani linalokua kwa kasi. Jiji la Arusha ni kitovu cha shughuli za kidiplomasia na kibiashara Afrika Mashariki, likiwa mwenyeji wa taasisi za kikanda na kimataifa, mikutano ya kimataifa, na shughuli za utalii wa kiwango cha juu.

Kihistoria, Arusha ni eneo lenye umuhimu mkubwa kisiasa na kijamii nchini, likihusishwa na matukio muhimu ya kitaifa kama Azimio la Arusha la mwaka 1967. Leo, mkoa unaendelea kuwa kitovu cha mikutano ya kikanda kupitia taasisi kama Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na mashirika ya kimataifa, hali inayochochea ukuaji wa sekta za hoteli, usafiri wa anga, na huduma za mikutano (MICE – Meetings, Incentives, Conferences and Exhibitions).

Kijiografia, Arusha inapakana na Mkoa wa Kilimanjaro (Mashariki), Mkoa wa Manyara (Kusini), Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Mara (Magharibi), na Kenya upande wa Kaskazini. Ukaribu wake na mpaka wa Namanga na nchi ya Kenya unaifanya kuwa lango muhimu la biashara ya mipakani na usafirishaji wa watalii na bidhaa kati ya Tanzania na Afrika Mashariki.

Kiuchumi, Arusha ni kitovu cha utalii wa kimataifa nchini Tanzania. Mkoa unahudumia mzunguko wa utalii wa kaskazini (Northern Circuit) unaojumuisha vivutio kama Hifadhi ya Taifa ya Arusha, Mlima Meru, na Ziwa Duluti, na pia ni lango la kuelekea Serengeti, Ngorongoro, na Kilimanjaro. Utalii huu umechochea uwekezaji mkubwa katika hoteli za hadhi ya juu, kampuni za utalii, usafirishaji wa watalii, huduma za chakula, na sanaa za mikono. Makampuni mengi ya utalii yana makao yake Arusha, yakihudumia masoko ya Ulaya, Marekani, na Asia.

Katika sekta ya kilimo cha kibiashara, Arusha ni maarufu kwa uzalishaji wa kahawa, maua ya bustani (horticulture), mboga, na matunda yanayosafirishwa kwenda masoko ya kimataifa kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Mashamba ya maua katika maeneo ya Meru na Arumeru, pamoja na usindikaji wa mazao ya bustani, ni sehemu muhimu ya uchumi wa mkoa. Sekta hii imevutia uwekezaji wa kampuni za ndani na nje zinazojihusisha na uzalishaji na usafirishaji wa mazao mabichi.





Ziara A TO Z

Sekta ya viwanda pia inaendelea kukua Arusha, hasa viwanda vinavyosindika mazao ya kilimo, viwanda vya bidhaa za ngozi, chakula na vinywaji, pamoja na viwanda vya nguo. Mfano wa uwekezaji mkubwa wa viwanda ni A to Z Textile Mills Ltd, sehemu ya A-Z Group of Companies, ambayo imekua kutoka uzalishaji mdogo hadi kuwa kundi la kampuni lenye shughuli za kimataifa katika sekta ya nguo, bidhaa za afya, na viwanda vingine. Uwekezaji wa aina hii unaonyesha uwezo wa Arusha kuwa kitovu cha uzalishaji wa viwanda vinavyotegemea malighafi za ndani na masoko ya nje.





Miundombinu ya Arusha ni miongoni mwa bora nchini, ikijumuisha barabara kuu zinazounganisha na Nairobi, Dodoma, na mikoa ya kaskazini, pamoja na viwanja vya ndege vya Kilimanjaro International Airport (KIA) na Arusha Airport. Uwepo wa taasisi za kifedha, vyuo vikuu, na taasisi za mafunzo ya kimataifa unaongeza ubora wa rasilimali watu na mazingira ya uwekezaji.

Mkoa wa Arusha una fursa kubwa katika utalii wa kimataifa, hasa katika uwekezaji wa hoteli, huduma za mikutano, usafiri wa watalii, na utalii wa mazingira. Sekta ya kilimo cha bustani na maua inaendelea kutoa fursa za

uwekezaji katika uzalishaji, uhifadhi baridi (cold chain logistics), na usafirishaji wa mazao nje ya nchi. Arusha pia ina uwezo mkubwa wa kukuza viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, viwanda vya ngozi, na bidhaa za walaji. Aidha, nafasi yake kama kitovu cha mikutano ya kimataifa inatoa fursa kwa biashara za huduma, teknolojia ya mikutano, na ubunifu wa huduma za kidijitali.

Licha ya mafanikio, Arusha inakabiliwa na changamoto kadhaa, zikiwemo gharama kubwa za uendeshaji wa biashara, hasa kodi za majengo, gharama za ardhi, na huduma za mijini. Sekta ya utalii inakumbwa na msimu wa wageni (seasonality) unaoathiri mapato ya mwaka mzima. Wakulima wa mazao ya bustani hukumbana na changamoto za mabadiliko ya bei za soko la kimataifa, viwango vya ubora vinavyobadilika, na gharama za usafirishaji wa anga. Aidha, ukuaji wa miji unahitaji mipango bora ya matumizi ya ardhi ili kuepusha migongano kati ya makazi, kilimo, na uwekezaji wa viwanda.

## 2.21. Mkoa wa Iringa

Mkoa wa Iringa upo Kusini mwa Tanzania katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini, na ni miongoni mwa mikoa yenye mchango mkubwa katika uzalishaji wa kilimo, utalii wa hifadhi, na viwanda vya usindikaji wa mazao. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Iringa una wakazi takribani milioni 1.2, hali inayotoa nguvu kazi muhimu kwa shughuli za kiuchumi pamoja na soko la ndani linalokua.

Kihistoria, Iringa ina nafasi muhimu katika historia ya Tanzania, ikihusishwa na harakati za kupinga ukoloni. Utamaduni wa Wahehe ni sehemu ya utambulisho wa mkoa huu na unaendelea kuwa kivutio cha kitamaduni na kijamii. Kijiografia, Iringa inapakana na Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Singida upande wa Kaskazini, Mkoa wa Morogoro upande wa Mashariki, Mkoa wa Njombe upande wa Kusini, na Mkoa wa Mbeya upande wa Magharibi. Mkoa huu upo katika nyanda za juu zenye hali ya hewa ya baridi hadi ya wastani, inayofaa kwa kilimo cha mazao ya biashara na chakula.

Sekta ya kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Iringa. Mkoa unazalisha kwa wingi mahindi, ambayo ni zao la chakula na biashara, pamoja na alizeti, maharage, viazi, na mbogamboga katika maeneo ya nyanda za juu. Mazao ya biashara kama chai (hususan wilayani Mufindi), kahawa, na alizeti yana mchango mkubwa katika kipato cha wakulima na uchumi wa mkoa. Iringa pia ni moja ya mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa asali yenye ubora wa

juu, inayopata masoko ndani na nje ya nchi. Uwekezaji katika minyororo ya thamani ya mazao haya unaendelea kuongezeka.

Katika sekta ya utalii, Iringa ni lango la kuelekea Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, ambayo ni miongoni mwa hifadhi kubwa zaidi barani Afrika na inajulikana kwa wingi wa tembo, simba, na mandhari ya kipekee ya savanna na mito. Vivutio vingine ni pamoja na Mapango ya Isimila, yenye ushahidi wa kihistoria wa kale wa binadamu. Utalii umechochea uwekezaji katika hoteli, lodges, kambi za watalii, usafirishaji wa watalii, na huduma za chakula, na kutoa ajira kwa vijana na jamii zinazozunguka hifadhi.

Kwa upande wa viwanda na usindikaji, Iringa inaendelea kuwa kitovu cha usindikaji wa mazao ya kilimo, hususan nafaka. Mfano ni Ruaha Milling Company Limited (RMC), inayojihusisha na uchakataji na ufungashaji wa mchele na unga wa mahindi. Uwekezaji wa aina hii unaongeza thamani ya mazao ya wakulima na kupanua fursa za masoko ya ndani na nje. Mkoa pia una fursa katika usindikaji wa alizeti kuwa mafuta ya kula, maziwa, mazao ya misitu, na bidhaa za asali. Aidha, uwepo wa rasilimali za maji na miradi mikubwa ya nishati kama Bwawa la Mwalimu Nyerere unaongeza uhakika wa nishati kwa maendeleo ya viwanda katika ukanda wa kusini.






Ziara ofisi za TNCC Iringa

Miundombinu ya Iringa imeimarika kwa kiwango kikubwa katika miaka ya karibuni. Mkoa unapitiwa na Barabara Kuu ya TANZAM (Dar es Salaam – Zambia), ambayo ni uti wa mgongo wa biashara ya kikanda Kusini mwa Afrika. Pia, kuna mtandao wa barabara za mikoa na wilaya unaorahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo kwenda masoko ya ndani na nje. Uwepo wa umeme wa gridi ya taifa na upanuzi wa huduma za mawasiliano unasaidia kuimarisha mazingira ya biashara.

Iringa ina fursa kubwa katika usindikaji wa mazao ya kilimo kama mahindi, mchele, alizeti, na mazao ya bustani, hali inayoweza kuongeza thamani na ajira. Sekta ya asali ina nafasi ya kupanua uzalishaji na masoko ya kimataifa kupitia uwekezaji katika ubora, vifungashio, na uongezaji thamani. Utalii wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha unaendelea kutoa fursa katika ujenzi wa miundombinu ya malazi, huduma za usafirishaji wa watalii, na utalii wa kiikolojia. Aidha, hali ya hewa ya baridi na ardhi nzuri inafaa kwa uwekezaji katika ufugaji wa kisasa na viwanda vya maziwa, pamoja na fursa za viwanda vinavyotumia nishati ya uhakika kutoka miradi mikubwa ya umeme.

Pamoja na fursa hizo, Iringa inakabiliwa na changamoto kadhaa, zikiwemo upatikanaji wa uhakika wa malighafi za viwandani kutokana na uzalishaji wa wakulima kuwa wa msimu na usio na mikataba thabiti ya masoko. Ukatikaji wa umeme na gharama za nishati bado huathiri uzalishaji wa viwanda vidogo na vya kati. Wafanyabiashara na wasindikaji hukumbana pia na utegemezi mkubwa wa soko la ndani, changamoto za usafirishaji wakati wa mvua katika baadhi ya maeneo ya vijijini, pamoja na mzigo wa kodi na tozo mbalimbali zinazoongeza gharama za uzalishaji na kupunguza ushindani wa bidhaa katika soko la kikanda.

## 2.22. Mkoa wa Kilimanjaro

Mkoa wa Kilimanjaro upo Kaskazini mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na unatajwa miongoni mwa mikoa yenye mchango mkubwa wa kiuchumi kutokana na kilimo, utalii, biashara, na huduma. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Kilimanjaro una idadi ya wakazi inayokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 1.9, ikitoa soko kubwa la ndani pamoja na nguvu kazi ya sekta mbalimbali. Kilimanjaro inapakana na Mkoa wa Tanga upande wa Mashariki, Mkoa wa Manyara upande wa Kusini, Mkoa wa Arusha upande wa Magharibi, na Kenya upande wa Kaskazini. Ukaribu wake na mpaka wa kimataifa unachochea biashara ya mipakani na ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na nchi jirani. Jiografia ya mkoa inajumuisha milima, mabonde, na maeneo ya nyanda za juu zenye hali ya hewa ya baridi hadi wastani, hali inayofaa kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na ufugaji wa kisasa.

Sekta ya kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Kilimanjaro. Mkoa unajulikana kimataifa kwa uzalishaji wa kahawa ya Arabica ya Kilimanjaro, ambayo ina soko la kimataifa na inaleta mapato kwa wakulima wengi. Mbali

na kahawa, mkoa pia huzalisha viazi mviringo, mazao ya mboga, matunda, maua ya bustani (horticulture), na mazao ya kibiashara yanayoenda masoko ya ndani na nje ya nchi. Sekta hii ina fursa kubwa ya kuendelezwa zaidi kupitia uwekezaji katika uzalishaji wa mbegu bora, umwagiliaji wa kisasa, maghala ya kuhifadhi mazao (cold storage), na viwanda vya kuongezea thamani malighafi za kilimo. Hata hivyo, changamoto kubwa ni upungufu wa mitaji kwa wakulima wadogo, upatikanaji wa pembejeo za kisasa, na uhaba wa mikataba ya masoko ya muda mrefu.

Utalii ni sekta nyingine ya msingi kwa uchumi wa Kilimanjaro. Vivutio kama Mlima Kilimanjaro—mlima mrefu zaidi barani Afrika—na Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro huvutia maelfu ya watalii kila mwaka na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ajira na huduma za kitalii kama hoteli, usafiri wa watalii, na shughuli za burudani. Katika maeneo kama Wilaya ya Same, maeneo ya kipekee yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji viwandani na kilimo cha mkonge (ekari 8,000), pamoja na maeneo ya madini kama dhahabu, bauxite, gypsum, na limestone, ni fursa zilizobainishwa zinazoweza kuvutia uwekezaji wa ndani na nje. Changamoto katika sekta ya utalii ni pamoja na kutegemea misimu na upungufu wa miundombinu ya kiutalii yenye viwango vya kimataifa katika maeneo ya mbali.

Miundombinu ya usafiri na huduma za anga inachangia pakubwa ukuaji wa uchumi wa Kilimanjaro. Uwepo wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro unarahisisha usafiri wa kimataifa, utalii, na biashara ya haraka ya bidhaa zenye thamani ya juu kama maua na matunda. Aidha, barabara kuu zinazounganisha mkoa huu na mikoa jirani na nchi jirani hufanya Kilimanjaro kuwa lango muhimu la biashara ya kikanda.

Mkoa wa Kilimanjaro una fursa nyingi za kiuchumi. Kilimo cha kibiashara kina nafasi kubwa ya kupanuliwa kupitia uzalishaji wa kahawa, viazi mviringo, maua, na matunda, na kuingizwa katika masoko ya kimataifa. Utalii wa kimataifa unaendelezwa zaidi kwa kuwekeza katika huduma za malazi za hali ya juu, usafiri wa vituko (adventure tourism), na huduma za usaidizi. Sekta ya viwanda vya usindikaji ina nafasi ya kukua, ikijumuisha viwanda vya nguo, ngozi, na nishati mbadala. Aidha, kwa sababu ya ukaribu na Kenya, biashara ya mipakani na masoko ya kikanda ina fursa ya ukuaji kupitia miundombinu bora ya usafirishaji na ushirikiano wa kitaasisi.

Changamoto za mkoa ni pamoja na ushindani wa bei za bidhaa za kilimo sokoni kimataifa, upungufu wa mtaji na huduma za kifedha kwa wakulima na viwanda vidogo, changamoto za msimu wa utalii unaoathiri mapato ya mwaka mzima, gharama za juu za uzalishaji wa viwanda, na changamoto

za uratibu wa sera kati ya ngazi za serikali na wafanyabiashara. Pia, baadhi ya maeneo ya mbali yanakosa miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji wa haraka wa mazao.

## 2.23. Mkoa wa Manyara

Mkoa wa Manyara upo Kaskazini mwa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye mandhari asilia ya kipekee, urithi wa kiutamaduni, na fursa nyingi za kiuchumi. Ulianzishwa rasmi mwaka 2002, na tangu wakati huo umeendelea kujijenga kama kitovu cha kilimo cha biashara, ufugaji, utalii wa kiikolojia, na shughuli za kibiashara zinazohusiana na soko la Afrika Mashariki. Kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, idadi ya wakazi wa Manyara ni zaidi ya milioni 1.4, huku wakazi wengi wakijihusisha na kilimo, ufugaji, na biashara ndogo ndogo, na hivyo kuifanya sekta binafsi kuwa chachu ya maendeleo ya mkoa. Manyara inapakana na Mkoa wa Arusha upande wa Kaskazini, Mkoa wa Kilimanjaro upande wa Kaskazini-Mashariki, Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Singida upande wa Kusini-Magharibi, na Mkoa wa Dodoma upande wa Kusini. Makundi ya milima, mabonde, na bonde la ufa yanaipa mkoa mazingira bora kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo, ufugaji wa kisasa, na shughuli za umwagiliaji zinazohitaji ardhi yenye rutuba na maji ya kutosha.

Kilimo na ufugaji ni nguzo kuu za uchumi wa Manyara. Mazao ya chakula kama mahindi, mtama, maharage, na mpunga, pamoja na mazao ya biashara kama mbaazi na alizeti, huchangia pakubwa katika pato la kaya na uchumi wa mkoa. Kahawa ya Manyara pia ina soko la ndani na nje ya nchi, ingawa mara nyingi uzalishaji wake umekumbwa na changamoto za pembejeo na masoko. Uwekezaji unaohusiana na viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, ubora wa mbegu, maghala ya uhifadhi ya kisasa (cold storage), na miundombinu ya masoko unaweza kuongeza thamani ya uzalishaji na mapato kwa wakulima na wafanyabiashara.

Ufugaji wa kisasa wa ng'ombe, mbuzi, na kondoo pia ni sehemu muhimu ya uzalishaji wa Manyara, huku malighafi zake kama maziwa na ngozi zikitoa fursa za uwekezaji katika usindikaji wa bidhaa za maziwa na ngozi. Kuanzishwa kwa viwanda vya usindikaji wa maziwa na ngozi, kama vile Maziwa Mtanzania Ltd au sekta za artisanal cheese, kunaweza kukuza ajira na mapato katika mkoa huu.





Ziara ofisi ya mkuu wa mkoa Manyara

Sekta ya utalii wa kiikolojia ni mojawapo ya vipaumbele vya kiuchumi katika Mkoa wa Manyara. Mkoa una vivutio maarufu vya kimataifa kama Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, maarufu kwa simba wanaopanda miti na aina mbalimbali za ndege, pamoja na Hifadhi ya Tarangire, maarufu kwa mkusanyiko wake mkubwa wa tembo na wanyamapori wengine. Utalii huu umeongeza ajira na kuibua fursa za uwekezaji katika malazi ya hadhi mbalimbali, huduma za usafiri wa watalii, watoa huduma wa safari (safari operators), na shughuli zinazohusiana na utalii wa kijamii na wa kifahari. Hata hivyo, changamoto kama msimu wa watalii (seasonality) na upungufu wa huduma za kitalii za hali ya juu katika maeneo ya mbali zinahitaji juhudi za pamoja kati ya sekta binafsi na umma.

Katika upande wa viwanda na usindikaji wa bidhaa, Mkoa wa Manyara una fursa nyingi zinazoibuka. Mfano ni Mati Super Brands Ltd, kampuni ya Kitanzania inayozalisha vinywaji kama Premium Vodka na Strong Dry Gin, ambayo inaonyesha uwekezaji wa kisasa katika teknolojia na rasilimali watu. Viwanda kama hivi vinaweza kupanuliwa zaidi kwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa za ndani na kuchukua nafasi katika masoko ya kimataifa. Fursa nyingine ni pamoja na viwanda vya usindikaji wa ngozi, uzalishaji wa nishati mbadala (biogas, jua), na usindikaji wa mazao ya kilimo kama alizeti na mbaazi






Ziara Mati Superbrands

Kwa upande wa madini, Mkoa wa Manyara una rasilimali kama tanzanite, chokaa, na madini mengine ya viwandani, ambayo yanatoa nafasi ya uwekezaji katika uchimbaji na usindikaji wa madini kwa kutumia teknolojia endelevu. Changamoto hapa ni pamoja na kiwango cha chini cha utafiti na uainishaji wa rasilimali, pamoja na hatari ya uharibifu wa mazingira endapo shughuli za uchimbaji hazitafanyika kwa uwajibikaji.

Miundombinu ya usafiri na huduma za nishati katika Mkoa wa Manyara inaendelea kuboreshwa. Barabara kuu zinazounganisha mkoa na mikoa jirani pamoja na masoko ya Afrika Mashariki, pamoja na huduma za umeme na mawasiliano, zinaongeza ushindani wa mkoa kama kituo cha biashara. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya vijijini bado yanakabiliwa na changamoto za miundombinu dhaifu ya barabara za mwisho wa shoka (last-mile) na upatikanaji wa umeme wa uhakika, jambo linaloathiri uzalishaji wa viwanda na huduma za biashara za kisasa.

Mkoa wa Manyara una fursa kubwa katika kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa mazao ya biashara, uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na bidhaa za ngozi, sekta ya utalii wa kiikolojia, na madini ya thamani kama tanzanite na chokaa. Aidha, uwekezaji katika miundombinu ya kuhifadhi mazao (cold chain, maghala), nishati mbadala, na huduma za usafiri unachangia kukua kwa uchumi wa mkoa na kuimarisha mazingira ya biashara.

Changamoto kuu zinajumuisha miundombinu isiyokamilika ya barabara za vijijini, uhaba wa mtaji na upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wakulima na wafanyabiashara wa MSMEs, changamoto za msimu wa utalii na gharama za uzalishaji, pamoja na changamoto za sera na kodi zisizo rafiki kwa wawekezaji wadogo. Aidha, upungufu wa taarifa za soko la kimataifa

na uhaba wa rasilimali mbadala za nishati unaathiri uwezo wa kukuza viwanda vya kuongeza thamani kikamilifu.

## 2.24. Mkoa wa Mbeya

Mkoa wa Mbeya upo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye mchango mkubwa katika kilimo, biashara, utalii, na viwanda, huku ukiwa na historia ya kipekee na miundombinu ya kimkakati inayounganisha Tanzania na nchi jirani za Zambia na Malawi. Mbeya ni mkoa muhimu kikanda katika kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia sekta binafsi, ukiwa na ardhi yenye rutuba, rasilimali asilia, na miundombinu ya barabara, reli, na anga inayorahisisha biashara ya ndani na nje ya nchi. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, mkoa huu una idadi ya watu inayokadiriwa kufikia milioni 3.0, ikitoa nguvu kazi kubwa katika uzalishaji na huduma mbalimbali.

Kilimo ni sekta kuu ya uchumi wa Mkoa wa Mbeya. Mkoa unajivunia uzalishaji wa mazao ya chakula kama mahindi, mpunga, viazi mviringo, na pareto, pamoja na mazao ya biashara kama kahawa na chai. Kahawa ya Mbeya, inayolimwa katika nyanda za juu, ina soko la kimataifa kutokana na ladha yake na ubora wa kimazingira, jambo linaloifanya kuwa chanzo kikuu cha mapato kwa wakulima. Aidha, uzalishaji wa mbogamboga na matunda unachangia kwa kiasi kikubwa katika masoko ya ndani na ya nje, hasa kupitia Mbeya Food Park, ambayo ni mtandao wa wajasiriamali na viwanda vidogo vinavyotoa huduma za masoko na teknolojia kwa wakulima wa mboga na wafanyabiashara wadogo. Kwa mtazamo wa TNCC, fursa katika kilimo ni pamoja na kuanzishwa kwa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao, mifumo ya umwagiliaji, maghala ya kuhifadhi mazao (cold storage), na mikataba ya masoko ya muda mrefu kwa wakulima wadogo.

Utalii ni sekta nyingine yenye mchango mkubwa kwa uchumi wa Mkoa wa Mbeya. Vivutio vya kiikolojia kama Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, maarufu kwa maua ya porini yanayochanua msimu wa mvua, Maporomoko ya Mto Kalambo, na mandhari ya Mlima Rungwe pamoja na Ziwa Ngozi, vimeifanya Mbeya kuwa kivutio kikubwa kwa watalii wa ndani na wa kimataifa. Utalii huu umechochea uwekezaji katika malazi, huduma za utalii, na shughuli za burudani, na kutoa ajira kwa vijana na wanawake. Fursa za utalii ni pamoja na kuendeleza hoteli za hadhi ya juu na lodges, safari za mazingira (eco-

tourism), na huduma za usafiri wa watalii, hasa kwa kutumia miundombinu ya barabara na anga iliyopo.

Sekta ya viwanda katika Mkoa wa Mbeya inaendelea kukua, hasa katika usindikaji wa mazao ya kilimo kama chai na kahawa, pamoja na uzalishaji wa nishati kupitia miradi ya umeme wa maji (hydropower). Mfano wa uwekezaji wa viwandani ni Mbeya Rice Group Ltd (MRG), ambayo imewekeza katika mashine za kukoboa mpunga na kufungasha mchele, jambo linaloonyesha uwekezaji katika uongezaji thamani wa mazao ya kilimo. Hata hivyo, changamoto kama ukosefu wa maeneo makubwa ya uwekezaji, upatikanaji mdogo wa mikopo kwa viwanda vidogo na vya kati, na gharama za nishati zinahitaji mipango ya sera na ushirikiano kati ya sekta binafsi na umma.



Mkoa wa Mbeya pia una rasilimali za madini kama makaa ya mawe na chokaa, ambazo hutoa fursa kwa uwekezaji katika uchimbaji na sekta ya ujenzi, ikiwa ni pamoja na viwanda vya kusindika chokaa na bidhaa zinazotokana na madini hayo. Aidha, mazingira ya mkoa, ikiwemo mabonde ya ziwa na maeneo ya milima yana nafasi ya kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa nishati mbadala kama jua na upepo, hasa katika maeneo ya pembezoni mwa mkoa.

Miundombinu ya usafirishaji ni nguzo muhimu ya maendeleo ya biashara katika Mkoa wa Mbeya. Barabara kuu zinazounganisha mkoa na nchi za Zambia na Malawi, pamoja na reli ya TAZARA (Tanzania–Zambia Railway Authority) na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, zinachangia kwa kiasi kikubwa kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na watu, hivyo kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Fursa za miundombinu zinajumuisha

kuboresha mtandao wa barabara za vijijini, kupanua huduma za anga kwa mizigo, na kuimarisha huduma za mawasiliano na nishati ili kukuza soko la biashara za kisasa.

Mkoa wa Mbeya una fursa nyingi za uwekezaji wa kiuchumi, zikiwemo kuendeleza uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa njia ya kisasa na viwanda vya kuongeza thamani, utalii wa kiikolojia na kitamaduni kupitia uwekezaji katika malazi na huduma zinazoambatana, uwekezaji katika usindikaji wa chakula na nishati mbadala, pamoja na miradi ya madini ya viwandani. Pia, nafasi ya biashara ya kikanda kupitia barabara na reli inatoa fursa kwa wajasiriamali kushirikiana na masoko ya kimataifa kupitia mikoa jirani na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Licha ya fursa hizo nyingi, Mkoa wa Mbeya unakabiliwa na changamoto kadhaa. Mojawapo ni ukosefu wa mikopo nafuu kwa viwanda vidogo na vya kati, jambo linalozuia upanuzi wa viwanda vinavyotegemea malighafi za ndani. Pia, ukosefu wa maeneo makubwa ya uwekezaji (strategic industrial areas) umekuwa kikwazo kwa viwanda vikubwa vya kuongeza thamani. Changamoto nyingine ni gharama za nishati na ukosefu wa miundombinu ya vijijini, pamoja na changamoto za masoko endelevu ya mazao ya kilimo katika soko la kimataifa. TNCC inasisitiza umuhimu wa sera rafiki za biashara, kuboresha miundombinu ya masoko, na kuimarisha huduma za fedha kwa wajasiriamali.

Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa yenye uwezo mkubwa wa kuchochea ukuaji wa uchumi wa Tanzania kupitia sekta za kilimo, utalii, viwanda, na biashara ya kikanda. Kuimarisha miundombinu ya usafirishaji, kuweka sera rafiki za uwekezaji, na kuimarisha huduma za kifedha kwa MSMEs kutachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo endelevu ya mkoa na nchi kwa ujumla. Mkoa wa Mbeya una nafasi ya kuwa kitovu cha biashara na uwekezaji katika Ukanda wa Kusini mwa Afrika, ukiwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa.

## 2.25. Mkoa wa Njombe

Mkoa wa Njombe upo Kusini mwa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa iliyoundwa hivi karibuni, ulioanzishwa rasmi mwaka 2012 baada ya kugawanywa kutoka Mkoa wa Iringa. Mkoa wa Njombe ni mkoa wenye rasilimali nyingi na fursa za biashara ambazo zinaweza kuchochea ukuaji wa uchumi wa mkoa na Taifa kwa ujumla. Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya

Watu na Makazi ya mwaka 2022, mkoa huu una wakazi takribani milioni 0.8, idadi inayotoa nguvu kazi kwa shughuli za kilimo, biashara, na huduma zinazohusiana na sekta binafsi. Mkoa wa Njombe unapakana na Mkoa wa Iringa upande wa Kaskazini, Mkoa wa Mbeya upande wa Magharibi, Mkoa wa Ruvuma upande wa Kusini, na kwa upande wa Kusini-Magharibi una mipaka ya kimataifa na nchi ya Malawi kupitia Ziwa Nyasa. Jiografia hii inajumuisha milima, mabonde, na maeneo ya nyanda za juu yenye hali ya hewa ya baridi inayofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali na ufugaji wa kisasa.

Kilimo ni nguzo kuu ya uchumi wa Mkoa wa Njombe na ndicho chanzo kikuu cha maisha kwa wakazi wengi. Mazao makuu yanayolimwa ni pamoja na chai, kahawa, mahindi, viazi mviringo, na mazao ya misitu kama miti ya mbao. Hali ya hewa ya baridi na ardhi yenye rutuba imesaidia kilimo cha mazao ya biashara kama chai na kahawa, ambayo huuzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Chai ya Njombe, kwa mfano, ina soko la kikanda na kimataifa, jambo linaloipa mkoa nafasi ya kukuza viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya chai, kama usindikaji wa chai, uzalishaji wa chai za kibiashara (blends), na bidhaa zinazohusiana na kilimo cha chai.

Mkoa wa Njombe pia una rasilimali za misitu ya asili na miti ya kupandwa, ikitoa fursa kubwa kwa sekta ya usindikaji wa mbao, uchakataji wa bidhaa za misitu, na uzalishaji wa nishati mbadala kama vile biomass na umeme wa maji. Mfano wa uwekezaji mkubwa katika sekta hii ni Tanganyika Wattle Company (TANWAT), sehemu ya RAI Group, ambayo huzalisha mbao za aina mbalimbali zinazotumika katika ujenzi, fanicha, na uzalishaji wa nishati ya umeme kutokana na magogo ya miti. Kampuni hii imeonyesha jinsi misitu ya kibiashara inaweza kutumika kuongeza thamani, kutoa ajira, na kuchangia mapato ya mkoa. Hata hivyo, changamoto kubwa inayokumba sekta hii ni mzigo wa kodi, tozo, na ada mbalimbali, zikiwemo gharama za ghala la mizigo, tozo za kusafirisha malighafi, na changamoto za udhibiti wa mazingira.

Ufugaji wa kisasa wa ng'ombe, mbuzi, na kondoo ni eneo jingine lenye mchango mkubwa katika uchumi wa Mkoa wa Njombe. Huku uzalishaji wa maziwa na nyama ukizidi kuwa muhimu kwa chakula na biashara, fursa ni kubwa kwa kuanzisha viwanda vya kusindika maziwa na nyama karibu na maeneo ya uzalishaji. Uwekezaji katika mihimili hii unaweza kusaidia kuongeza thamani ya mazao ya mifugo kabla ya kuingia sokoni, na hivyo kuongeza mapato kwa wakulima na wafanyabiashara.

Uvuvi na utalii pia ni sekta zenye fursa kubwa, hususan kupitia Ziwa Nyasa, ambalo ni chanzo muhimu cha uvuvi wa kibiashara na shughuli za utalii wa maji na burudani. Fursa ya kuendeleza hoteli za pwani ya ziwa, vivutio vya maji, na shughuli za uvuvi wa kisasa inaweza kuchangia ukuaji wa sekta ya huduma na ajira kwa vijana na wanawake. Hata hivyo, changamoto kama mabadiliko ya msimu wa soko na miundombinu duni ya umeme na barabara za kufikia maeneo ya mbali zinaweza kupunguza tija ya uwekezaji kama huo.

Mkoa wa Njombe ni mkoa wa kimkakati kwa biashara ya kikanda kutokana na barabara kuu zinazounganisha maeneo ya kusini mwa Tanzania na nchi jirani za Malawi na Zambia. Uwepo wa Barabara Kuu ya Mbeya–Njombe–Makambako na reli ya TAZARA (Tanzania–Zambia Railway Authority) unarahisisha usafirishaji wa mazao na bidhaa, jambo linalochochea biashara za ndani na za kimataifa. Hata hivyo, changamoto endelevu ni pamoja na miundombinu ya barabara za vijijini ambayo bado haijakamilika kikamilifu, hali inayoongeza gharama za usafirishaji wa bidhaa.

Mkoa wa Njombe una fursa nyingi za kiuchumi, ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa chai na kahawa wenye soko la kimataifa; uwekezaji katika usindikaji wa mazao ya kilimo unaoongeza thamani; usindikaji wa mbao na uzalishaji wa nishati mbadala kama umeme wa biomass; uwekezaji katika viwanda vidogo vya maziwa na nyama unaoweza kuongeza mapato kwa wakulima; Ziwa Nyasa lenye fursa za uwekezaji katika huduma za burudani, hoteli, na uvuvi wa kisasa; pamoja na miundombinu ya barabara na reli inayowezesha biashara ya kimataifa na ya mipakani.

Changamoto kuu zinazokabili mkoa ni pamoja na kodi, tozo, na ada nyingi katika sekta ya misitu na biashara, zinazoongeza gharama za uzalishaji. Miundombinu ya barabara za vijijini na upatikanaji wa umeme wa uhakika bado havijakamilika kikamilifu, hali inayoacha maeneo mengi yasiyofikiwa vyema. Upatikanaji mdogo wa mitaji kwa wakulima na viwanda vidogo unaathiri uwezo wa kupanua uzalishaji, na masoko endelevu ya kimataifa kwa mazao kama chai, kahawa, na mbao bado yanahitaji kuboreshwa kupitia mikataba ya masoko na viwango vya ubora.

## 2.26. Mkoa wa Tanga

Mkoa wa Tanga upo Kaskazini-Mashariki mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni miongoni mwa mikoa yenye historia ya kipekee na mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi. Mkoa wa Tanga ni mkoa wa kimkakati wenye rasilimali nyingi, historia tajiri, na miundombinu muhimu inayochochea biashara ya ndani, kikanda, na kimataifa. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Tanga una idadi ya wakazi inayokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 2.2, na wakazi wengi hutegemea kilimo, biashara ya pwani, ufugaji, uvuvi, na huduma za bandari. Mkoa wa Tanga unapakana na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki, Mikoa ya Kilimanjaro na Manyara upande wa Magharibi, Mkoa wa Pwani upande wa Kusini, na nchi ya Kenya upande wa Kaskazini. Ukaribu na mpaka wa Kenya pamoja na pwani ndefu unaifanya Tanga kuwa lango muhimu la biashara ya kimataifa kupitia mikoa ya ndani na nchi jirani. Mandhari ya mkoa inajumuisha fukwe, bonde la ufa, milima ya Usambara, na misitu ya asili kama Amani Nature Reserve, ambayo ina sifa ya kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi.

Kilimo ni sekta kuu ya uchumi wa Mkoa wa Tanga, kikihusisha uzalishaji wa mazao ya biashara kama mkonge, kahawa, chai, na korosho, pamoja na matunda na mbogamboga. Mazao haya yana soko la ndani na nje ya nchi, hasa katika masoko ya Afrika Mashariki. Kilimo cha umwagiliaji kinaweza kuendelea kupanuka, hasa katika bonde la ufa na maeneo yaliyo chini ya miradi ya maji, kikitoa nafasi kwa uwekezaji wa kisasa wa kilimo cha kibiashara na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao. Hata hivyo, changamoto kubwa kwa kilimo ni pamoja na upungufu wa pembejeo bora, gharama za usafirishaji, na ujumuishaji mdogo wa wakulima katika minyororo ya thamani ya kimataifa, jambo linalohitaji sera na mipango ya ushirikiano kati ya sekta binafsi na umma kupitia TNCC.

Bandari ya Tanga ni mojawapo ya rasilimali kuu za mkoa, ikitoa huduma za usafirishaji kwa mikoa ya ndani na nchi jirani kama Uganda, Rwanda, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Bandari hii ni lango muhimu la biashara ya kimataifa na ya kikanda, na ina nafasi kubwa kwa uwekezaji katika miundombinu ya kuhifadhi mizigo (logistics hubs), njia za reli, na usafiri wa anga.

Sekta ya utalii ni nguzo muhimu ya uchumi wa Mkoa wa Tanga, ikiongozwa na vivutio kama Mji Mkongwe wa Tanga, Hifadhi ya Taifa ya Saadani, eneo la Pangani, na Mapango ya Amboni. Utalii huu una nafasi ya kuvutia

uwekezaji katika hoteli, huduma za safari za utalii, utalii wa mazingira (eco-tourism), na utalii wa pwani, hasa kupitia maendeleo ya vivutio vya baharini kama michezo ya maji na safari za majini.

Sekta ya viwanda inakua polepole katika Mkoa wa Tanga, hasa kupitia usindikaji wa mazao ya kilimo na bidhaa za chakula, matumizi ya nishati mbadala, na uingizaji wa teknolojia mpya. Mfano wa uwekezaji wa viwanda ni Tanga Fresh, kiwanda kinachosindika na kuuza maziwa, ambacho kinaonyesha matumizi ya teknolojia za kisasa katika uzalishaji wa bidhaa za maziwa. Viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uzalishaji wa matunda yaliyosindikwa, uzalishaji wa mafuta ya korosho, na usindikaji wa kahawa vina nafasi kubwa ya kukua.

Njia nyingine ya ukuaji wa mkoa ni Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi (EACOP) unaopitia Chongoleani ndani ya Mkoa wa Tanga, pamoja na miradi ya kuzalisha umeme wa upepo na jua, ambayo inaongeza fursa za uwekezaji katika sekta ya nishati, uchakataji wa mafuta, na huduma za usambazaji wa umeme. Miundombinu ya barabara, reli, na usafiri wa anga ni muhimu katika kuhakikisha ufanisi wa biashara katika Mkoa wa Tanga. Uboreshaji wa miundombinu ya barabara za lami kati ya maeneo ya uzalishaji, bandari, na masoko, pamoja na huduma bora za anga, utachangia kuongeza tija na kupunguza gharama za uzalishaji.

Mkoa wa Tanga una fursa nyingi za uwekezaji na biashara, ikiwa ni pamoja na kilimo cha kibiashara na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao kama mkonge, chai, kahawa, matunda, na mbogamboga; miundombinu ya bandari na huduma za logistiki za kimataifa, ikijumuisha kuendeleza Bandari ya Tanga na huduma za kuhifadhi, kusafirisha, na kushughulikia mizigo; utalii wa kimataifa na shughuli za mazingira, kupitia utalii wa hifadhi za wanyamapori, utalii wa pwani, na vivutio vya kihistoria kama Mji Mkongwe; nishati mbadala na miradi ya mafuta, hasa kupitia EACOP, uzalishaji wa umeme wa jua na upepo; na viwanda vya usindikaji wa chakula na bidhaa za maziwa, vinavyotoa ajira na kuongeza thamani ya uzalishaji wa ndani.

Changamoto zinazokabili mkoa ni pamoja na kodi, tozo, na ada zinazoathiri uzalishaji na ushindani wa viwanda vidogo na vya kati; miundombinu ya barabara na reli isiyokamilika, hasa katika maeneo ya mbali, inayoongeza gharama za usafirishaji; upatikanaji mdogo wa mtaji na huduma za kifedha kwa wajasiriamali kwa ajili ya kukuza viwanda na biashara, pamoja na upungufu wa huduma zenye viwango vya kimataifa katika maeneo ya mbali.

Mkoa wa Tanga ni lango la kiuchumi, kibiashara, na kihistoria lenye nafasi kubwa ya uwekezaji katika kilimo, utalii, bandari, nishati, na viwanda vya kuongeza thamani. Kwa mtazamo wa TNCC, kuboresha sera za uwekezaji, miundombinu, na ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali kutachochea ukuaji wa uchumi wa mkoa na kuchangia maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

# SURA YA TATU: UCHAMBUZI WA TATHMINI

## 3.1. Juhudi za Serikali katika Kuboresha Mazingira ya Biashara

Pamoja na uwepo wa changamoto mbalimbali zinazoendelea kuwakabili wafanyabiashara, Chemba inatambua na kupongeza hatua na juhudi mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara hapa nchini kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI), maarufu kama Blueprint.

Hususan, Chemba inaipongeza Serikali kwa kufanya maboresho ya mazingira ya biashara katika maeneo yafuatayo:

i. Kupunguza na kufuta ada na tozo mbalimbali zilizokuwa zikitozwa na mamlaka za udhibiti kama vile GCLA, SBT, TMDA, TBS, OSHA, na FRF, ambapo katika kipindi cha mwaka 2017/18 hadi 2022/23, jumla ya ada na tozo 374 zilifutwa. Kwa ujumla, maboresho haya yamesaidia kupunguza gharama za kuanzisha na kuendesha biashara nchini.

ii. Kufutwa na kuunganishwa kwa baadhi ya mamlaka za udhibiti kumeleta nafuu kubwa kwa jumuiya ya wafanyabiashara kwa kupunguza urasimu na muda wa kushughulikia masuala mbalimbali ya kibiashara.

iii. Kuanzishwa kwa mifumo ya kielektroniki kumesaidia kupunguza kwa kiwango kikubwa muda wa uchakataji wa vibali vya biashara, kupunguza urasimu, na kupunguza mianya ya vitendo vya rushwa. Aidha, mifumo ya kidijitali imerahisisha kwa wananchi na wafanyabiashara kuwasilisha maombi ya leseni na vibali mbalimbali kupitia majukwaa ya mtandaoni bila kulazimika kufika ofisini.

iv. Mfumo wa Government Electronic Payment Gateway (GePG) umerahisisha ulipaji wa ada na tozo kwa kutumia njia mbalimbali za malipo kama vile simu za mkononi, benki, na mawakala wa benki.

v. Kupungua kwa kiwango cha malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuhusu taasisi za udhibiti kumetokana na uboreshaji wa utoaji wa huduma katika taasisi hizo. Hata hivyo, Chemba

inaishauri Serikali kuendelea kuboresha huduma katika baadhi ya taasisi kama FFR, NEMC, na TAEC.

vi. Kuanzishwa kwa Idara za Viwanda, Biashara na Uwekezaji (DITI) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ni hatua muhimu katika kuendeleza mazingira rafiki ya biashara, pamoja na kuwezesha uanzishwaji wa vituo shirikishi (one-stop centres) katika ngazi ya halmashauri.

vii. Kufutwa na kuunganishwa kwa baadhi ya taasisi za udhibiti kumesaidia kupunguza muingiliano wa majukumu na kuboresha utendaji wa taasisi hizo. Hatua hii imeleta nafuu kwa wafanyabiashara kwa kupunguza gharama za ada na tozo pamoja na muda wa kushughulikia masuala mbalimbali ya kibiashara.

viii. Chemba inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Ofisi ya Mdhibiti wa Malalamiko ya Kodi (Tax Ombudsman Service), ambayo jukumu lake ni kupokea, kuchambua na kushughulikia malalamiko ya walipakodi yanayohusiana na huduma, taratibu, au utawala. Chemba inaiomba Serikali kuendelea kuiboresha ofisi hii ili kuongeza ufanisi na thamani yake katika kuboresha mazingira ya biashara nchini.

ix. Uanzishwaji wa madawati ya msaada kwa wafanyabiashara katika baadhi ya Wizara, kama vile Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ni hatua ya kupongezwa. Mfumo huu umeonesha ufanisi katika kushughulikia changamoto zinazowakumba wafanyabiashara katika sekta husika. Hivyo, Chemba inaishauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa mifumo kama hii katika Wizara nyingine ili kuongeza manufaa kwa biashara katika sekta mbalimbali.

TNCC inaishukuru Serikali kwa jitihada zake za kufanya maboresho ya sheria mbalimbali ili kuleta ufanisi na kuboresha mazingira ya biashara nchini. TNCC inatambua kuwa jumla ya maboresho ya sheria 55 yaliyofanyika kati ya mwaka 2019 hadi 2024 yamesaidia kwa kiasi fulani kupunguza mzigo wa gharama za kufanya biashara kwa wafanyabiashara nchini.

## 3.2. Changamoto zinazokabili Biashara na Uwekezaji

Pamoja na jitihada kubwa za Serikali kama zilivyoainishwa hapo juu, TNCC imebaini kuwa bado kuna changamoto za ujumla kama ifuatavyo:

i. Miundombinu isiyokidhi mahitaji (barabara, nishati, maji, bandari na TEHAMA): Mikoa mingi bado ina barabara zisizopitika mwaka mzima, gharama kubwa za umeme, upatikanaji mdogo wa maji kwa shughuli za uzalishaji, na huduma hafifu za intaneti, hasa katika maeneo ya vijijini. Athari kwa biashara na uwekezaji ni pamoja na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji, kupungua kwa ushindani wa bidhaa za ndani sokoni, kuchelewa kwa minyororo ya ugavi (supply chains), kukatisha tamaa wawekezaji wanaohitaji miundombinu ya uhakika, na kupunguza kasi ya maendeleo ya viwanda katika mikoa ya ndani.

ii. Upatikanaji mgumu wa mitaji na huduma za kifedha: Wafanyabiashara wengi katika mikoa, hususan MSMEs, hukosa dhamana, historia ya mikopo, na elimu ya kifedha inayohitajika kupata mikopo kutoka taasisi za fedha. Hali hii husababisha biashara kushindwa kupanuka au kuongeza uzalishaji, kukwamisha ubunifu na uwekezaji mpya, kuwafanya wajasiriamali wengi kubaki katika biashara ndogo zisizokua, na kupunguza ajira pamoja na mapato ya kodi kwa Serikali.

iii. Urasimu na mwingiliano mkubwa wa tozo, leseni, na vibali: Biashara hulazimika kushughulika na taasisi nyingi kwa ajili ya vibali, leseni, na ukaguzi wa mara kwa mara, mara nyingine kwa taratibu zisizoeleweka vizuri kwa wafanyabiashara. Hali hii huongeza gharama za kufanya biashara (cost of compliance), hupoteza muda wa uzalishaji, huchochea mazingira ya rushwa, huwazuia wawekezaji wadogo na wa kati kuingia rasmi kwenye mfumo, na hupunguza mvuto wa mikoa kwa wawekezaji wapya.

iv. Ukosefu wa masoko ya uhakika na mnyororo hafifu wa thamani: Mikoa mingi huzalisha mazao au bidhaa lakini hukosa miundombinu ya kuchakata, kuhifadhi, na kuunganisha wazalishaji na masoko ya ndani na nje ya nchi. Hali hii husababisha bidhaa kuuzwa kwa bei ya chini kwa walanguzi, pamoja na upotevu mkubwa wa mazao baada ya mavuno (post-harvest losses).

v. Uhaba wa ujuzi na nguvu kazi stadi: Sekta nyingi katika mikoa hukosa mafundi stadi, wataalamu wa teknolojia, usimamizi wa biashara, na uendeshaji wa mitambo ya kisasa. Hali hii husababisha uzalishaji kuwa wa kiwango cha chini, kampuni kulazimika kuleta wataalamu kutoka mikoa mingine au nje ya nchi, na wawekezaji wakubwa kusita kuwekeza nje ya miji mikubwa.

vi. Kutotabirika kwa sera na mabadiliko ya mara kwa mara ya kanuni: Baadhi ya biashara hukumbwa na mabadiliko ya kodi, tozo, au kanuni bila muda wa kutosha wa maandalizi. Hali hii huongeza hatari ya uwekezaji (investment risk), husababisha wawekezaji kuchelewesha au kufuta miradi, kuifanya biashara kushindwa kupanga kwa muda mrefu, na kupunguza imani ya sekta binafsi katika mazingira ya biashara.

vii. Changamoto za ardhi na migogoro ya umiliki: Upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji huchukua muda mrefu, huku kukiwa na migogoro ya mipaka, fidia, na matumizi ya ardhi kati ya jamii na wawekezaji. Hali hii husababisha miradi mikubwa kuchelewa kuanza, kuongezeka kwa gharama za uwekezaji, na baadhi ya wawekezaji kuhamishia miradi yao katika nchi au mikoa mingine.

viii. Uelewa mdogo wa fursa za uwekezaji za kimkoa: Mikoa mingi haina hifadhidata wazi za fursa za uwekezaji, tafiti za masoko, au taarifa zilizoboreshwa za rasilimali zilizopo. Hali hii husababisha wawekezaji kukosa taarifa muhimu za kufanya maamuzi, fursa nyingi kubaki hazijatumika, uwekezaji kujikita zaidi mijini kuliko mikoani, na ukuaji wa uchumi kuwa usio na uwiano.

ix. Mabadiliko ya tabianchi na hatari za mazingira: Mikoa inayotegemea kilimo, uvuvi, na utalii huathirika na ukame, mafuriko, au uharibifu wa mazingira. Mabadiliko haya ya tabianchi husababisha uzalishaji kutotabirika, hasara kwa wawekezaji wa kilimo na utalii, kuongezeka kwa gharama za bima na ulinzi wa miundombinu, na kuwafanya wawekezaji kuona sekta hizi kuwa na hatari kubwa.

x. Mtazamo hasi na kutokuaminiana kati ya sekta binafsi na taasisi za umma: Baadhi ya wafanyabiashara huziona taasisi za udhibiti kama vyombo vya adhabu badala ya washirika wa maendeleo. Kutokuaminiana huku husababisha biashara kuepuka kuwa rasmi, kupungua kwa ushirikiano katika ukusanyaji wa mapato, kuongezeka kwa migogoro kati ya wafanyabiashara na mamlaka, na mazingira ya biashara kukosa utulivu.

## 3.3. Fursa za Biashara na Uwekezaji

Uchambuzi wa TNCC unaonesha kuwa Tanzania ina fursa pana zinazotokana na rasilimali asilia, jiografia yake ya kimkakati, soko la kikanda, na idadi kubwa ya watu wenye uwezo wa kushiriki katika uzalishaji. Iwapo fursa hizi zitaunganishwa na maboresho ya miundombinu, sera thabiti, na ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, zinaweza kuifanya Tanzania kuwa kitovu kikuu cha biashara na uwekezaji barani Afrika.

Fursa hizo ni pamoja na:

i. Uwekezaji katika kilimo cha kibiashara na uongezaji thamani: Tanzania ina ardhi kubwa yenye rutuba, hali ya hewa inayoruhusu uzalishaji wa mazao mbalimbali mwaka mzima, na nguvu kazi ya kutosha vijijini. Fursa kubwa ipo si tu katika uzalishaji wa mazao, bali zaidi katika kuongeza thamani kupitia usindikaji, ufungashaji, na usambazaji wa kisasa. Maeneo ya fursa ndani ya sekta hii ni pamoja na viwanda vya kusindika mazao (nafaka, matunda, mboga, mafuta ya kula, kahawa, chai, viungo); uwekezaji katika maghala, cold storage, na mifumo ya kuhifadhi mazao; pamoja na kilimo cha mkataba (contract farming) kinachounganisha wakulima na viwanda. Uwekezaji huu utapunguza upotevu wa mazao, kuongeza kipato cha wakulima, kuongeza ajira za viwandani, na kuongeza mauzo ya nje ya bidhaa zilizoongezwa thamani badala ya kuuza malighafi ghafi.

ii. Uwekezaji katika viwanda vya kati na vidogo (agro-processing na manufacturing): Ukuaji wa soko la ndani na kikanda unatoa fursa kubwa kwa uwekezaji katika viwanda vya bidhaa za matumizi ya kila siku kama vyakula vilivyosindikwa, vinywaji, vifaa vya ujenzi, bidhaa za plastiki, nguo, na bidhaa za ngozi. Maeneo mahsusi ni pamoja na viwanda vinavyotumia malighafi za ndani; uzalishaji wa bidhaa

mbadala wa zile zinazoagizwa kutoka nje (import substitution); pamoja na maendeleo ya maeneo maalum ya viwanda (industrial parks na SEZs). Uwekezaji huu utaongeza ajira, kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje, kuimarisha sarafu ya taifa, na kuifanya Tanzania kuwa kituo cha uzalishaji kwa soko la Afrika Mashariki na SADC.

iii. Biashara ya mipakani na masoko ya kikanda: Tanzania imezungukwa na nchi nyingi zisizo na bandari na ni mwanachama wa EAC, SADC, na AfCFTA. Hali hii inaleta fursa kubwa ya kuwa kitovu cha biashara na usambazaji wa bidhaa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika. Fursa zilizopo ni pamoja na uwekezaji katika maghala ya kisasa ya kuhifadhia bidhaa za usafirishaji; huduma za usafirishaji (logistics, trucking, clearing and forwarding); pamoja na uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya soko la kikanda. Biashara ya mipakani itapunguza utegemezi wa soko la ndani pekee na kupanua wigo wa biashara za Tanzania katika soko la kikanda lenye zaidi ya watu milioni 400.

iv. Uwekezaji katika sekta ya madini na uongezaji thamani: Mbali na uchimbaji, fursa kubwa ipo katika uongezaji thamani wa madini hapa nchini kupitia usafishaji, uchakataji, na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na madini. Maeneo ya fursa ni pamoja na vituo vya kusafisha madini (mineral processing plants); uzalishaji wa vito vya thamani na bidhaa zitokanazo na madini; pamoja na huduma saidizi za migodi kama vifaa, usafirishaji, usalama, na chakula. Uwekezaji katika sekta ya madini utaongeza mapato ya ndani, kuimarisha ajira za ujuzi wa kati na juu, na kuifanya Tanzania kunufaika zaidi na rasilimali zake badala ya kuuza malighafi ghafi.

v. Utalii wa aina mbalimbali (diversified tourism): Mbali na utalii wa wanyamapori, kuna fursa kubwa katika utalii wa fukwe na bahari (blue tourism); utalii wa kiutamaduni na kihistoria; pamoja na utalii wa mikutano na maonesho (MICE). Fursa za uwekezaji katika sekta hii ni pamoja na hoteli za kati na ndogo katika mikoa; huduma za utalii wa jamii (community tourism); pamoja na miundombinu ya burudani na michezo. Uwekezaji huu utaongeza mapato ya utalii, kupanua wigo wa vivutio vya nchi, na kuongeza ajira katika sekta ya huduma.

vi. Uchumi wa buluu (blue economy): Kutokana na uwepo wa ukanda mrefu wa pwani na maziwa makubwa, Tanzania ina fursa katika uvuvi wa kisasa na usindikaji wa samaki; ufugaji wa samaki (aquaculture); maendeleo ya bandari ndogo na huduma za usafiri wa majini; pamoja na uzalishaji wa nishati ya upepo na mawimbi ya bahari. Uwekezaji katika uchumi wa buluu utaongeza ajira kwa jamii za pwani, kuongeza mauzo ya bidhaa za baharini nje ya nchi, na kupanua wigo wa uchumi zaidi ya kilimo cha nchi kavu.

vii. Nishati na nishati mbadala: Ukuaji wa viwanda na miji unaongeza mahitaji ya nishati, hali inayotoa fursa kwa uwekezaji katika uzalishaji wa nishati jadidifu kama jua, upepo, na biomasi; maendeleo ya mini-grids kwa maeneo ya vijijini; pamoja na huduma na vifaa vya nishati safi kwa viwanda na kaya. Uwekezaji huu utasaidia kupunguza gharama za uzalishaji, kuwezesha uanzishwaji wa viwanda katika maeneo mapya, na kuongeza uwekezaji katika maeneo ya vijijini.

viii. Huduma za kifedha na kidigitali: Ukuaji wa biashara unahitaji huduma za kifedha zilizo karibu na wananchi. Fursa zilizopo ni pamoja na huduma za kifedha kwa MSMEs (microfinance, leasing, insurance); suluhisho za malipo ya kidigitali; pamoja na mifumo ya biashara mtandao (e-commerce). Uwekezaji katika eneo hili utaongeza ujumuishaji wa kifedha, kurahisisha biashara kufanyika kwa uwazi na kwa kasi, na kuongeza mapato ya Serikali kupitia mifumo rasmi.

ix. Miundombinu ya biashara na maghala: Kadri uzalishaji unavyoongezeka, mahitaji ya masoko ya kisasa, maghala ya kuhifadhi bidhaa, vituo vya ukusanyaji mazao, na vituo vya usafirishaji (logistics hubs) yanaongezeka. Uwekezaji katika eneo hili utapunguza upotevu wa mazao, kuongeza ufanisi wa usambazaji, na kuvutia wawekezaji wanaohitaji minyororo ya ugavi iliyoimarika.

x. Maendeleo ya ujuzi na huduma za kitaalamu: Ukuaji wa sekta binafsi unaongeza uhitaji wa mafunzo ya ufundi stadi, huduma za ushauri wa biashara, pamoja na teknolojia na ubunifu (innovation hubs). Uwekezaji katika eneo hili utaongeza tija, kuwezesha vijana kujiajiri, na kuwafanya wawekezaji kupata nguvu kazi yenye ujuzi ndani ya nchi.

# SURA YA NNE: MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

Sura hii imejikita katika kutoa mapendekezo yanayotokana na uchambuzi wa fursa na changamoto zilizoainishwa kupitia tathmini ya TNCC kuhusu hali ya biashara na uwekezaji katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Aidha, mapendekezo haya yanalenga kuunganisha maoni na hoja zilizotokana na uchambuzi wa kina wa mazingira ya biashara, ili kutoa mwongozo wa hatua madhubuti za kuboresha mazingira hayo. Mapendekezo haya yamegawanyika katika sehemu kuu tatu, ambazo ni: mapendekezo ya kiutendaji au kiutawala, mapendekezo kwa Serikali za Mitaa, pamoja na mapendekezo ya kisera.

## 4.1. Mapendekezo ya Kiutendaji au Kiutawala

Mapendekezo ya kiutendaji ni hatua mahsusi zinazopendekezwa kwa lengo la kuboresha utendaji na kutatua changamoto zilizobainishwa katika sekta mbalimbali. Sura hii inaeleza kwa ufupi sababu za msingi zinazohitaji maboresho, pamoja na madhumuni ya mapendekezo haya katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Aidha, sehemu hii inaangazia changamoto mbalimbali na kueleza namna ambavyo mapendekezo yaliyotolewa yanalenga kuzitatua kwa njia endelevu, yenye tija na inayowanufaisha wadau wote, wakiwemo Serikali, sekta binafsi na jamii kwa ujumla. Vilevile, kuna umuhimu wa kutumia mbinu za kiutendaji zinazozingatia rasilimali zilizopo, malengo ya muda mfupi na muda mrefu, pamoja na athari zake kwa uchumi na jamii. Mapendekezo haya yanatokana na uchambuzi wa kina wa takwimu, ushahidi wa kitaalamu, na maoni ya wadau mbalimbali, na yanalenga kuleta matokeo chanya katika utekelezaji wa shughuli za kila siku. Kwa ujumla, jumla ya mapendekezo ya kiutendaji thelathini na moja (31) yameainishwa, yakitokana na changamoto mbalimbali zilizobainishwa katika tathmini hii.

i. Changamoto za wavuvi katika Ziwa Tanganyika: Licha ya jitihada zilizofanyika katika kutatua changamoto za wavuvi katika Ziwa Tanganyika, bado wanakabiliwa na mzigo wa tozo zinazotozwa na taasisi ya TASAC. TNCC inapendekeza TASAC kutoa elimu ya kutosha kwa wavuvi kuhusu majukumu yake, mfumo wa utozaji wa tozo, pamoja na uhalali wake wa kisheria, ili kuongeza uelewa, uwazi na kukubalika kwa tozo hizo (rejea kipengele ‘G’).

ii. Upungufu wa mafuta ya kula ya alizeti: Changamoto ya upungufu wa mafuta ya kula ya alizeti inachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa mbegu bora za alizeti. Katika kukabiliana na changamoto hii, TNCC inapendekeza yafuatayo:

a. Serikali ihamasishe uzalishaji wa mbegu bora za alizeti kwa kushirikiana na wakulima wazawa, ili kuongeza uzalishaji wa malighafi kwa viwanda vya mafuta ya kula.
b. Serikali iweke motisha (incentives) kwa wazalishaji wa mbegu bora, ikiwa ni pamoja na ruzuku, mikopo nafuu na upatikanaji wa pembejeo, ili kuimarisha uzalishaji na kuchangia usalama wa chakula nchini (National Food Security).
c. Serikali iongeze uwekezaji katika ajira na uwezo wa maafisa ugani ili kuwajengea wakulima uwezo wa kutumia mbinu bora za kilimo na kuongeza tija ya uzalishaji.
d. Serikali ishirikiane na wadau wa sekta binafsi (kama TCCIA, TAHA, na Baraza la Kilimo) katika kutambua, kuratibu na kuimarisha mchango wa maafisa ugani binafsi katika ngazi za vijiji, kata na wilaya.

iii. Changamoto ya uelewa mdogo wa sera kwa wananchi: Uelewa mdogo wa sera kwa wananchi ni changamoto inayokwamisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo, kupunguza ushiriki wa wananchi, na kudhoofisha ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi. TNCC inapendekeza Serikali kuimarisha utoaji wa elimu ya sera kwa wananchi kupitia kampeni za uhamasishaji, majukwaa ya wadau na matumizi ya vyombo vya habari, kwa kushirikiana na sekta binafsi. Mfano wa sera zinazohitaji uelewa mpana ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III).

iv. Tatizo la masoko ya mazao: Changamoto ya uuzaji wa mazao ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakumba wakulima katika karibu mikoa yote ya Tanzania. Changamoto hii inajumuisha ukosefu wa masoko ya uhakika, bei zisizo tabirika, changamoto katika mfumo wa stakabadhi ghalani, miundombinu duni, pamoja na upungufu wa teknolojia ya kisasa na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao. Licha ya jitihada mbalimbali zilizofanyika, bado kuna haja ya Serikali, TNCC na sekta binafsi kuimarisha juhudi za pamoja za kuhamasisha

uwekezaji katika teknolojia za usindikaji na uchakataji wa mazao ya kilimo, hususan matunda, mbogamboga, viazi na mazao mengine yenye thamani ya kibiashara. Uwekezaji huu utasaidia kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno, kuongeza thamani ya bidhaa, na kuboresha kipato cha wakulima pamoja na ushindani wa bidhaa katika masoko ya ndani na nje.

v. Uwepo wa bandari bubu: Serikali inapoteza mapato makubwa kutokana na uwepo wa bandari zisizo rasmi (bandari bubu), ambapo bidhaa zinazoingia au kutoka hazilipii kodi na ushuru unaostahili. Hali hii inaathiri ukusanyaji wa mapato ya Serikali na uwezo wake wa kutekeleza miradi ya maendeleo. Katika kukabiliana na changamoto hii, TNCC inapendekeza yafuatayo:

   a. Serikali iimarishe udhibiti wa mipaka ya majini kwa kufanya doria za mara kwa mara, kutumia teknolojia za ufuatiliaji, na kuongeza ushirikiano kati ya taasisi za usalama na mamlaka za bandari ili kudhibiti na kutokomeza bandari bubu nchini.
   b. Serikali ipitie na kuoanisha mfumo wa kodi na ushuru kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, ili kupunguza mianya ya ukwepaji wa kodi na kuimarisha ushindani wa haki katika biashara.

vi. Changamoto ya wavuvi kutoshirikishwa kwenye mikopo nafuu: Katika utekelezaji wa mipango ya mikopo nafuu kwa wavuvi, bado kuna upungufu wa ushirikishwaji wa walengwa katika kubaini mahitaji yao halisi. TNCC inapendekeza Serikali kuhakikisha ushirikishwaji wa wavuvi katika kubuni na kutekeleza programu za mikopo nafuu, ili fedha zinazotolewa ziendane na mahitaji halisi ya sekta ya uvuvi na kuongeza ufanisi wa matumizi yake. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inashauriwa kuimarisha utoaji wa elimu kwa wavuvi kuhusu mbinu bora na salama za uvuvi, ikiwa ni pamoja na kuzingatia marufuku ya matumizi ya jenereta katika shughuli za uvuvi na kuhamasisha matumizi ya vifaa rafiki kwa mazingira. Hatua hii itachangia uhifadhi wa mazingira na kulinda uhai wa viumbe vya majini.

vii. Hali duni ya mazingira ya kilimo na biashara ya korosho: Kilimo na biashara ya korosho vinakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa teknolojia za kisasa za uchakataji na uhifadhi,

upatikanaji mdogo wa mitaji na uwekezaji, pamoja na changamoto za masoko. Katika kukabiliana na changamoto hizi, TNCC inapendekeza yafuatayo:

a. Serikali iboreshe mazingira ya biashara ya korosho kwa kuimarisha mifumo ya masoko, hususan kwa kuhakikisha matumizi sahihi na yenye uwazi ya mfumo wa Tanzania Mercantile Exchange (TMX) katika minada ya korosho, ili kulinda maslahi ya wakulima na wafanyabiashara.

b. Bodi ya Korosho iimarishwe katika kutoa mafunzo kwa wanachama wa vyama vya ushirika kuhusu uendeshaji wa shughuli za korosho, upatikanaji wa pembejeo bora, pamoja na mbinu bora za uzalishaji na masoko.

viii. Upungufu wa elimu na ujuzi kwa watendaji wa TRA: Upungufu wa elimu na ujuzi kwa baadhi ya watendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ni changamoto inayoweza kuathiri ubora wa huduma, ufanisi wa ukusanyaji wa kodi, na uhusiano kati ya mamlaka na walipakodi. Katika kukabiliana na changamoto hii, TNCC inapendekeza yafuatayo:

a. Watendaji wa TRA na mamlaka nyingine zinazohudumia wafanyabiashara wapewe mafunzo ya mara kwa mara kuhusu huduma kwa wateja, ili kuboresha mawasiliano, uwazi na kuridhika kwa walipakodi.

b. Serikali iendelee kuimarisha mahusiano kati ya taasisi zake na wafanyabiashara kwa kuanzisha majukwaa ya mazungumzo, mifumo ya kushughulikia malalamiko kwa ufanisi, na kujenga mazingira ya kuaminiana yatakayochochea hiari ya ulipaji kodi.

ix. Changamoto ya HS Code ya mvinyo (2204): Changamoto zinazohusiana na HS Code ya mvinyo (2204) zinajumuisha masuala ya kodi, ushuru, biashara na ufuatiliaji wa bidhaa, hali inayoweza kuathiri ushindani wa wazalishaji wa ndani, uwazi wa soko, pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Katika kukabiliana na changamoto hii, TNCC inapendekeza yafuatayo:

a. Wizara ya Viwanda na Biashara iwasilishe pendekezo la kutenganisha HS Code ya mvinyo (2204) ili kubainisha tofauti

kati ya mvinyo ghafi na mvinyo uliosindikwa, kwa lengo la kuweka mfumo sahihi wa kodi na ushuru unaoendana na thamani ya bidhaa.

b. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ihamasishe na kuwekeza katika uzalishaji wa vifungashio vya ndani kwa bidhaa za mvinyo na bidhaa nyingine, ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza ushindani wa bidhaa za ndani.

c. Serikali kwa kushirikiana na taasisi za sekta binafsi iendelee kuhamasisha wawekezaji wa ndani kusajili biashara zao kupitia TISEZA, ili waweze kunufaika na vivutio vya uwekezaji vinavyotolewa na mamlaka hiyo.

x. Malipo ya wazabuni kwa wakati: Changamoto ya ucheleweshaji wa malipo kwa wazabuni inaathiri mtiririko wa fedha, uwezo wa utekelezaji wa miradi, uwajibikaji, pamoja na ubora wa huduma zinazotolewa. Hali hii pia hupunguza imani ya sekta binafsi katika kushiriki kikamilifu katika zabuni za Serikali. Katika kukabiliana na changamoto hii, TNCC inapendekeza yafuatayo:

a. Serikali ihakikishe malipo kwa wazabuni yanafanyika kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya mikataba ya zabuni. Aidha, pale ambapo kunatokea ucheleweshaji wa malipo, wazabuni wa ndani waruhusiwe kudai riba (interest) kwa mujibu wa sheria na vipengele vya mikataba husika.

b. Serikali, hususan kupitia wakurugenzi watendaji wa mamlaka mbalimbali, izingatie kikamilifu taratibu na sheria za manunuzi ya umma katika mchakato wa kupata huduma kutoka kwa wazabuni, ili kuhakikisha uwazi, ushindani wa haki, na ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma.

xi. Changamoto ya kilimo cha umwagiliaji: Kilimo cha umwagiliaji kinakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazodhoofisha juhudi za wakulima katika kutumia rasilimali za maji ili kuongeza tija na uhakika wa mavuno. Changamoto hizi ni pamoja na upungufu wa miundombinu ya umwagiliaji, uwekezaji mdogo katika miradi ya maji, na ukosefu wa teknolojia za kisasa za umwagiliaji. Katika kukabiliana na changamoto hizi, TNCC inapendekeza Serikali kuendelea

kuwekeza katika miradi ya kilimo cha umwagiliaji, hususan ujenzi wa visima, mabwawa na mifumo ya kisasa ya usambazaji wa maji katika maeneo ya kimkakati ya uzalishaji wa mazao. Maeneo yenye uzalishaji mkubwa kama mashamba ya vitunguu mkoani Singida yanapaswa kupewa kipaumbele ili kuongeza uzalishaji, kupunguza utegemezi wa mvua, na kuimarisha usalama wa chakula nchini.

xii. Ushuru na tozo mbalimbali: Taasisi mbalimbali za Serikali hutoza ushuru, tozo na ada kwa ajili ya utoaji wa huduma, vyeti na leseni za uendeshaji wa shughuli za biashara. Hali hii, hususan pale inapokuwa na wingi na muingiliano wa tozo, huongeza gharama za uendeshaji wa biashara na kuathiri mazingira ya uwekezaji kwa ujumla. Miongoni mwa taasisi zinazohusika ni pamoja na OSHA, Fire, NEMC, TBS, TAEC, GCLA, WMA, LGAs na TFS. Katika kukabiliana na changamoto hii, TNCC inapendekeza yafuatayo:

a. Serikali ifanye mapitio ya kina ya mfumo wa utozaji wa tozo na ada ili kupunguza mzigo kwa wafanyabiashara, hususan kwa kuepuka ulipaji wa ada nyingi kwa wakati mmoja (lump sum). Aidha, upangaji wa muda wa kulipia leseni na tozo uzingatie mzunguko wa biashara na uwezo wa walipaji.

b. Serikali ianzishe na kuimarisha uratibu wa ukaguzi kwa kuhakikisha mamlaka mbalimbali za udhibiti zinafanya ukaguzi wa pamoja (joint inspections), ili kupunguza urasimu, gharama na usumbufu kwa wafanyabiashara.

xiii. Mifumo ya TRA kutokuwa madhubuti: Changamoto ya mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokuwa madhubuti inahusu udhaifu katika mifumo ya ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa kodi na utoaji wa huduma kwa walipakodi. Hali hii huathiri ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kusababisha changamoto kwa wafanyabiashara na walipakodi kwa ujumla. Katika kukabiliana na changamoto hii, TNCC inapendekeza yafuatayo:

a. Serikali kupitia TRA iboreshe mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuhifadhi na kusimamia kanzidata za wafanyabiashara kwa uwazi, usahihi na upatikanaji wa taarifa kwa pande zote; TRA na wafanyabiashara.

b. Serikali kupitia TRA iendelee kuimarisha utoaji wa elimu ya mlipakodi kwa wafanyabiashara, hususan kuhusu vifungu vya sheria za kodi, ili kuongeza uelewa na hiari ya ulipaji kodi.

c. Serikali itekeleze kwa vitendo maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhusu kutoendelea kudai madeni ya kodi yenye zaidi ya miaka mitatu (3), kwa lengo la kupunguza mzigo kwa wafanyabiashara na kuimarisha mazingira ya biashara.

d. Ili kuimarisha utekelezaji wa agizo hilo, Serikali itoe mwongozo rasmi kupitia waraka au Tangazo la Serikali (Government Notice – GN), ili kulipa uzito wa kisheria na kuhakikisha utekelezaji wake unaeleweka kwa wadau wote.

e. Serikali kupitia TRA, kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi (ikiwemo TNCC), iongeze juhudi za utoaji wa elimu ya mlipakodi katika maeneo yenye uhitaji mkubwa kama Mkoa wa Simiyu, ili kuboresha uelewa wa kodi na kuongeza ushiriki wa wafanyabiashara katika mfumo rasmi.

f. Pamoja na Serikali kuunda Tume Maalumu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kupitia mfumo wa kodi nchini, inapendekezwa kuwa mchakato huo uwe shirikishi kwa kuhakikisha tume inakusanya maoni kutoka ngazi zote (wilaya, mikoa na kitaifa) kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi, ili kupata mapendekezo jumuishi ya kuboresha mfumo wa kodi.

g. TRA inashauriwa kuharakisha uundwaji wa mfumo wa utoaji wa risiti kwa kila muagizaji wa mizigo inayoingia nchini, badala ya utaratibu wa sasa ambapo consolidator ndiye anayepokea risiti ya jumla. Hatua hii itaongeza uwazi na ufuatiliaji wa kodi.

h. Aidha, TRA inapaswa kuimarisha utekelezaji wa utaratibu wa utenganishaji wa mizigo (deconsolidation) ili kuhakikisha kila mfanyabiashara anapata risiti halali ya kielektroniki (EFD receipt) kwa manunuzi yake.

i. Serikali inashauriwa kupitia upya na kuboresha mfumo wa usajili wa VAT ili kuhakikisha biashara nyingi zaidi, hususan katika maeneo yenye shughuli kubwa za kibiashara kama Soko la

Kariakoo, zinaingizwa katika wigo wa kodi kwa kuzingatia vigezo na uwezo wa biashara husika.

j. Miundombinu ya barabara na huduma za msingi katika eneo la Soko la Kariakoo iboreshwe ili kurahisisha upatikanaji wa soko hilo kwa wateja, hususan wa kimataifa, na hivyo kuongeza shughuli za biashara na ukusanyaji wa mapato.

k. Serikali inashauriwa kuoanisha (harmonize) mfumo wa VAT kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, ili kupunguza mianya ya ukwepaji wa kodi na kuimarisha ushindani wa haki katika biashara.

l. Serikali inapaswa kuoanisha sera na mazingira ya kodi katika maeneo ya mipakani ili kuchochea urasimishaji wa biashara na kupunguza biashara zisizo rasmi.

m. TRA inashauriwa kutekeleza kifungu cha 67 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi kwa kuzingatia kikamilifu taratibu za kisheria na kuhakikisha haki na uwazi katika utekelezaji wake kwa walipakodi.

xiv. Changamoto ya miundombinu kwenye mwalo wa Kibirizi: Changamoto hizi zinaathiri moja kwa moja tija na mapato ya wavuvi, na kwa kiasi kikubwa huathiri uchumi wa eneo hilo. Kutokuwepo kwa miundombinu ya kutosha pia kunaweza kupunguza usalama na ubora wa mazao ya uvuvi, na hivyo kuathiri afya ya walaji na thamani ya soko. Serikali kupitia TPA inashauriwa kuharakisha kuboresha miundombinu kwenye mwalo wa Kibirizi (na masoko ya mialo mingine nchini) ili kuboresha shughuli za uvuvi kwenye mwalo huo.

xv. Mfumo wa utoaji leseni za uvuvi: Kuna matatizo na vikwazo katika mchakato wa kupata leseni za uvuvi zinazotolewa kwa wavuvi na wafanyabiashara wa sekta ya uvuvi ili kuwapa kibali rasmi cha kufanya shughuli zao. Wizara ya Mifugo na Uvuvi inashauriwa kuboresha mfumo wa utoaji leseni za uvuvi ili ziwe za mzunguko wa mwaka mzima tangu mwombaji alivyokata, tofauti na utaratibu wa sasa unaozingatia kalenda ya mwaka.

xvi. Miundombinu kwenye hifadhi Southern Circuit: Changamoto hizi zinaathiri moja kwa moja sekta ya utalii na ukuaji wa uchumi katika mikoa ya Kusini. Kwa upande mmoja, upungufu wa miundombinu unazuia utalii wa kimataifa na wa ndani, huku ikizua changamoto kwa wawekezaji wa kitalii ambao wanataka kujenga au kuboresha huduma.

a. Serikali kupitia Wizara ya Utalii iendelee kuwekeza kwenye hifadhi zilizopo Southern Circuit kwa kuweka miundombinu kama vile viwanja vya ndege, barabara n.k.
b. Kuongeza wanyama kama faru pamoja na kutangaza vivutio vilivyopo ili kufikia lengo la watalii milioni 5 ifikapo mwaka 2025 kama lilivyo lengo la Serikali katika sekta ya utalii.

xvii. Ufinyu wa viwanda vya vifungashio: Changamoto hizi zinaathiri moja kwa moja uchumi wa nchi, kwani viwanda vya vifungashio ni muhimu katika kuhakikisha bidhaa zinazalishwa na kusambazwa kwa ufanisi. Ufinyu wa viwanda vya vifungashio pia unaweza kupunguza ushindani wa bidhaa za ndani kwenye masoko ya kimataifa, kuathiri biashara za ndani, na kuongeza gharama za bidhaa. Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa kushirikiana na sekta binafsi, ihamasishe uwekezaji kwenye viwanda vya vifungashio katika mikoa mbalimbali nchini.

xviii. Ushuru wa umeme na maji kwa wawekezaji: Changamoto ya ushuru wa umeme na maji kwa wawekezaji inahusu mzigo mkubwa wa gharama ambazo wawekezaji wanakutana nazo kutokana na bei za juu za huduma za umeme na maji.

a. Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Wizara ya Maji ifanye mapitio ya ushuru hizo za umeme na maji ili kuleta ahueni ya gharama za uwekezaji.

b. Serikali iongeze ubora wa huduma za umeme na maji ili kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa upotevu wa umeme na maji viwandani.

c. Serikali ihamasishe na kuendelea kuwekeza kwenye matumizi ya nishati mbadala kama gesi asilia.

d. Serikali iweke mazingira mazuri ya uwekezaji wa gesi asilia (incentives) ili kuongeza tija ya uwekezaji wa sekta hii.

e. Serikali ielimishe wamiliki wa vituo vya mafuta na ihamasishe vituo vya mafuta vilivyopo viwekeze kwenye upatikanaji wa nishati ya gesi vituoni humo.

xix. Upungufu wa elimu ya uwekezaji: Changamoto ya elimu ya uwekezaji inahusu ukosefu wa maarifa, ujuzi, na uelewa wa kina kuhusu masuala ya uwekezaji, jinsi ya kuanzisha na kusimamia miradi ya uwekezaji, na hatari zinazohusiana na uwekezaji.

a. Serikali kupitia TISEZA itoe elimu kwa wananchi juu ya taratibu za kupata fursa za uwekezaji.

b. Mkoa wa Ruvuma (na mingine) uongeze jitahada za kujitangaza nchini na nje ya nchi kuhusiana na fursa zipatikanazo mkoani humo.

c. Wilaya ya Tanganyika ina maeneo makubwa ya uwekezaji wa kilimo.

d. Baadhi ya wawekezaji wamehodhi maeneo makubwa ambayo hayajafanyiwa uwekezaji kama ilivyotarajiwa. Yatengwe maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya kilimo cha mkakati (commercial farming) ili kupata wawekezaji wakubwa kwenye kilimo.

xx. Changamoto ya matumizi bora ya ardhi

a. Serikali inashauriwa kuweka matumizi bora ya ardhi kwa makundi hayo ya kilimo, ufugaji na utunzaji wanyamapori.

b. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi inashauriwa kuwa na mpango maalum wa matumizi ya ardhi, yaani kuweka mfumo wa upanuzi wima (vertical expansion) kuliko upanuzi wa usawa (horizontal expansion). Tuweke mpango ambao unatoa nafasi ya maendeleo ya baadaye kwani kwa sasa wananchi wanatawanyika mpaka tunakosa maeneo ya kufanya shughuli za maendeleo kama kilimo, ufugaji, madini, miundombinu n.k.

xxi. Upungufu wa utekelezaji wa sheria katika ukusanyaji wa madeni: Changamoto ya kutotumia sheria katika ukusanyaji wa madeni inahusu hali ambapo sheria zinazohusiana na ukusanyaji wa madeni, hasa madeni ya kodi, mikopo, au malipo ya huduma, hazitekelezwi kikamilifu au zimetumika vibaya.

Taasisi za serikali zinashauriwa kutumia taratibu na sheria zilizopo katika ukusanyaji wa madeni kwa wadau wake, ikiwemo kuwasilisha kesi mahakamani badala ya kutumia taratibu zilizo nje ya sheria. Kwa kuwa sekta binafsi ni injini ya ukuaji wa uchumi, ni muhimu serikali kuilinda na kuiendeleza kwa nguvu zote ili kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

xxii. Kulegalega kwa utengenezaji wa sheria na sera ya maendeleo ya sekta binafsi: Tatizo la kucheleweshwa, kutozingatia haraka, au kutokuwa na ufanisi katika kuunda sheria, sera, na mipango inayohusu maendeleo ya sekta binafsi inaweza kuwavunja moyo wawekezaji wa ndani na nje, na hivyo kupunguza maendeleo ya sekta binafsi.

a. Serikali inashauriwa kuharakisha mchakato wa kutengeneza sheria na sera ya maendeleo ya sekta binafsi itakayosaidia sekta binafsi kujiratibu yenyewe, kuilinda na kuiendeleza sekta binafsi sambamba na kuridhia utaratibu wa "universal membership", ambapo kila mfanyabiashara atakuwa mwanachama wa TNCC. Utaratibu huu utaondoa wanufaika wa matokeo ya utetezi bila kulipia huduma hizo 'free riders'.

b. Serikali inashauriwa kuweka utaratibu unaofanyika Zanzibar wa kuifanya ZNCC kuwa chombo pekee cha sekta binafsi, ufanyike pia Tanzania Bara kuifanya TNCC iwe chombo pekee cha sekta binafsi.

c. Serikali inashauriwa kuona namna ya kuongeza ushirikishwaji wa sekta binafsi katika sehemu tofauti za maendeleo kwani mchango wake ni mkubwa sana.

xxiii. Changamoto za miundombinu ya Bandari ya Tanga: Hali ya miundombinu iliyopo katika bandari ya Tanga kutokidhi mahitaji ya kisasa ya usafirishaji wa mizigo na abiria. Bandari ya Tanga ni moja ya

bandari kuu nchini Tanzania, lakini inakutana na changamoto kadhaa ambazo zinazuia ufanisi wake.

a. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iendelee kuboresha miundombinu ya bandari ya Tanga ili kukidhi viwango vya fursa za biashara.

b. Itengwe maeneo maalumu ya kuhifadhia mizigo hatarishi.

xxiv. Viwanda vingi mkoani Tanga kutokufanya kazi: Kuzorota au kufungwa kwa viwanda vingi katika mkoa huo, jambo linaloathiri uchumi na ajira katika eneo hilo. Tanga ni mkoa muhimu kibiashara na kiuchumi, lakini viwanda vingi vilivyokuwa vikiendesha shughuli za uzalishaji vimekumbwa na changamoto mbalimbali zinazozuia ukuaji na ufanisi wao. Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara ifikirie kufufua viwanda mkoani Tanga kama Tip Soap Industries Ltd/Shellcrafts Ltd, Unique Steel Rolling Mills Ltd, Pembe Flour Mills Ltd na Afritex Mills Ltd ili kuongeza masoko ya uhakika ya wakulima na wafugaji.

xxv. Udhaifu wa kufuatilia na kutekeleza maazimio yatokanayo na Baraza la Biashara: Changamoto ya kufuatilia na kutekeleza maazimio yatokanayo na Baraza la Biashara inahusiana na ugumu na upungufu wa ufanisi katika kuhakikisha kuwa maazimio na mapendekezo yaliyotolewa na Baraza la Biashara yanafanyiwa kazi na utekelezaji wake unakuwa na matokeo chanya kwa sekta ya biashara.

a. Serikali inashauriwa kufuatilia na kutekeleza maazimio yatokanayo na Baraza la Biashara.

b. Serikali itengeneze na kuweka wazi kalenda za mabaraza ya biashara ya mikoa na wilaya ili kuongeza ufanisi wa mabaraza hayo.

c. Serikali inashauriwa kurudisha mwongozo wa kwanza wa mabaraza ya biashara.

xxvi. Changamoto ya uchafu wa bahari na maziwa: Changamoto ya uchafu wa bahari na maziwa nchini Tanzania inahusiana na tatizo la uchafuzi wa vyanzo vya maji vikubwa, kama vile Bahari ya Hindi na maziwa, kutokana na shughuli za kibinadamu. Uchafu huu unaathiri mazingira, afya ya wanadamu na wanyama, na ustawi wa uchumi wa

taifa, hasa katika maeneo ya pwani na visiwa. Serikali ifanye usafi kwenye bahari na maziwa (water bodies) ili kuongeza ufanisi wa bahari, mito na maziwa, ili kuboresha uchumi wa buluu.

xxvii. Ufinyu wa ushirikishwaji wa makampuni ya ndani: Changamoto ya makampuni ya ndani kushindwa kushirikishwa ipasavyo katika shughuli za kiuchumi, miradi mikubwa, na masoko. Hii inatokana na vikwazo mbalimbali vinavyozuia makampuni ya ndani kushiriki katika biashara kubwa au mikataba na serikali na sekta binafsi. Tunashauri serikali iboreshe sheria ya local content, iweze kushirikisha makampuni ya ndani, na pia kutoa malipo kwa wakati kwa makampuni yaliyoshinda zabuni ili yaweze pia kulipa wafanyakazi wao kwa wakati.

xxviii. Uhaba wa maeneo maalumu ya kuzalisha bidhaa katika eneo maalumu la kiuchumi: Serikali na taasisi za kiuchumi hazijapanga maeneo maalumu kwa ajili ya viwanda na uzalishaji wa bidhaa, hivyo kuchangia uchanganyiko wa matumizi ya ardhi na kushindwa kubainisha maeneo ya kiuchumi. Tunashauri serikali kutengeneza mpango maalumu wa kuweka maeneo maalumu ya kiuchumi ya uzalishaji wa bidhaa (Special Economic Zones - SEZ) kwa ajili ya usafirishaji (export), mfano maeneo ya Songwe na Rukwa yanaweza kuwekwa kama SEZ kwa ajili ya kulenga nchi ambazo hazina bahari kama DRC, Rwanda, Burundi, Zambia, Malawi, Afrika ya Kati na Zimbabwe.

xxix. Ukosekanaji wa maeneo maalumu ya kuuza bidhaa za madini: Changamoto ya kutokuwepo kwa maeneo rasmi na maalumu ambapo biashara ya madini inaweza kufanyika kwa urahisi, kwa usalama, na kwa ufanisi, ikiwa ni pamoja na soko la kutosha kwa bidhaa za madini kama dhahabu, almasi, na madini mengine. Tunapendekeza serikali itenge maeneo maalumu ya kuuza bidhaa za madini yatakayowavutia wanunuzi kutoka dunia nzima. Kwa mfano, serikali ingeweza kujenga katika mkoa wa Geita soko la kimataifa la kuuza madini yote (dhahabu, tanzanite, diamond, rubi n.k.) ambayo yameongezwa thamani. Pia tunashauri vijana wapelekwe kujifunza uongezaji thamani wa madini yetu yote. Vilevile tunaweza kuajiri wataalamu wa kuongeza thamani.

xxx. Kutojitosheleza kwa tafiti za mazao ya kilimo: Changamoto ya kukosekana kwa tafiti za kina, sahihi, na za kisasa ambazo zinahusu mazao ya kilimo, na zinazoweza kusaidia wakulima kuboresha uzalishaji na kukabiliana na changamoto mbalimbali za kilimo. Tunashauri serikali kuwekeza zaidi kwenye tafiti zitakazowezesha kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mazao ya kilimo ili kufikia viwango vya kimataifa. Hii ni kwa mazao yote kama mpunga, korosho, mahindi, maharage n.k.

xxxi. Changamoto kwenye mfumo wa ufugaji wa mifugo: Matatizo yanayokwamisha ukuaji na ufanisi wa sekta ya ufugaji wa mifugo nchini. Changamoto hizi zinahusiana na mbinu duni za ufugaji, ukosefu wa rasilimali, na vikwazo vya kiutawala na kifedha. Serikali kupitia Wizara ya Mifugo itengeneze mfumo mzuri wa kufuatilia ufugaji wa wanyama, kwa mfano ng'ombe wengi wa Tanzania wanachukua zaidi ya miaka 8 hadi 15 kuweza kufika kilo 400 za kuuzwa nje, wakati wenzetu wa nchi kama Brazil ng'ombe huyo huchukua miezi 8 kufika kilo hizo 400. Hivyo ni lazima tuwe na juhudi kubwa na tubadili mfumo wote wa ufugaji Tanzania ili tuweze kushindana na kuongeza pato la taifa.

## 4.2. Mapendekezo kwa serikali za mitaa

Mapendekezo ya serikali za mitaa yanalenga kuboresha utawala wa maeneo ya ndani ili kuimarisha huduma kwa wananchi, kuongeza uwazi, na kuhamasisha ushiriki wa jamii katika maamuzi yanayowahusu. Serikali za mitaa zina jukumu muhimu katika kutekeleza sera na miradi inayoboresha maisha ya wananchi katika ngazi ya chini, huku zikisaidia kufikisha huduma za msingi kama elimu, afya, maji, na miundombinu kwa ufanisi zaidi. Mapendekezo haya yanalenga kuboresha ufanisi wa serikali za mitaa kwa kuimarisha ushirikiano kati ya serikali kuu na za mitaa, kuongeza rasilimali, na kuunda mifumo ya kisasa ya usimamizi inayowezesha uwazi na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma. Mapendekezo hayo kumi na tano (15) ni kama ifuatavyo:

i. Ufahamu mdogo wa fursa za uwekezaji kwenye mikoa ya Tanzania: Wawekezaji na wananchi wanakosa kujua fursa tofauti zilipo kwenye mikoa yote ya Tanzania ili waweze kuongeza uwekezaji.

Tunatoa rai kwa serikali za mikoa, kwa kushirikiana na TNCC katika mikoa yao pamoja na wadau muhimu, washirikiane katika kutangaza fursa za biashara na uwekezaji katika mikoa yao.

ii. Kutokuwa na miundombinu mizuri kwenye soko la vitunguu Singida, Soko la Manzese mkoani Ruvuma na soko la Tanga. Soko la vitunguu Singida halina miundombinu ya kuwakinga wafanyabiashara na wateja wa kimataifa dhidi ya jua/mvua.

a. Halmashauri ya Manispaa ya Singida iboreshe miundombinu ya soko kukidhi hadhi ya "kimataifa" ya soko la vitunguu la Misuna (Mkoa wa Singida).

b. Inapendekezwa kuwa serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Singida ijenge miundombinu inayoendana na hadhi ya soko pamoja na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii (maji safi, chakula, maliwato n.k.) ambazo kwa sasa haziridhishi. Soko hili likiimarishwa litachochea upatikanaji wa mapato serikalini.

c. Halmashauri ya mji wa Songea inashauriwa kuharakisha mchakato wa ukarabati wa soko la Manzese mkoani Ruvuma ili kusaidia wafanyabiashara waendelee na shughuli zao.

d. Serikali inashauriwa kumaliza ujenzi wa soko la Tanga (maeneo ya Kange) ili wafanyabiashara wapate soko rasmi la kufanyia shughuli zao.

iii. Changamoto ya fursa za uwekezaji na uhamasishaji: Uhaba wa taarifa za wazi na za kina kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta mbalimbali, jambo linalosababisha wawekezaji kutokuwa na ufahamu wa fursa zinazopatikana.

a. Serikali ikishirikiana na sekta binafsi inashauriwa kuainisha fursa za uwekezaji na kuhamasisha uwekezaji kwenye maeneo ya fursa hizo, kwa mfano ufinyu wa viwanda vya kuchakata malighafi zipatikanazo mkoani Kagera kama nyama (samaki, ng'ombe, mbuzi, kondoo) na maziwa hazichakatwi kuongezewa thamani sokoni.

b. Serikali inashauriwa kuwekeza katika miundombinu ya uokoaji baharini na katika Mto Rufiji katika halmashauri ya Bagamoyo,

Rufiji na kwingineko ili kusaidia wafanyabiashara nyakati za majanga.

iv. Utofauti wa ushuru wa mazao (produce cess) katika halmashauri: Baadhi ya halmashauri huweka viwango vya juu kwenye tozo za gunia la mpunga (ushuru wa mazao - produce cess), kwa mfano Halmashauri za Malinyi na Mlimba. Viwango vya tozo hizo vya asilimia 3 vishushwe kulingana na uhalisia wa wafanyabiashara wa wilaya hizo.

v. Tuhuma kwa baadhi ya washauri wa kodi (Tax Consultants): Changamoto hii imelenga baadhi ya washauri wa kodi kutokuwa waaminifu. Hivyo serikali inashauriwa kuboresha udhibiti kwa washauri wa kodi (kupitia NBAA na TRA), kuwadhibiti washauri wa kodi (Tax Consultants) ili kukomesha wafanyabiashara wasio waaminifu katika kuwasilisha ritani na kusababisha serikali kupoteza mapato ya kodi.

vi. Malalamiko ya wachimbaji wadogo wa madini: Kuna malalamiko kuwa wachimbaji wadogo wa madini wanakandamizwa katika haki za uchimbaji pale mwekezaji mkubwa akijitokeza.
Serikali iendelee kuweka msisitizo wa kusimamia masharti yaliyopo kwenye mikataba ya uchimbaji wa madini kama sheria inavyowataka.

vii. Kutokupewa nafasi kwa utalii wa kitamaduni: Utalii wa kitamaduni (Cultural Tourism) haujapewa kipaumbele, kwa hiyo nchi inakosa fursa kubwa ya kiuchumi.

a. Serikali inashauriwa kuwekeza nguvu katika utalii wa kitamaduni (Cultural Tourism).

b. Wafanyabiashara wanashauriwa kuwekeza kwenye sekta hii ya utamaduni.

viii. Mabadiliko ya gharama za huduma katika sekta ya afya: Mabadiliko ya gharama za huduma katika sekta ya afya kupitia NHIF na mifumo mingine ya bima yana athari kubwa kwa upatikanaji wa huduma na ustawi wa wanachama, na yanahitaji usimamizi mzuri ili kuleta uwiano kati ya gharama na ubora wa huduma zinazotolewa.

Wizara ya afya inashauriwa kupitia upya gharama za huduma katika sekta ya afya. Mfano: Sekta ya afya katika bango kitita la NHIF: Kushusha bei ya upasuaji wa akina mama wajawazito kutoka laki 3

hadi laki 1 bila kuwashirikisha wadau husika kunaleta ugumu kwa watoa huduma hizo.

ix. Changamoto ya miundombinu hafifu ya usafirishaji wa malighafi na minofu: Kujaa kwa maji ya Ziwa Viktoria na kuharibu barabara zinazoelekea kiwandani Supreme Perch Mkoani Kagera.

   Serikali inashauriwa kuboresha miundombinu ya barabara iendayo Supreme Perch kilomita 3 kutoka njia panda ya uwanja wa ndege hadi kiwandani ili kuboresha mapato ya kodi yatokanayo na kiwanda hicho.

x. Utozwaji wa tozo na ushuru kwa wavuvi Mkoani Mara: Wavuvi Mkoani Mara wanalalamikia tozo na ushuru vinavyotozwa bila mpangilio. Tozo hizo hazina uwiano kati ya wilaya moja na nyingine.

   Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI ioanishe ushuru wa bidhaa zinazofanana kutoka halmashauri moja kwenda nyingine ili kuweka ushindani sawa wa bidhaa zinazoenda kwenye soko moja.

xi. Kutopewa kipaumbele wadau wa madini Mkoani Mara na Chunya: Wadau wa madini Mkoani Mara na Chunya wanalalamikia tozo zitokanazo na sheria ndogondogo (by-laws) zinazokinzana na sheria mama za madini.

   Serikali inashauriwa ifanye mapitio ya tozo za madini zinazotozwa na halmashauri za Mara na Chunya kwani zinawaumiza wachimbaji.

xii. Uchakavu wa miundombinu ya maeneo ya biashara Wilayani Same Mkoani Kilimanjaro: Soko la Same lina changamoto ya miundombinu ya barabara, maji safi na taka n.k.

   Serikali kupitia ofisi za Halmashauri ya Same iboreshe miundombinu ya maeneo ya biashara kwani ni chakavu.

xiii. Kutokuwa na ufanisi wa vikundi vya kisekta vya vijana nchini: Vikundi vya kisekta vya vijana nchini, mfano: vilivyopo Mkoani Manyara, havina ufanisi. Vikundi hivyo viwezeshwe viwe na ufanisi ili viweze kukopesheka kupitia Halmashauri husika na vitumie fedha hizo kwa ufanisi.

a. Halmashauri zifanye tathmini yakinifu ya vikundi vya kisekta vya vijana nchini kwani vingi siyo fanisi, mfano: vilivyopo Mkoani Manyara. Lengo ni kuboresha biashara ndogo, za kati na za vijana.

b. Serikali inashauriwa kutumia ofisi za TNCC katika kuwachuja na kuwachagua vijana wanufaika wa mikopo ili kuongeza ufanisi wa malengo ya mikopo hiyo.

xiv. Muundo wa mabaraza ya biashara ya wilaya na mikoa: Serikali inashauriwa kurudisha muundo wa zamani wa mabaraza yote ya biashara, ambapo wenyeviti wa TNCC wa wilaya na mikoa walikuwa wenyeviti wenza wa mabaraza ya wilaya na mikoa.

xv. Kutumia kwa ukamilifu maeneo ya viwanda (industrial parks): Katika miji mikubwa kama Dar es Salaam kuna changamoto ya viwanda kuanzishwa katika maeneo ya makazi. Viwanda hivi si tu vinasababisha uchafuzi wa mazingira katika makazi ya watu, ila pia vinakosa huduma maalum za viwanda kama umeme mkubwa unaotosheleza viwanda, maji ya uhakika na barabara zenye uwezo wa kuhimili uzito mkubwa wa magari makubwa.

Tunapendekeza uongozi wa manispaa jijini Dar es Salaam uwaelekeze wawekezaji wa viwanda kwenda maeneo ya viwanda yaliyotengwa maalum katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa jirani wa Pwani. Mkoani Pwani kuna industrial parks kama vile Modern Industrial Park iliyoko Mlandizi wilayani Kibaha, ambayo ina miundombinu yote ya kutosha kwa viwanda vya aina mbalimbali. Ukaribu wa Modern Industrial Park na bandari ya Dar es Salaam pamoja na barabara kuu ya Dar es Salaam–Morogoro unafanya maeneo haya ya viwanda kuwa muafaka zaidi.

## 4.3. Mapendekezo ya sera

Mapendekezo ya sera yanahusu mawazo na hatua za kimkakati zinazolenga kuboresha mifumo, kubuni mbinu mpya, au kurekebisha sera zilizopo ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika jamii au sekta mbalimbali. Sera bora ni msingi wa maendeleo endelevu, na ndiyo njia ambayo serikali na taasisi mbalimbali hutumia kufanikisha malengo ya kijamii na kiuchumi kwa ufanisi zaidi. Mapendekezo haya yameundwa kwa kuzingatia

uchambuzi wa kina wa takwimu, uzoefu wa nchi nyingine, na mitazamo ya wataalamu, ili kutoa mwelekeo wa sera zinazokidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye.

Kwa kuongeza uwazi, uwajibikaji, na kushirikisha wadau mbalimbali katika mchakato wa uundaji wa sera, mapendekezo haya yanatarajiwa kuongeza ufanisi wa utekelezaji wake, kuboresha maisha ya wananchi, na kusaidia kufikia malengo ya kitaifa kwa ustawi wa jamii na uchumi kwa ujumla. Majumuisho ya mapendekezo kumi na saba (17) kwenye sera yameorodheshwa hapo chini.

i. Changamoto ya mfumo wa stakabadhi ghalani: Mfumo una mapungufu ya kutotoa uwazi wa bei za mazao husika mapema kwa wakulima. Mapendekezo ya sera kuhusiana na mfumo wa stakabadhi ghalani:

    a. Serikali kupitia wizara ya kilimo ipitie upya michakato na mfumo mzima wa stakabadhi ghalani kwa manufaa ya wafanyabiashara na kwa manufaa ya nchi.

    b. Serikali iweke kima cha chini cha bei ya mazao na kuja kuwalipa wakulima hao fidia ("mabaki") baada ya mazao hayo kuuzwa kwenye soko la dunia.

    c. Serikali imruhusu mkulima kuleta mteja mwenye bei nzuri ghalani ili mazao yaweze kuuzwa kwa bei nzuri na kwa wakati kwa manufaa ya mkulima na nchi.

    d. Serikali itumie mfumo wa risiti (warehouse receipt system) kwa wakulima ili waweze kuitumia kupata fedha kutoka kwenye vyanzo vingine wakati serikali ikiendelea kutafuta masoko (Wizara ya Kilimo).

ii. Changamoto ya ushuru wa huduma (Service Levy): Kiwango cha ushuru kinatofautiana kati ya wilaya na wilaya, jambo ambalo linawapa changamoto wafanyabiashara wanaofanya kazi kwenye maeneo mbalimbali. Hii inaweza kufanya baadhi ya maeneo yawe na ushindani mdogo wa kibiashara. Kutatua changamoto ya ushuru wa huduma (Service Levy):

Pamoja na serikali kufanya maboresho ya ushuru wa huduma kutoka asilimia 0.3 hadi asilimia 0.25 kwenye mwaka wa fedha 2025/2026, bado ushuru huu ni mkubwa, hivyo:

a. Serikali inashauriwa kufuta ushuru wa huduma kwa sababu msingi wake ni sawasawa na kodi ya mapato. Sambamba na hilo, ushuru wa huduma unaongeza gharama za biashara na uzalishaji.

b. Mbadala, serikali inashauriwa kubadilisha sheria ili ushuru wa huduma utozwe kwenye faida badala ya mapato ghafi.

c. Kwa mkakati wa muda mfupi, serikali inashauriwa kupunguza ushuru wa huduma kutoka 0.25% mpaka 0.1% ya mapato ghafi sambamba na kuongeza wigo wa walipa ushuru.

iii. Kutokukidhi uhalisia kwa wajumbe wa ofisi ya msuluhishi wa masuala ya kodi: Wajumbe wa ofisi ya msuluhishi wa masuala ya kodi hawakidhi uhalisia kwa dhumuni la chombo hicho. Kwa sasa, wadau wa sekta binafsi siyo wajumbe wa chombo hicho muhimu. Suluhisho kwa wajumbe wa ofisi ya msuluhishi wa masuala ya kodi kutokidhi uhalisia kwa dhumuni la chombo hicho: Vitu vifuatavyo vifanyike:

a. Tunapendekeza ofisi ya msuluhishi wa malalamiko na taarifa za kodi iundiwe sheria inayojitegemea tofauti na sasa, ambapo uanzishwaji wa taasisi hii umetajwa kwenye sheria ya usimamizi wa kodi CAP 438 REV 2019 katika kifungu cha 28.

b. Halikadhalika, ofisi ya msuluhishi iwe na nguvu ya kusikiliza changamoto za kiutendaji zilizojitokeza hata baada ya 'tax decision' kutolewa na Kamishina Mkuu. Kwa sasa, sheria hairuhusu kushughulikia mashauri yaliyo kwenye hatua ya tax decision.

c. Pia, chombo hicho kishirikiane na sekta binafsi kutoa taarifa na elimu ya shughuli zake kwa umma kwa manufaa ya walipa kodi.

iv. Changamoto ya wadau wa sekta ya misitu (Commercial Plantation): Wadau wa sekta ya misitu kutozwa tozo za kupanda miti. Kwa mujibu wa GN namba 387 ya tarehe 14/05/2021 chini ya "The Environmental Management Act" CAP 191, inaelekeza kulipa tozo ya shilingi 50,000/= kwa kila ekari 50 kwa wapandaji wa misitu.

   a. Serikali ipitie tozo ya upandaji wa misitu kwa sababu upandaji wa misitu ni mojawapo ya utunzaji wa mazingira; kuweka tozo isiyo rafiki imeongeza gharama za uzalishaji na hivyo kupelekea wawekezaji kwenye sekta ya misitu kupunguza upandaji wa miti.

   b. Pia, serikali iwekeze kwenye mfumo wa kupokea malipo ya kupunguza hewa ukaa (Carbon Credit) ili kuongeza kunufaika kwa wawekezaji hao wa misitu.

v. Ukubwa wa tozo ya Skills Development Levy (SDL): SDL ni kubwa na kandamizi kwa waajiri, hivyo mapendekezo yafuatayo yazingatiwe:

   Serikali iendelee kupunguza kiwango cha Skills Development Levy (SDL) kutoka 3.5% kwenda 2% ya payroll ili kufikia kiwango ambacho kinapendekezwa na shirika la ILO (2%) na kupunguza mzigo kwa waajiri.

vi. Changamoto ya sera za uwekezaji: Sera za uwekezaji zinatumika ndani ya miezi 12–18 tu. Hali hii haiwavutii wawekezaji wakubwa ambao wanataka waweke miradi nchini kwa kipindi kikubwa zaidi.

   Kwenye uwekezaji wa kimkakati, serikali inashauriwa kuweka sera zinazotabirika na za muda mrefu kuanzia angalau miaka 3 ili kuendelea kuchochea uwekezaji wa ndani.

vii. Kiwango cha chini cha mauzo cha kusajiliwa VAT: Mapendekezo ya kiwango cha chini cha mauzo cha kusajiliwa VAT ni ifuatavyo:

   a. Serikali inashauriwa kuongeza kiwango cha VAT threshold kutoka TZS millioni 200 mpaka TZS millioni 500.

   b. Serikali inashauriwa kuweka utaratibu wa refund wa VAT kwa walaji wa mwisho ili kuchochea walaji wa mwisho kudai risiti za kielektroniki na hivyo kuongeza mapato ya kodi yatokanayo na VAT. Pendekezo hili likichukuliwa litakuwa ni motisha (incentive) ya wateja kudai risiti, kwa mfano: Mfumo wa marejesho wa VAT

wa Afrika ya Kusini (https://www.gov.za/services/services-organisations/tax/custom-duties/apply-vat-refund): Ambayo inaruhusu hata wafanyabiashara wa kigeni kupata "VAT refund". Nchini Marekani, fursa ya kudai marejesho ya VAT kwa ujumla ni kwa ajili ya wafanyabiashara wa kigeni na watalii ambao wamepata VAT kwenye gharama zinazostahiki ndani ya nchi zinazotoza VAT. Wafanyabiashara wa Marekani pia wanaweza kuomba marejesho ya VAT kutokana na gharama zao za kibiashara katika nchi hizo.

viii. Changamoto ya gharama zinazotozwa na taasisi ya urekebu ya OSHA: Gharama kubwa zinazotozwa na taasisi ya urekebu ya OSHA kwenye kupima wafanyakazi na gharama za ukaguzi na mafunzo.

a. Serikali inashauriwa kupunguza gharama za OSHA kwa kiwango cha asilimia 60 kama ifuatavyo:

- Normal check up: Tshs 20,000 kwa kila mfanyakazi – inapendekezwa Tshs 8,000 kwa kila mfanyakazi

- Vision test: Tshs 15,000 kwa kila mfanyakazi – inapendekezwa Tshs 6,000 kwa kila mfanyakazi

- Audiometry: Tshs 15,000 kwa kila mfanyakazi – inapendekezwa iwe Tshs 6,000 kwa kila mfanyakazi

- Lung function test: Tshs 25,000 kwa kila mfanyakazi – inapendekezwa Tshs 10,000 kwa kila mfanyakazi

b. Mbadala, majukumu ya kupima afya za wafanyakazi yafanywe na hospitali za serikali ngazi ya wilaya.

ix. Malalamiko ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT): Wazabuni wanalazimika kulipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya bidhaa na huduma walizotoa kabla ya kupata malipo kutoka serikalini. Sheria ya VAT kifungu cha 16 ifanyiwe marekebisho ili kuondoa takwa la utoaji wa tax invoice/stakabadhi kabla ya malipo kuhesabika kama malipo yameshafanyika na hivyo kupelekea wazabuni kutakiwa kulipa VAT.

x. Elimu inayotolewa vyuo vya ufundi stadi kutokukidhi mahitaji: Sekta zinazotegemea ufundi stadi kama viwanda, ujenzi, na teknolojia zinakosa wafanyakazi wenye ujuzi wa kisasa, hivyo kushusha ufanisi na tija.

    a. Serikali inashauriwa kuandaa sera ambayo itawezesha vyuo vya ufundi stadi kama VETA kutoa elimu itakayoweza kusaidia sekta binafsi ili kuweza kuendana na soko la ajira.

    b. Vyuo vya VETA vitumike kuleta teknolojia za kisasa.

xi. Upungufu wa mpango maalumu wa kuongeza thamani bidhaa zetu: Ukosefu wa mikakati madhubuti inayolenga kuboresha na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini, ili ziweze kushindana vyema kwenye masoko ya ndani na nje.
Inapendekezwa serikali itengeneze sera nzuri ya kuweka mpango maalum wa kuongeza thamani bidhaa za nchini na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

xii. Kutokuwa na sheria imara inayosimamia “mauzo kwa mkopo” (credit sales): Hii inamaanisha mauzo ambayo mteja anapokea bidhaa au huduma na analipa baadaye badala ya kulipa papo hapo.

    Ni muhimu sana kwa serikali kuwa na sheria inayosimamia (credit sales); zabuni zisitolewe bila serikali kuwa na pesa za kutosha.

    Tunashauri kila zabuni iwe na mkataba; pia kuwe na sehemu tatu: manunuzi (serikali), bank na supplier (biashara mzabuni), na serikali itabaki na bank; hii itaokoa sana sekta binafsi.

## 4.4. Hitimisho

Kitabu hiki kimetoa taswira ya kina kuhusu hali halisi ya biashara na uwekezaji nchini Tanzania kwa kuzingatia ushahidi wa moja kwa moja kutoka kwa wadau wa sekta binafsi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kupitia tathmini hii, imeonekana wazi kuwa sekta binafsi ina mchango mkubwa na usiopingika katika kukuza uchumi wa taifa, kuongeza ajira, kupanua wigo wa uzalishaji, na kuimarisha mapato ya serikali. Hata hivyo, mchango huu

unaweza kuongezeka zaidi iwapo mazingira ya biashara na uwekezaji yataimarishwa kwa njia jumuishi, thabiti na endelevu.

Tathmini imeonesha kuwa Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi za kiuchumi, nafasi ya kijiografia yenye fursa za kibiashara kikanda na kimataifa, pamoja na nguvu kazi kubwa. Fursa hizi zinaonekana dhahiri katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, biashara ya mipakani, madini na huduma. Ikiwa zitaunganishwa vyema na sera bora, miundombinu imara, na uwekezaji wa kimkakati katika uongezaji thamani, sekta hizi zinaweza kuwa mhimili mkuu wa mapinduzi ya kiuchumi yanayolenga uchumi shindani na jumuishi.

Pamoja na fursa hizo, changamoto zilizobainishwa katika kitabu hiki zinaonesha hitaji la maboresho ya haraka na ya kimkakati. Wingi wa kodi, tozo na ada mbalimbali, tafsiri zisizo sawia za sheria na kanuni, urasimu katika utoaji wa huduma, pamoja na ucheleweshaji wa maamuzi na malipo, vinaongeza gharama za kufanya biashara na kupunguza ushindani wa bidhaa na huduma za Tanzania. Aidha, upungufu wa miundombinu bora ya uzalishaji na usafirishaji, gharama za nishati, na upatikanaji mdogo wa mitaji nafuu vinaendelea kuwa vikwazo vikubwa kwa ukuaji wa sekta binafsi, hususan kwa biashara ndogo na za kati.

Maoni ya wadau pia yamebainisha umuhimu wa kuimarisha uratibu kati ya taasisi za serikali katika ngazi za kitaifa na za mitaa. Kukosekana kwa uwiano katika utekelezaji wa sera na kanuni kati ya maeneo tofauti kumeongeza mkanganyiko na kutengeneza mazingira yasiyotabirika kwa wawekezaji na wafanyabiashara. Hivyo, hitaji la kuoanisha mifumo ya kodi, leseni, tozo na taratibu za kiudhibiti ni la msingi ili kujenga mazingira ya biashara yenye haki, uwazi na utabirikaji.

Kwa upande mwingine, tathmini imeonesha kuwa kuna mwamko na utayari mkubwa wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika mikoa mingi. Mikutano na majadiliano kati ya TNCC, viongozi wa serikali na wafanyabiashara imeweka msingi mzuri wa majadiliano ya pamoja kuhusu suluhisho la changamoto zilizopo. Huu ni mtaji muhimu wa kijamii na kitaasisi ambao unapaswa kuendelezwa kupitia majukwaa ya mara kwa mara ya majadiliano, ubia wa maendeleo, na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika mchakato wa uundaji na utekelezaji wa sera.

Kitabu hiki pia kimeonesha umuhimu wa kuimarisha taasisi za uwakilishi wa sekta binafsi kama TNCC ili ziweze kukusanya na kuwasilisha hoja za wafanyabiashara kwa ufanisi zaidi. Uwezo wa Chemba katika ngazi za mikoa

na wilaya unahitaji kuongezwa ili iweze kutoa huduma bora kwa wanachama, kufanya tafiti za mara kwa mara, na kushiriki kikamilifu katika mijadala ya maendeleo ya kiuchumi ya maeneo husika. Hii itahakikisha kuwa sauti ya sekta binafsi inasikika ipasavyo katika ngazi zote za maamuzi.

Kwa ujumla, hitimisho kuu la kitabu hiki ni kwamba Tanzania ina msingi mzuri wa kukuza biashara na uwekezaji, lakini mafanikio ya juhudi hizi yatategemea kasi na uthabiti wa maboresho ya sera, mifumo na miundombinu. Utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa, ikiwemo kurahisisha taratibu za kibiashara, kupunguza mzigo wa tozo na urasimu, kuimarisha miundombinu ya uzalishaji na masoko, pamoja na kujenga uaminifu na ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi utakuwa hatua muhimu kuelekea mazingira bora zaidi ya biashara.

Mwisho, kitabu hiki kinatoa wito kwa wadau wote (serikali, sekta binafsi, taasisi za fedha, washirika wa maendeleo na jamii kwa ujumla) kuchukua hatua za pamoja katika kutekeleza mapendekezo yaliyowasilishwa. Kupitia ushirikiano, uwazi na dhamira ya pamoja, Tanzania inaweza kujenga mazingira ya biashara na uwekezaji yanayochochea ukuaji jumuishi wa uchumi, kuongeza ajira kwa vijana na wanawake, na kuinua ustawi wa wananchi wa vizazi vya sasa na vijavyo. Hili ndilo dira kuu ya maendeleo endelevu ambayo kitabu hiki kinahamasisha.